# Mafunzo ya Haki za Binadamu kwa jeshi la Polisi – Tanzania



# MWONGOZO WA MKUFUNZI

**IMEANDALIWA NA:**

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU
BARABARA YA OCEAN
JENGO LA TULYER, GOROFA YA 2
S.L.P. 75254
Dar es Salaam, TANZANIA

Simu: 255-051-113177, 117768, 118353
Fax: 255-051-113177
Email: lhrctz@raha.com

HRE/ED/6/swa/1

18925

**YALIYOMO** .................... i

**DIBAJI** .................... ii
**UTANGULIZI, MWONGOZO, MADHUMUNI NA WATUMIAJI** .................... iv
- Mwongozo unahusu nini? .................... iv
- Sababu za kuwalenga polisi .................... iv
- Namna ya kuutumia mwongozo .................... v
- Muundo wa mwongozo .................... vi

## *SEHEMU YA 1*

**SURA YA KWANZA**
HAKI ZA BINADAMU NA UTEKELEZAJI WA SHERIA .................... 1
KAZI ZA POLISI KATIKA DEMOKRASIA .................... 5

## *SEHEMU YA 2*

**SURA YA PILI**
KUKAMATA .................... 16

**SURA YA TATU**
UCHUNGUZI WA POLISI .................... 28

**SURA YA NNE**
KUWEKA KIZUIZINI .................... 36

**SURA YA TANO**
KUTUMIA NGUVU NA SILAHA .................... 46

**SURA YA SITA**
KAZI ZA POLISI NA USALAMA WA UMMA (RAIA) .................... 53

**SURA YA SABA**
KAZI ZA POLISI NA HAKI ZA MAKUNDI MAALUM NA
WAATHIRIKA WA UKIUKWAJI WA HAKI ZA BINADAMU .................... 65

**SURA YA NANE**
KAZI ZA POLISI NA HAKI ZA WAKIMBIZI NA RAIA WAGENI (WASIO RAIA) ....... 85

**SURA YA TISA**
HAKI ZA BINADAMU KATIKA UTAWALA, AMRI NA UONGOZI WA POLISI .......... 96

## *SEHEMU YA 3*

**SURA YA KUMI**
UFUATILIAJI NA TATHMINI .................... 99

## *SEHEMU YA NNE*

**Viambatanisho**
Orodha ya mikataba ya kimataifa ya haki za Binadamu na sheria za nchi. ....... 103
Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu. .................... 106
Misingi muhimu ya watekelezaji wa sheria. .................... 112

LIBRARY - BIBLIOTHEQUE OHCHR



HRF/TD/6 kiswa/1

# DIBAJI

Ni ukweli ulio dhahiri, kwamba katika baadhi ya duru za utekelezaji wa sheria hasa katika demokrasia changa, heshima kwa haki za binadamu inaonekana kama pingamizi katika kutekeleza sheria kwa ufanisi. Hii falsafa iliyopitwa na wakati na isiyo na misingi ni kigezo kinachotumiwa na vyombo vya utekelezaji wa sheria "kupinda taratibu kidogo" wakati wakikabili uhalifu.

Ni imani hiyohiyo inayosababisha matumizi ya nguvu katika kupata habari toka kwa mahabusu, kutumia nguvu kupita kiasi katika kukamata watuhumiwa wa uhalifu, kuwanyima watu dhamana na kutumia nguvu kupita kiasi na silaha kuzuia maandamano. Hivi vitendo vya polisi vinakiuka utawala wa kisheria. Sana sana vinageuza kazi za polisi kutoka kusimamia na kukuza utawala wa sheria, kuwa ni wakala wanaosimamia uvunjaji wa utawala huo wa sheria. Hakika hali hii ni tatizo kubwa ambalo misingi yote ya haki za binadamu pamoja na katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatafuta kuliondoa. Kufuatana na hali hii, ni vyema kunukuu utangulizi wa Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu.

*"Pamoja na kwamba inamlazimu binadamu anapokosewa haki zake kwa udhalimu na ukandamizaji kuamua kupambana, bado ni lazima haki za binadamu zilindwe na sheria".*

Kwa lugha hiyo, utangulizi huo hapo juu, unaelezea sababu au haja ya kusambaza ufahamu wa Haki za Binadamu kwa watekelezaji wa sheria. Sababu ni njema tu; nayo ni kuhakikisha uwepo wa amani, utulivu na usalama. Katika kusisitiza haya Mwana Tume ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Binadamu anatamka:

*"Bila kutunza utawala wa sheria, ukiukwaji wa haki hutokea na upinzani huandaliwa. Matokeo yake hayaepukiki: Ukiukaji wa haki za binadamu hauwezi kuchangia katika kulinda utulivu na usalama, bali unaweza tu kuongeza kudidimia kwake. Huu ujumbe hadi sasa inabidi uonekane bayana. Kwa Umoja wa Mataifa hakuna kilicho wazi zaidi ya ukweli huu".*

Ukweli huu ndio umechangia katika dhumuni pana la Umoja wa Mataifa na mashirika na taasisi katika nchi kuingia katika ufundishaji wa Haki za Binadamu kwa watekelezaji wa sheria ili kukuza utawala wa sheria katika utu wa mtu. Utu wa mtu ndio kigezo katika kulinda amani, utulivu na maendeleo ya mwanadamu.

Hata hivyo kufundisha haki za binadamu kwa watekelezaji wa sheria hakulengi tu katika kuwaelekeza kurejea katika kutekeleza kazi zao kwa mujibu wa sheria na maadili ya kazi bali pia kuhakikisha utekelezaji ulio bora wa kazi yao. Hakika, mafanikio yafuatayo

katika mfumo wa utekelezaji wa sheria yanaweza kuhusianishwa na heshima na uzingatiaji wa haki za binadamu utakaofanywa na watekelezaji wa sheria:

- Askari polisi hawataonekana kama "walinzi wa dola" bali kama sehemu ya jumuiya wakitoa huduma zenye manufaa kwa jamii.
- Askari polisi watakuwa karibu na raia na watajenga ushirikiano (na raia) ambao utafanya kazi na majukumu yao kuwa ya mafanikio zaidi kwa vile utakua ni upolisi wenye mwelekeo wa kupata mafanikio zaidi.
- Kazi ya kuendesha mashtaka itakuwa na mafanikio daima mahakamani jambo ambalo linaweza likapunguza uhalifu.
- Jeshi la polisi linaweza kutoa njia nyingine ya amani katika kutatua migogoro na malalamiko.

Kwa ujumla, kama serikali na raia wanahitaji kufanikiwa katika madhumuni ya utekelezaji wa sheria na kuwa na mfumo wa utekelezaji wa sheria usiotegemea woga wa watu, bali heshima, matumizi ya taaluma na sheria, basi hawawezi kuepuka changamoto ya kuwafundisha watekelezaji wa sheria haki za binadamu.

Mwongozo wa Haki za Binadamu kwa polisi umeandaliwa ili kutoa maelezo na mbinu muafaka kwa mkufunzi wa Haki za Binadamu kwa watekelezaji wa sheria hususan Polisi wa Tanzania. Mwongozo huu unatarajiwa kuwa nyenzo katika elimu ya Haki za Binadamu kwa Polisi wa Tanzania

**Na: Helen Kijo-Bisimba**
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU**

# UTANGULIZI

## Mwongozo, Madhumuni na Watumiaji

### Mwongozo unahusu nini?

Mwongozo huu unakusudiwa kuwa kiongozi na nyenzo kwa wakufunzi wa Haki za Binadamu kwa watekelezaji wa sheria. Watekelezaji wa sheria waliolengwa ni Polisi. Mwongozo huu basi, utatoa maelekezo juu ya namna mafunzo yanavyoweza kuendeshwa. Aidha mada za mafunzo zimetolewa kiasi kwa matumizi ya mkufunzi. Kama nyenzo ya utendaji kwa mkufunzi, mwongozo unatilia maanani ukweli unaojitokeza katika hali halisi ya kazi za polisi Tanzania, pamoja na mfumo wa sheria. Haya mawili yanaoanishwa na kupata muafaka katika katiba ya nchi na vipimo vya haki za binadamu vya kimataifa. Mwongozo huu unasimama kama nyenzo ya kukuza uwezo kwa mkufunzi yeyote wa haki za binadamu katika **eneo hili Tanzania wakati vilevile** mada zilizopo zinaweza kutumiwa na wanafunzi.

### Sababu za kuwalenga Polisi

Polisi ni watekelezaji wa sheria wanaofanya kazi na watu. Katika kazi yao wanapaswa kuangalia kwa makini haki za watu hata kama ni wahalifu, waathirika wa uhalifu au raia wa kawaida. Mtaala wa Jeshi la Polisi unaotumika kufundisha polisi haukuingiza haki za binadamu kama sehemu (ndani) ya kila kinachofundishwa. Kiutendaji katika matukio kadhaa polisi wamekuwa wakikiuka haki za watu bila kutambua kuwa wanazikiuka. Mwongozo huu una lenga mafunzo ya polisi kwa sababu maalum ambazo inabidi zifikiwe baada ya kutumia mwongozo huu kwa walengwa:

1. Kujenga uelewa wa vipimo vya Haki za Binadamu kwa maofisa wa polisi.
2. Kuwahamasisha watekelezaji hao wa sheria katika jukumu lao la kulinda haki za binadamu na heshima kwa njia ya kulinda na kukuza haki za binadamu
3. Kujenga na kukuza uwezo wa waalimu na wakufunzi wa polisi Tanzania ili waweze kuendesha mafunzo ya haki za Binadamu kwa maofisa wa polisi wanaofanya mafunzo ya awali, chuoni na mafunzo ya kujiendeleza.
4. Kuwezesha uanzishwaji wa sera na mipango katika jeshi la polisi, kwa lengo la kufanikisha uzingatiaji wa Haki za Binadamu kikamilifu katika kazi za polisi.
5. Kubadilisha mfumo wa utekelezaji wa sheria Tanzania kutoka katika hali ya kuwa chombo cha mabavu cha serikali hadi kuwa chombo cha huduma ya umma ili kiweze kufanikisha dhumuni lake jema la awali.
6. Kuwawezesha maafisa wanaotekeleza sheria kufanya kazi yao ya upolisi kwa ufanisi na uhalali kwa kuzingatia katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na vipimo vya kimataifa vya Haki za Binadamu.
7. Kurejesha imani ya watu kwenye Jeshi la Polisi la Tanzania ili kufanya watu washirikiane nalo, jambo ambalo ni kigezo muhimu katika ufanisi wa kazi za jeshi hilo.

## Chimbuko la Mwongozo

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (ambacho tutakiita Kituo kwa ufupi) kilipata mvuto wa kuwa na nyenzo kamili ya kufundishia Haki za Binadamu kwa maofisa wanaotekeleza sheria kutoka kwenye mpango wa kituo wa kufundisha polisi uliotekelezwa mwaka 1996. Vilevile habari ambazo kituo kilipata wakati wa kufundisha raia wa kawaida, zilionesha kutojua haki za binadamu kwa askari polisi wa ngazi za chini na wanamgambo, hali iliyoongezea msukumo wa kituo katika suala hili.

Wakati kituo kinatafakari kuhusu suala la mwongozo wa Haki za Binadamu kama nyenzo itakayofaa katika kuingiza uelewa wa haki za binadamu kwa watekelezaji wa sheria Tanzania, kiliwasiliana na Kituo cha Haki za Binadamu cha Denmark ambao walikuwa na mpango wa kusaidia mafunzo ya Haki za Binadamu kwa watekelezaji wa sheria Afrika, Marekani ya Kusini na Ulaya Mashariki. Kupitia mradi huo wa Kituo cha Denmark na kwa ushirikiano na Polisi Tanzania, Kituo kilichunguza mtaala wa mafunzo ya polisi na kugundua haja ya kuwa na mwongozo kwa wakufunzi. Wakufunzi wataweza kutumia mwongozo huu kufundisha polisi wanaoandaliwa katika mafunzo ya awali kwenye shule ya mafunzo ya Polisi, maafisa wa polisi wakiwa mafunzoni katika chuo cha polisi na maofisa wa polisi katika mafunzo ya kujiendeleza.

Semina ya mwanzo ya kuandaa mwongozo huu ilifanyika Copenhagen mji mkuu wa Denmark na iliandaliwa na Kituo cha Haki za Binadamu cha Denmark kuanzia tarehe 19 - 23 November, 1998. Wajumbe hutoka nchi nane zikiwemo Tanzania, Uganda, Malawi, Msumbiji, Afrika Kusini, Albania, Luthiania na Guatemala walishiriki.

Hakika habari nyingi, uzoefu na uwezo ulipatikana kutoka katika warsha hiyo na kwa kiasi kikubwa yaliyopatikana yalichangia katika kuandaa mwongozo huu. Katika warsha hiyo kila kikundi kilipanga mpango wake wa utekelezaji uliokuwa ufuatwe wakati wa kuandaa mwongozo.

## Namna ya kutumia Mwongozo

Mwongozo huu si kitabu cha kiada bali ni kiongozi cha utendaji kwa mkufunzi, kwa hiyo inategemewa kuwa mkufunzi atakuwa analielewa somo la msingi katika upolisi kama vile kukamata, kupekua, kupeleleza n.k. Mwongozo unatilia mkazo vipengele vya Haki za Binadamu katika kazi za Polisi. Mwongozo unashauri matumizi ya sanaa na kisa mkasa kama njia ya kuibua masuala. Hata hivyo, mkufunzi ana uhuru wa kutumia njia zaidi au hata njia nyinginezo kutegemeana na hali halisi na ubunifu wake. Kwa hiyo, mwongozo huu unaweza kutumiwa na wakufunzi wa polisi au mkufunzi mwingine yeyote anayetaka kufundisha polisi. Yametumiwa 'masanduku Habari' kutoa mada za sheria na mikataba ya Haki za Binadamu inayowiana na somo linalozungumziwa. Mkufunzi anashauriwa kuwa na sheria au mikataba husika katika ujumla wake kama anaweza kuipata. Mwongozo huu unaweza kutumiwa kwa pamoja na mpango wa kufundishia

ulioandaliwa na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba (unaoitwa kwa kiingereza Lesson Plan) pia mwongozo wa Umoja wa Mataifa ambao unatoa mada za mtaala wa Polisi zinazohusiana na Haki za Binadamu. Katika njia za ufundishaji mwongozo huu unafuata njia ya ushirikishwaji ambao unashauri mfumo wa kujifunza ambapo washiriki wanawezeshwa kujenga hoja kutoka katika ufahamu na uzoefu wao wa sheria na vipimo vya Haki za Binadamu. Hivyo washiriki wanashiriki katika majadiliano, sanaa, kutoa mrejesho, kuchangia mawazo wakisaidiwa na vielelezo vinavyoonekana kama picha, sinema n.k. Hata hivyo, pamekuwepo bidii ya makusudi katika kufanya mwongozo huu uwe rahisi kutumia. Kwa hali hiyo basi, lugha iliyotumika, mifano, kisamkasa vyote vinaonesha ukweli wa kijamii, utamaduni na hali za kisiasa za Tanzania.

## Muundo wa Mwongozo

Mwongozo huu una sehemu nne. Sehemu ya kwanza ina sura ya kwanza ambayo inatoa habari za utangulizi kuhusu mradi wa kutoa mafunzo kwa Polisi. Sehemu hii pia inatoa maelezo ya ufafanuzi wa maana ya haki za binadamu na pia orodha ya mikataba na maazimio ya haki za binadamu iliyonukuliwa katika mwongozo huu. Mwisho, inaelezea sababu na madhumini ya mafunzo ya Haki za Binadamu kwa watekelezaji wa sheria.

Sehemu ya pili ya mwongozo, inahusu mada ya mafunzo yaani kazi na utendaji wa watekelezaji wa sheria. Sehemu hii inaanzia sura ya pili hadi ya tisa. Kama ilivyotajwa hapo awali, mada za mafunzo zimechaguliwa kwa kuzingatia hali halisi inayogusa utendaji wa kazi wa Polisi Tanzania. Hivyo, mada hizo zinalenga kurekebisha mapungufu katika maeneo hayo.

Sehemu ya tatu inahusu ufuatiliaji na tathmini ya mafunzo. Inalenga kuwapatia wakufunzi uwezo wa kufuatilia na kutathmini mafunzo ili kupima matokeo ya mafunzo hayo.

Sehemu ya nne na ya mwisho katika mwongozo huu ina viambatanisho vya Mikataba ya Kimataifa ya Haki za binadamu ambayo ni ya msingi katika kutoa vipimo vya majukumu na utendaji wa maofisa wanaotekeleza sheria. Inategemewa kuwa viambatanisho hivi vinaweza kutumika kama rejea kwa wakufunzi.

# SURA YA KWANZA

## A: HAKI ZA BINADAMU NA POLISI

**Utangulizi:**

Haki za binadamu zinahusu binadamu wa aina zote duniani, bila kujali umri, jinsi, kabila, lugha, umbo, ukubwa n.k. Haki hizi ni za msingi sana kwa vile zinahusiana na suala la mtu kuwa binadamu au ubinadamu. Utu wa mtu ndio kipimo cha haki za binadamu. Polisi kama watekelezaji wa sheria katika eneo la utulivu wa umma na usalama wanafanya kazi kwa kiasi kikubwa na watu. Wanaweza kutumia bunduki, mbwa nk. lakini nia hasa ni kumlinda binadamu. Hii ikiwa ndio hali halisi, sehemu hii inajaribu kutoa tafsiri ya haki za binadamu ili baadaye iweze kuhusianishwa na mijadala kuhusu kazi za polisi.

### MATARAJIO

Mwishoni mwa sehemu hii washiriki wataweza:-

1. Kutoa tafsiri ya haki za binadamu
2. Kuainisha aina za haki za binadamu
3. Kutaja haki za binadamu wanazozifahamu na vyombo vya haki za binadamu Kimataifa.

### Haki za Binadamu ni nini?

Tumia maswali yafuatayo kubonga bongo na washiriki kuhusiana na maana ya haki za binadamu.

- Unaposikia haki za binadamu unaelewa nini?
- Kuna sababu yoyote ya kujifunza haki za binadamu?
- Kwa nini polisi wajifunze haki za binadamu?

Kutokana na majibu ya washiriki, elezea haki za binadamu na madhumini ya mafunzo ya haki za binadamu kwa polisi.

## SANDUKU HABARI 1:A

Haki za binadamu wakati mwingine hueleweka na kutafsiriwa tofauti tofauti kutegemea na hali tofauti, hali ambayo huweza kusababisha matokeo yasiyo mazuri kwa Haki zenyewe za binadamu. Kwa hiyo uelewa uliokubalika kwa pamoja wa haki za binadamu ni kwa mujibu wa Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu kama ilivyo katika utangulizi wake kuwa ni za muhimu katika kufanikisha ukuzaji wa heshima ya ujumla na ulinzi wa haki za binadamu na uhuru wa watu. Haki za Binadamu zinatafsiriwa kuwa ni **"misingi ya ujumla iliyokubalika ya usawa na haki"**. Ni haki za kiitikeli ulimwenguni zilizo sawa kwa watu wote, kwa kuwa tu wao ni binadamu. Hakika haki za binadamu mara nyingine zinasemekana kuwa ni zile haki za asili au haki zilizotolewa na Mungu kwa kuwa hazipaswi kununuliwa kufanyiwa kazi, au kurithiwa. Zipo kwa ajili ya kila mwanadamu bila kujali jinsia, asili, rangi, lugha, utaifa, umri, tabaka au dini au msimamo wa kisiasa.

- Haki za binadamu ni haki zisizoondosheka, huwezi kupoteza haki hizo bila kupoteza ubinadamu wako.
- Haki za binadamu ni haki zisizogawanyika au kuchagulika. Huwezi kunyimwa haki kwa sababu haina umuhimu au ina umuhimu mdogo.
- Haki za binadamu ni haki zinazotegemeana; Haki zote za binadamu ni sehemu ya muundo unaowiana. Hii ina maana kuwa uwezo wa mtu kushiriki katika serikali yake inaathiriwa moja kwa moja na haki yake ya kujieleza na kupata elimu na zaidi sana haki ya kupata mahitaji muhimu.

**Aina za haki za Binadamu**

Haki hizi zimepangwa kwa jinsi zilivyokua katika kutambulika kimataifa hivyo kupatikana aina hizi tatu:-

- Haki za kiraia na kisiasa
- Haki za kijamii, kiuchumi na kiutamaduni
- Haki za mazingira na maendeleo

### Haki za kiraia na kisiasa:

Haki hizi zinafahamika sana kwa jina la Haki za kizazi cha kwanza na wakati mwingine zimeitwa Haki zinazohusu Uhuru kwa vile zinatoa haki ya uhuru, kujitawala na usawa. Haki hizi zinajumuisha uhuru wa kufikiri na kupata habari, haki ya kuishi na haki mbele ya sheria. Haki za kiraia zinajumuisha Haki ya uhuru, usawa, kuabudu au kutokuabudu kama apendavyo mtu. Haki za kisiasa zinahusu Haki ya kupiga kura, kusema unachoamini, kupata habari, kuhudhuria mikutano na mikusanyiko kwa uhuru, na kujiunga na vyama vya siasa na mashirika mengine.

**Haki za kijamii, kiuchumi na kiutamaduni:**

Haki hizi nazo hujulikana kama haki za kizazi cha pili. Haki hizi zinahusu maisha ya watu, kazi zao na mahitaji yao katika maisha. Haki ya kupata mahitaji ya lazima kama chakula, malazi na mavazi. Haki ya utamaduni, elimu afya na kazi. Pia nafasi ya kuweza kushiriki katika maisha ya jamii kwenye masuala ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

**Haki za Mazingira na maendeleo:**

Haki hizi zinajulikana kama haki za kizazi cha tatu. Haki hizi zinatambua kuwa watu wana haki ya kuishi katika mazingira safi yasiyochafuliwa na kulindwa kutokana na uharibifu.

**ANGALIZO:**

***Haki nyingine zinapatikana katika kizazi zaidi ya kimoja. Kwa mfano haki ya kuoana na kuwa na familia. Hii ni haki ya kijamii na vile vile ni haki ya kiraia. Pia itiliwe maanani kuwa huku kugawa haki katika vizazi kumezua mjadala kwa vile watu wengine wanaelezea kuwa haki zote za binadamu ni muhimu, hakuna iliyopungua nguvu kuliko nyingine na inabidi zipatikane kwa pamoja kwa vile zinategemeana. Kwa kuzigawa haki inaweza kuonekana kuwa inamaanisha haki za kizazi cha kwanza zinazoweza kulindwa na haki za vizazi vingine zisitiliwe maanani. Unaweza kuingia kwenye mjadala huu na kutoa mapendekezo.***

## MASWALI YA KUJADILI:

(ii) Andika Haki tano ambazo ni za muhimu sana.

(iii) Ni haki zipi zinazopaswa kulindwa?

(iv) Ni Haki zipi zinalindwa zaidi nchini Tanzania?

(v) Je mtu anaweza kuzitofautisha haki katika vizazi hivyo vitatu na kufaidi aina moja na sio nyingine?

(vi) Unadhani ni haki zipi ambazo serikali ya Tanzania haiwezi kuhakikisha kuzitoa na kwa nini?



Mkufunzi ahitimishe mjadala kwa kuelezea haja ya Haki za binadamu kulindwa na watu wote kwa ajili ya wote.

**Hati rasmi za Kimataifa**

Mkufunzi ataje aina mbali mbali za vyanzo vya vipimo vya kimataifa vya Haki za binadamu.

- Mkataba wa Umoja wa Mataifa.

- Haki za kikatiba za kimataifa ambazo ni :-
  a) Tamko la Kimataifa la Haki za binadamu
  b) Mkataba wa Kimataifa wa Haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni
  c) Mkataba wa Kimataifa wa Haki za kisiasa na kiraia.
- Mkataba wa Kiafrika wa Haki za binadamu na za watu.
- Mkataba wa Haki za mtoto.
- Mkataba wa kuzuia aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake.

**Zoezi:**

Washiriki waelekezwe kujisomea aina mbalimbali za mikataba kwa wakati wao, na waainishe tofauti na yale yanayoshabihiana. Zoezi hili linaweza kufuatiwa na majadiliano siku nyingine.

## REJEO

- Haki za Binadamu ni zile haki alizo nazo mtu kwa sabatu tu yeye ni binadamu.
- Haki za binadamu ni za asili kwa kila binadamu, Dola/serikali haiwapi watu haki hizi bali inapaswa kuzilinda ili kila mtu aweze kuzifaidi.
- Kutambuliwa kwa haki za Binadamu kimataifa kumekuwa kuna kukua kulikofanya haki ziwekwe katika vizazi cha kwanza haki cha tatu.
- Haki za binadamu ni sehemu ya binadamu kwa hiyo haziwezi kuondolewa na pia zinategemeana hivyo kwamba moja haiwezi kuwepo bila ya nyingine.

# B: UPOLISI NA DEMOKRASIA

## Utangulizi

Demokrasia sio neno la kisheria na halina tafsiri moja kamili. Kwa lugha rahisi, Demokrasia inamaanisha utawala wa watu. Katika kujaribu kuipata, demokrasia imetafutwa kwa njia tofauti. Sura ya demokrasi iliyoundwa Tanzania inaonekana katika ibara za katiba ya Jamhuri ya Muungano. Sura hii inahusianisha demokrasia na mambo mengine muhimu katika utekelezaji wa sheria, kama utawala wa sheria na ukuzaji na ulinzi wa haki za binadamu. Sura hii inalenga kujadili mchecheto wa kidemokrasia unaofaa na utawala wa sheria ambazo ni nguzo zinazolinda vyema haki za binadamu na ambazo ni muhimu katika utekelezaji wa sheria. Pale ambapo utawala wa sheria upo, polisi wanawajibishwa na sheria. Sura hii pia inazingatia haki ambazo ni muhimu katika demokrasia na wajibu wa polisi kuhusiana na haki hizo wakati wa uchaguzi wa kidemokrasia.

### MATARAJIO

Mwishoni mwa sura hii washiriki wanapaswa kupata uelewa kwamba:

1. Demokrasia ni sehemu ya haki za binadamu hivyo utekelezaji wa sheria unapaswa ujizatiti katika kuilinda.
2. Polisi kama chombo cha uwakala kwa umma inapaswa kufanya kazi kwa mujibu wa sheria za nchi na kufuatana na vipimo vya haki za binadamu.
3. Pamoja na mambo mengine maofisa wa polisi wanategemewa kulinda haki za kidemokrasia za raia wakati wa uchaguzi
4. Polisi kama chombo cha uwakala kwa umma wanapaswa kutokuwa na upendeleo wakati wanasimamia mipango ya uchaguzi.

**ZOEZI LA KWANZA:**

### Polisi na Demokrasia

Mkufunzi awagawe washiriki katika makundi madogo. Katika makundi, washiriki wajadiliane wanavyoelewa neno 'demokrasia' Kundi si lazima lipate maana ya demokrasia kwa kutafsiri neno hilo ila wanaweza kulielezea neno demokrasia au kuorodhesha misingi muhimu ya demokrasia.
Washiriki warudi katika kundi moja na vikundi vidogo vipokezane kutoa taarifa zao. Yale matokeo yaliyoandikwa yaoneshwe bayana wakati kila kundi linatoa ripoti yake. Mkufunzi aruhusu majadiliano zaidi na ufafanuzi. Mkufunzi anapaswa kuwaongoza washiriki pale ambapo mambo muhimu yameachwa au yameeleweka vibaya.

Mkufunzi awasomee na kujadili tafsiri iliyopo hapa chini wakiwa katika kundi moja na wajibu maswali yatakayofuata.

## KUTAFSIRI DEMOKRASIA

Neno demokrasia linaweza kufikiriwa katika sura ya serikali ya watu kwa njia ya utawala wa wengi. Hii inaweza kuwa katika njia ya serikali ambayo nguvu za juu za kiutawala zipo mikononi mwa watu na zinatumiwa na watu moja kwa moja, (wakati mwingine hujulikana kama demokrasia ya moja kwa moja) au kwa njia ya serikali ambayo nguvu za juu za kiutawala zipo mikononi mwa watu na kutumiwa na watu kwa njia ya uwakilishi na kugawa madaraka, ambapo watu huchagua viongozi na wawakilishi katika uchaguzi huru unaofanywa kwa vipindi maalumu. Mfumo huu hujulikana kama demokrasia ya uwakilishi. Misingi ya demokrasia inayoonekana katika tafsiri hiyo hapo juu inaonekana pia katika sheria za kimataifa na sheria za nchi.

### SANDUKU HABARI I 1:1

**HATI RASMI ZA KIMATAIFA**

1. **Tamko la kimataifa la Haki za Binadamu, Ibara 21: inatamka haki ya kila mtu:**
   - Kushiriki katika serikali ya nchi yake moja kwa moja au kupitia wawakilishi waliochaguliwa kwa uhuru
   - Kupata kwa usawa huduma za umma katika nchi yake

*Ibara ya 21 inaelezea zaidi kwamba:*
- *Matakwa ya watu ndio yatakuwa msingi wa mamlaka ya serikali.*
- *Matakwa haya yatajieleza katika chaguzi za vipindi na za haki.*
- *Chaguzi zitakuwa kwa wote na kwa haki na zitafanyika kwa njia ya siri au kwa njia huru za kura zinazofanana na hiyo.*

2. **Mkataba wa kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa.**

*Ibara ya 24 inataja haki hizo hizo*

*(vii) Kushiriki katika masuala ya umma moja kwa moja au kwa uwakilishi*
*(viii) Kuwa na uwezo wa kupata huduma za umma*
*(ix) Kupiga kura katika chaguzi za vipindi na za haki.*

3. **Mkataba wa Kiafrika kuhusu Haki za watu na Haki za Binadamu Ibara ya 13 inafafanua haki za:**
   - *Kupata huduma za umma za nchi yake*
   - *Kutumia mali ya umma*

***Dokeza kwa Mkufunzi:***

*Mikataba ifuatayo ya Haki za binadamu kikanda pia ina ibara zinazofanana na hizo hapo juu:*

*(i) Mkataba wa Haki za Binadamu wa Kimarekani ibara ya 23*

*(ii) Mkataba Nyongeza nambari I katika mkataba wa Haki za Binadamu wa Ulaya - Ibara ya 3.*

**SHERIA ZA NCHI**

1. Katiba ya Jamhuri ya Muungano Tanzania - Ibara ya 21 (1) inahusu masharti ya kuchagua na kuchaguliwa, kuteua na kuteuliwa katika masuala yanayohusiana na utawala wa nchi.

*Kila raia wa Jamhuri ya Muungano anayo haki ya kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi, ama moja kwa moja au kwa kupitia wawakilishi waliochaguliwa na wananchi kwa hiari yao kwa kuzingatia ratiba iliyowekwa na sheria au kwa mujibu wa sheria.*

**(I) <u>ZOEZI KWA WANAFUNZI:</u>**

Rejea maelezo yaliyomo katika sanduku habari hapo juu, pitia vifungu vya habari hapo chini kisha jadili iwapo unakubali au kukataa yaliyomo katika vifungu hivyo:

1. Maafisa wa polisi waruhusiwe kushiriki katika serikali ya nchi moja kwa moja.
2. Maafisa wa polisi waruhusiwe kushiriki katika serikali ya nchi kwa kupitia uwakilishi tu.
3. Maafisa wa polisi waruhusiwe kujiunga na vyama vya siasa.
4. Maafisa wa polisi waruhusiwe kuwa na vyama vya wafanyakazi.
5. Maafisa wa polisi waruhusiwe kuandika barua za makala maalum katika magazeti.
6. Kutokuwa na upande wowote kwa upande wa maafisa wa polisi kunapingana na haki za binadamu za kimataifa za kushiriki katika mfumo wa uchaguzi kama wagombea.

**<u>ZOEZI LA PILI</u>**

**Polisi na utawala wa sheria**

Katika kundi kubwa mkufunzi awaongoze washiriki katika kujadili maana ya utawala wa sheria. Mkufunzi anaweza kuwasomea washiriki maelezo yafuatayo kuhusu utawala wa sheria.

## SANDUKU HABARI 1:2

**Utawala wa sheria**

Miongozo ya mambo ya jamii yaliyowekwa na makundi ya taratibu zilizo bayana na zisizobadilika ambazo hutumika bila ubaguzi kwa hali yoyote itakayojitokeza

**Misingi**

1. Kuwepo kwa kuzingatiwa kwa sheria kama chombo cha juu kinyume na matumizi mabaya ya nguvu na maamuzi huria.
   - Nguvu za dola zisitumike kwa kuzingatia maamuzi binafsi
   - Mtu yeyote asishtakiwe ila kwa mujibu wa sheria ya nchi
   - Sheria yoyote isitumike kinyumenyume (sheria ianze kutumika pale ilipoanza kuwepo)

2. Pia wote bila kujali hali yao ya maisha na sifa nyingine zozote wanapaswa kuwa sawa mbele ya sheria.

   - Serikali haipaswi kufaidi upendeleo usio wa lazima au kusamehewa katika sheria za kawaida.

**ii) <u>ZOEZI KWA WANAFUNZI:</u>**

Kwa kuzingatia maelezo yaliyotolewa hapo juu kuhusu utawala wa sheria, mkiwa katika makundi madogo, soma kisa mkasa kifuatacho na jibu maswali yatakayofuata

### POLISI KAZINI NA UTAWALA WA SHERIA

1. Umesimamishwa na Polisi katika kizuizi cha barabarani. Wanakagua gari lako kutafuta mali isiyo halali na hawapati kitu. Wanakuamrisha uegeshe gari lako pembeni mwa barabara na usubiri. Baada ya masaa matano wanakuambia uondoke lakini hawakuambii sababu za kukufanya usubiri kwa muda wote huo.

2. Sheria ya nchi inatamka ‘Afisa wa polisi au mtu yeyote hapaswi kutumia nguvu zaidi au kushusha hadhi ya mtu kuliko ilivyo lazima katika kumkamata’ Wajumbe watano wa kikundi kinachopinga serikali wanasimamishwa na Polisi wakiwa ndani ya gari. Polisi wanawatambua na mmoja wa hao wanaoshukiwa anatoa bunduki na mara polisi anamwaga risasi na kuwaua watuhumiwa wote watano.

**MASWALI:**

Katika kila kisa

i). Sheria gani inahusika?

ii). Nani amevunja sheria?

iii). Ni tendo / matendo gani yanadhihirisha ukiukwaji wa utawala wa sheria?

iv). Onesha ukiukwaji wa haki za binadamu uliojitokeza

## ZOEZI LA TATU

### Polisi na haki muhimu katika demokrasia

Mkufunzi atoe mhadhara mfupi kuhusu haki muhimu katika demokrasia. Anaweza kujadili na washiriki iwapo haki hizi ni timilifu, yaani zisizoweza kukiukwa au zinaweza kusitishwa kwa sababu mbali mbali. Maswali yanaweza kuulizwa ili kuibua mjadala. Vyombo vya kimataifa vya haki za binadamu na sheria za nchi zilizopo katika masanduku habari zirejewe.

**SANDUKU HABARI 1:3**

**HAKI MUHIMU KATIKA DEMOKRASIA**

**HATI RASMI ZA KIMATAIFA**

1. **Haki ya uhuru wa kufikiri dhamiri na dini;**

   Haki hii inalindwa chini ya:

   (i) **Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu.**

   *Ibara ya 18 inaeleza:*

   *Kila mtu ana haki ya uhuru wa kufikiri, dhamiri na dini, hii haki inajumuisha uhuru wa kubadili dini au imani na uhuru wa kuielezea dini yake au imani kwa kufundisha, kutenda au kuabudu.*

   (ii) **Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa: Ibara 18:**

   *"Kila mtu atakuwa na haki ya uhuru wa kufikiri, dhamiri na dini. Haki hii itajumuisha uhuru wa kuwa au kuingia katika dini au imani anayoichagua mtu na uhuru wa kuielezea dini yake au imani kwa kuabudu, kuifuata, kutenda na kuifundisha iwapo ni kibinafsi au mbele ya umma na watu wengine katika jamii.*

   (iii) **Mkataba wa Kiafrika Kuhusu Haki za Watu na Haki za Binadamu Ibara ya 8**

   *Uhuru wa dhamiri, taaluma na uhuru wa kuamini dini yoyote lazima vihakikishwe. Hakuna sheria au taratribu zitakazotumika kumnyima mtu yeyote uhuru huu.*

(iv) **Ifuatayo ni mikataba ya kikanda ya haki za binadamu yenye ibara zinazolingana na hiyo hapo juu**
- Mkataba wa Haki za Binadamu wa Kimarekani - Ibara ya 12
- Mkataba wa Haki za Binadamu wa Ulaya

2. **Haki ya uhuru wa kutoa maoni na kujieleza**

Haki hii inalindwa chini ya:-

(i) **Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu - Ibara ya 19**

Kila mtu ana uhuru wa kutoa maoni yake na kujieleza. Haki hii inajumuisha uhuru wa kusimamia maoni yake bila kuingiliwa na kutafuta, kupokea na kutoa habari na mawazo kupitia vyombo vya habari vya aina yoyote bila kujali mipaka.

(ii) **Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa - Ibara ya 19**

(a) Kila mtu atakua na haki ya kutoa maoni yake bila kuingiliwa.

(b) Kila mtu atakuwa na haki ya kujieleza.

(iii) **Mkataba wa Kiafrika Kuhusu Haki za Watu na Haki za Binadamu – Ibara ya 9**

(a) Kila mtu atakuwa na haki ya kupata habari

(b) Kila mtu atakuwa na haki ya kujieleza na kusambaza mawazo yake kulingana na sheria

**Ifuatayo ni mikataba ya Haki za Binadamu kikanda yenye Ibara zinazolingana na hizo hapo juu:**
- Mkataba wa Haki za Binadamu wa Kimarekani - Ibara ya 13
- Mkataba wa Haki za Binadamu wa Ulaya - Ibara ya 10

3. **Haki ya uhuru wa kukutana na watu wengine na kujumuika kwa amani.**

Haki hizi zinalindwa chini ya:

(i) **Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu ñ Ibara ya 20**

*(a) Kila mtu ana haki ya kukutana na watu wengine na kujumuika kwa amani.*

*(b) Hakuna mtu atakayelazimishwa kujiunga na umoja wowote.*

(ii) **Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa - Ibara ya 21– 22**

*Ibara ya 21 inaelezea kwamba Haki ya kujumuika kwa amani itatambuliwa. Pasiwepo vipingamizi katika kutekeleza haki hii ila kwa mujibu wa sheria na ambavyo ni muhimu katika jamii ya kidemokrasia na kwa kuzingatia usalama na ulinzi wa taifa, usalama wa raia na utulivu wa umma.*

(iii) **Mkataba wa Kiafrika Kuhusu haki za Watu na Haki za Binadamu – Ibara ya 10.**
*Kila mtu ana haki ya kujumuika na watu wengine kwa hiari ili mradi asivunje haki na uhuru wa wengine*

**Ibara ya 11.**
Na watu wote wana haki ya kujumuika kwa uhuru ili mradi asivunje sheria na uhuru wa watu wengine.

(iv) **Ifuatayo ni mikataba ya Haki za Binadamu kikanda yenye ibara zinazowiana na hizo hapo juu,**

- **Mkataba wa Haki za Binadamu wa Kimarekani – Ibara ya 15 na 16**
- **Mkataba wa haki za Binadamu wa Ulaya – Ibara ya 11.**

## SHERIA YA NCHI

**KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** ina Haki za Kikatiba zinazoainisha haki zilizo muhimu katika demokrasia.

1. **Uhuru wa kujieleza – Ibara ya 18 (1)**
*Kila mtu ana haki ya uhuru wa kutoa maoni na kujieleza, na kutafuta, kupokea na kusambaza habari na mawazo kupitia vyombo vya habari bila kujali mipaka ya nchi na pia ana haki ya uhuru wa kutoingiliwa katika mawasiliano.*

2. **Uhuru wa dini na mawazo – Ibara ya 19 (1)**
*Kila mtu ana haki ya kuwa na uhuru wa mawazo au dhamira, imani na uchaguzi katika mambo ya dini, pamoja na uhuru wa mtu kubadilisha dini au imani yake.*

3. **Uhuru wa kujumuika – Ibara ya (1)**
*Kila mtu, bila kuathiri sheria za nchi, ana haki ya kuwa huru, kukutana na watu wengine kwa hiari yake na kwa amani, kujumuika na kushirikiana na watu wengine, kutoa mawazo hadharani na hasa zaidi kuanzisha au kujiunga na kuendeleza imani au maslahi yake au maslahi mengineyo.*

## KISA MKASA

1. Kikundi cha kidini chenye msimamo mkali kinataka kufanya maandamano dhidi ya kundi la watu waliodhalilisha kitabu chao kitakatifu. Na pia wanataka vibanda vyote vinavyouza chakula kilichokatazwa na kitabu kitakatifu vivunjwe. Wanakataliwa ruhusa ya maandamano na polisi anayehusika.

2. Mpinzani wa kisiasa Bwana Manoti anachoma bendera ya chama kingine cha siasa katika mkutano wa hadhara na polisi wanamkamata
3. Kiongozi mmoja wa chama cha siasa katika mkutano wa hadhara anadai kuwa watu wa asili mojawapo anaowaita "Gabacholi" ni kundi dogo na wafuasi wa kiongozi huyo ni "walala hoi" ambao ni wengi na wenye hadhi zaidi kwa hiyo anataka wafuasi wake wawe na haki ya kumiliki maduka na biashara nyingine nchini. Polisi wanamkamata.
4. Gazeti moja lilitoa habari katika makala ya mhariri likidai kuwa serikali inahusika na rushwa na kwa hali hiyo watu wasilipe kodi. Polisi walikusanya magazeti yote kabla hayajatawanywa na kumkamata mhariri wa gazeti hilo.
5. Kundi la wanasiasa wanapanga / na kujadili katiba mpya katika mkutano wa vyama mbalimbali vya siasa. Mkutano huo unaingiliwa na kundi dogo la wanachama wa chama cha siasa kinachopinga majadiliano hayo. Maandamano yanasitishwa kulinda mlolongo wa majadiliano hayo. Mjini zaidi ya watu 50,000 wanatarajiwa kushiriki katika maandamano kuelekea ukumbi wa jiji. Kundi dogo la wanasiasa wanatishia kufanya fujo iwapo maandamano yatafanyika. Polisi wanakataa kutoa kibali cha kufanya maandamano.

## KAZI ZA VIKUNDI

Washiriki wakae katika makundi madogo yanayofaa. Wapewe maelekezo ya kupitia kila kisa mkasa katika hivyo vitano hapo juu kila kikundi kijaribu kuelezea kiasi cha ukiukwaji wa haki za kidemokrasia katika kila kisa.

## ZOEZI LA NNE

### Wajibu wa Polisi Wakati wa Uchaguzi

Katika kundi lote mkufunzi aongoze washiriki katika kujadili habari zilizopo katika sanduku. Kisha katika makundi madogo washiriki wajaribu kutayarisha miongozo kwa maafisa wa polisi, ya jinsi polisi wanavyoweza kutimiza wajibu wao vizuri wakati wa vipindi vya uchaguzi bila upendeleo na kutoonesha kufungamana na chama fulani cha siasa, katika kulinda utulivu, usalama na amani.

Baadaye, washiriki wote wakusanyike pamoja na kila kundi litoe taarifa yake kuhusiana na mjadala wao na miongozo waliyoandaa. Mkufunzi aruhusu muda wa majadiliano ya jumla.

## SANDUKU HABARI 1:4

Habari za ujumla kuhusu wajibu wa polisi wakati wa uchaguzi

1. **Taratibu za Mienendo kwa Maafisa Watekelezaji wa Sheria.**
   - *Ibara ya 1 inaweka wajibu wa kutumikia jamii kwa maafisa wote watekelezaji wa sheria.*
   - *Ibara ya 2 inawataka maafisa watekelezaji wa sheria kuheshimu utu na kulinda na kusimamia haki za binadamu*

   *Ibara ya 7 inawataka maafisa watekelezaji wa sheria kupinga na kuzuia vitendo vyovyote vya rushwa kwa nguvu zote na wasifanye vitendo vyovyote vya rushwa.*

2. **Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu**
   *Maafisa wa Polisi wanatakiwa kulinda utulivu wa jamii (amani ya jamii) ili mfumo wa siasa uweze kutekelezwa kwa mujibu wa katiba na sheria.*

Ibara ya 28 inaeleza kwamba
*"Kila mtu anastahili utulivu wa kijamii na wa kitaasisi ambapo haki na uhuru wake uliotolewa katika tamko hili hupatikana".*

3. **Mwogozo wa Mafunzo ya Haki za Binadamu kwa Polisi:** *Mfululizo wa mafunzo ya kitaaluma, Nambari 5 Umoja wa Mataifa N.Y. Geneva 1997 (Ukurasa wa 43, 44 - 45) unashauri kwamba wakati wa uchaguzi:*
   - *Afisa wa Polisi anahitaji kuweka mizani kati ya utulivu wa umma na makundi ya haki*
   - *Afisa wa Polisi anahitaji kuhamasishwa katika haja ya kuangalia kutofungamana na upande wowote na kutokuwa mbaguzi*
   - *Afisa wa Polisi anahitaji kubakia bila fungamano la kichama na asiwe na upendeleo*
   - *Polisi wanahitaji kukumbuka kuwa hawautumikii utawala maalum, mfano Polisi ni taasisi ya taifa na sio mali ya watawala.*
   - *Afisa yeyote wa Polisi atakayekuwepo katika sehemu za kujindikisha au kupiga kura inabidi awe mwangalifu mwenye kufanya kazi kitaaluma na kwa taratibu zinazokubalika.*

### SHERIA YA NCHI

1. *Mswada wa sheria wa kurekebisha sheria ya uchaguzi ya mwaka 1999, ulipitishwa tarehe 24 Machi 1995, sehemu ya 11 ya sheria ya mwaka 1995 imerekebisha ibara ya 63 ya sheria ya awali kwa kuondoa kifungi kidogo cha 2 na badala yake kuweka kifungu kifuatacho:-*

*(a) Hakuna mtu yeyote ila hawa wafuatao atakayeruhusiwa kuingia katika kituo cha kupigia kura.*
*(b) Afisa wa Polisi au mtu anayehusika na usalama katika kituo hicho.*

- *Sehemu ya 72 ya sheria ya awali inafutwa na badala yake inakuwa kama ifuatavyo:-*
  *(b) Hakuna mtu ila hawa wafuatao watakaokuwepo katika kuhesabu kura; Afisa wa Polisi au mtu mwingine anayehusika na usalama mahali kura zinapohesabiwa.*

## KAZI YA HIARI

1. Katika makundi madogo tayarisha kisa mkasa utakachokiundia mchezo mfupi wa kuigiza. Kazi ya kila kundi ni kuandaa mchezo wa kuigiza unaoonesha Polisi wakiwa wanaunga mkono chama fulani cha siasa na kuwa wabaguzi.
2. Washiriki wakusanyike pamoja na kila kundi kwa kupokezana waoneshe mchezo wao. Baada ya kuonesha mkufunzi awasaidie washiriki kufanya uchambuzi wa makosa ya maafisa wa polisi wakirejea vifungu maalum vya haki za binadamu katika katiba na hati rasmi za kimataifa.

**Mifano:**

1. Mwanasiasa anatoa matamko ya kuudhi. Mengi ya matamko haya yanaishutumu serikali iliyoko madarakani kuhusika na rushwa na ubadhirifu wa fedha za walipa kodi. Anakamatwa na polisi na kufunguliwa mashtaka kwa kuwachochea watu kutopiga kura. Mwanasiasa mwingine maarufu ambaye anapendwa na kukubalika na serikali anatoa tamko baya zaidi na lenye uchochezi akiwaita viongozi wa dola majambazi na wezi. Huyu yeye haguswi.
2. Watu wawili wanaounga mkono vyama vya upinzani wanapigwa na afisa mmoja wa polisi na kuumizwa vibaya. Wanashutumiwa kwa kushangilia ushidi wa chama cha upinzani katika uchaguzi wa serikali za mitaa. Siku hiyo hiyo wanajaribu kupiga ripoti polisi kuhusiana na tukio hilo lakini hawapatiwi msaada wowote. Afisa anayehusika hana ushirikiano kabisa. Anawaambia wanapoteza muda wake na hawezi kuwahudumia kwa vile ana mafua. Wanajaribu kupeleka tatizo lao kituo cha kati cha polisi lakini wanarudishwa kwenye kituo kile kile na wanaporudi tena hakuna anayewasikiliza.

## REJEO

Maafisa wa Polisi wana wajibu wa kulinda na kukuza haki za kidemokrasia za watu. Hivyo kazi zao zielekezwe katika kusimamia na kuheshimu misingi ifuatayo:

1. Kila mtu ana haki ya uhuru wa kujieleza na kutoa maoni
2. Kila mtu ana haki kwa hiari yake kujumuika, kujiunga kwenye ushirika, kushirikiana na watu wengine.
3. Kila mtu ana haki ya kushiriki katika masuala yanayohusu utawala wa nchi yake ikijumuisha kuchagua kiongozi na kuchaguliwa katika uongozi.
4. Wakati wa uchaguzi polisi lazima wahakikishe amani na utulivu wakati huo huo wakibakia katika hali ya kutopendelea au uonevu.

## REJEA

Kwa ufafanuzi zaidi unaweza kurejea


1. United Nations High Commission For Human Rights: **Human Rights and Law enforcement: A manual on human Rights training for Police** (Proffesional training services No. 5 Geneva, Switzerland 1997)
2. Wizara ya Sheria na mambo ya Katiba, **Haki za Binadamu na utekelezaji wa Sheria - Mpango wa kufundishia** (Ministry of Justice and Constitutional Affairs: **Human Rights and law enforcement: Lesson Plan 1999**.

# SEHEMU YA PILI
# SURA YA PILI

## KUKAMATA

### Utangulizi

Kukamata ni muhimu katika mfululizo wa utekelezaji wa sheria na usimamizi wa haki. Watekelezaji wa sheria Tanzania na hata katika nchi nyingine wamepewa mamlaka ya kukamata katika kuhakikisha haki, amani na utulivu. Kukamata kama sehemu ya utekelezaji wa sheria kumelengwa kutimiza madhumuni yafuatayo:

1. Kuwezesha mfululizo wa uchunguzi katika tuhuma za tendo la uvunjaji wa sheria.
2. Kumzuia mtuhumiwa kufanya au kuendelea kufanya kosa.
3. Kuwezesha mkondo wa sheria na haki kuchuka nafasi yake kuhusiana na anayetuhumiwa kwa kumfikisha mbele ya mahakama na kufungua shitaka dhidi yake.

Kwa lugha nyepesi, tendo la kukamata mtu linamaanisha kumnyima mtu huyo uhuru wake. Hata hivyo hakuna tafsiri pekee na ya moja kwa moja ya neno kukamata katika sheria za nchi yetu zinazosimamia wajibu na kazi za polisi ingawaje tunaweza kuangalia sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (Namba 9 ya 1985). Sheria hii katika kuelezea namna ya kukamata inatoa maelezo kwamba, afisa polisi atamgusa au kuzuia mtu anaye kamatwa labda tu mtu huyo ajisalimishe kwa neno au tendo. Hata hivyo Misingi ya Kulinda Haki za Watu Wote Walio Katika Aina Yoyote ya Kizuizi au Kifungo inatafsiri neno kukamata kama ifuatavyo:
*"Kitendo cha kumtia mtu nguvuni kwa tuhuma ya kufanya kosa au kwa amri ya mamlaka fulani"*

Nia ya kukamata ni kumnyima mtu anayehusika uhuru. Ikumbukwe kuwa uhuru wa mtu binafsi ndio nguzo mojawapo ya msingi wa haki za binadamu ambayo kukamata kunaizuia. Kwa hivyo basi kuizuia haki hii kunahitaji sababu za kihalali ambazo zinaweza tu kuthibitishwa na ukweli wa kisheria na ulazima wake.

### MATARAJIO

Mwishoni mwa sura hii inatarajiwa kuwa washiriki wataweza kuelewa yafuatayo:
1. Maana ya kukamata kwa mtazamo wa anayetuhumiwa.
2. Kukamata kutekelezwe vipi.
3. Nani ana mamlaka ya kukamata na katika mazingira gani.
4. Haki za mtu anayekamatwa

## ZOEZI LA KWANZA

### Nani ana uwezo wa kukamata?

Kabla swali hili halijajibiwa mkufunzi awatake washiriki kujiunga katika makundi madogo na kusoma au kuwasomea kisa kama kilivyoandikwa katika gazeti. Mkufunzi awatake washiriki kujadili na kutoa mrejesho kwa kujibu maswali yanayofuata kisa hicho

Ukurasa wa pili Dar es Salaam Post, Jumatatu Februari 21, 1999

**PROFESA KYOMA ADHALILISHWA NA KUNDI LA KOMANDOO**

Na mwandishi wetu, BOMBO

Kampeni zinazoendelea za uchaguzi wa rais na wabunge zimeandamana na mambo kadhaa yasiyo ya kawaida katika manispaa ya Bombo. Jambo mojawapo la aina hiyo na lisilopendeza lilitokea jana katika uwanja wa mpira wa Shule ya Msingi Kishura wakati wanachama watano wa tawi la vijana wa chama cha N.P.P maarufu kwa jina la kundi la komandoo walipomzunguka Katibu Mkuu wa Chama cha Mabaliko, Profesa Katoto Kyoma mara baada ya Profesa huyo kuzikandia sera za chama tawala cha N.P.P. Alielezea sera hizo kuwa hazifai. Kabla ya tukio hilo vijana hao waliokuwa wamevalia sare zao walimwonesha Profesa huyo vitambulisho vyao wakisema wanamkamata kwa kosa la kuchochea umma dhidi ya serikali iliyoko madarakani na hivyo kutishia usalama wa taifa.

Profesa Kyoma aliwapuuza akisema kwamba, kuwa kwao kikundi cha wasalama cha chama tawala hakiwapi madaraka ya kukamata mtu yeyote kwa vile wao si maafisa wa Polisi. Hata hivyo aliwaambia wanaweza kutoa ripoti polisi dhidi yake ambao ndio wanaoweza kumkamata. Makomandoo hao watano hata hivyo wakasisitiza kwamba wana mamlaka ya kukamata watu na hakika wamekuwa wakitumia mamlaka hayo tangu siku nyingi.

## MASWALI YA MAJADILIANO

Maswali haya yanayohusu ripoti hiyo ya gazeti yanatakiwa yajibiwe katika makundi ya washiriki. Kila kundi lichague mwakilishi atakayeelezea majibu ya kundi lao mbele ya washiriki wote. Majibu yawe yameandikwa katika karatasi kubwa.

1. Kwa kuzingatia matukio katika kisa hicho unadhani hao makomandoo watano walikuwa na mamlaka / uwezo wa kumkamata Profesa Kyoma?

2. Je unadhani kukataa kwa Profesa Kyoma kukubaliana na hilo kundi la makomandoo ni sahihi / halali?
3. Je, unaweza kutaja makundi yenye hadhi kama hili la komandoo hapa Tanzania?
4. Ni nani anayeweza kukamata mtuhumiwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania?

Mkufunzi aelezee washiriki mamlaka ya kukamata kama yalivyo katika Sanduku Habari hapa chini.

## UWEZO WA KUKAMATA
## SANDUKU HABARI 2:1

1. Kifungu 11: (1) **Sheria ya Mwenendo wa makosa ya Jinai nambari 9 (1985)**
   Wakati wa kukamata mtuhumiwa afisa wa Polisi au mtu yeyote anayekamata atalazimika kumgusa au kumzuia mtu anayekamatwa labda tu pawepo kujisalimisha kwa neno au tendo.

2. Kifungu 16 (1) Sheria ya Mwenendo wa makosa ya Jinai
   Raia yeyote ambaye si askari polisi anaweza kumkamata mtu yeyote atakayefanya kosa mbele yake lililoorodheshwa katika kifungu cha 14 cha sheria hii.

3. Kifungu cha 17: Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai
   Hakimu yeyote anaweza kukamata au kutoa hati ya kukamata mtu yeyote atakayedhaniwa ametenda kosa katika eneo la mamlaka yake.


### ZOEZI LA PILI

### Kuzuia ukamataji holela

Mkufunzi awaelekeze washiriki kukaa katika makundi ya watu watano watano.Itabidi awakumbushe kwamba kumkamata mtu kunamaanisha kumnyima mtu huyo uhuru wake, ambao ni msingi muhimu wa haki za binadamu. Hata hivyo, kukamata hufanyika kama jambo la muhimu katika kuhakikisha sheria na haki zinachukua mkondo wake. Hufanyika kukiwepo na hisia za kimsingi za kuwepo kwa uhalifu.

Kwa sababu hizo basi watekelezaji wa sheria wanapaswa kuwa na sababu za msingi za kumhusisha mtu na tuhuma za uhalifu ili waweze kumkamata. Ni kwa sababu hizi ukamataji holela unakatazwa. Mkufunzi anaweza kuelezea maana ya ukamataji holela kama hivi:

Ukamataji holela ni tendo la mtu anayetekeleza mamlaka ya Polisi kuweka mtu mwingine kizuizini kinyume cha sheria.



## MASWALI YA MAJADILIANO:

1. Kwa nini pawepo na sheria ya kuzuia ukamataji holela ?
2. Je unafahamu tukio lolote la ukamataji holela lililotokea Tanzania?
3. Ni nini kinachoweza kuwa sababu ya kuamua kukamata kiholela ?
4. Ainisha athari za ukamataji holela katika utendaji wa Jeshi la Polisi Tanzania
5. Je, inawezekana kuepuka ukamataji holela Tanzania?

### SANDUKU HABARI 2.2

**1. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 15**

*1. Kila mtu anayo haki ya kuwa huru na kuishi kama mtu huru*

*2. Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu kuwa huru na kuishi kwa uhuru, itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kukamatw,a kufunglwa, kuwekwa kizuizini, kuhamishwa kwa nguvu au kunyang'anywa uhuru wake isipokuwa tu:*

*a) Katika hali na kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria.*

*b) Katika kutekeleza hukumu, amri au adhabu iliyotolewa na mahakama kutokana na shauri au mtu kutiwa hatiani kwa kosa la jinai.*

**2. Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu: Ibara ya 9**

*Hakuna mtu atakayefungwa au kuwekwa kizuizini au kuhamishwa kinyemela (Bila mpango) au (bila kufuata sheria)*

***i. Mkataba wa Kiafrika Kuhusu Haki za Watu na Haki za Binadamu:***
*Ibara ya 6 Kila mtu atakuwa na haki ya uhuru na usalama wa utu wake. Mtu yeyote hastahili kunyimwa haki hii isipokuwa pale ambapo kuna sababu na masharti yaliyobainishwa awali kisheria. Kimsingi mtu yeyote hawezi kufungwa, au kukamatwa bila kufuata sheria zilizowekwa.*

***ii. Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa***
*Kila mtu ana haki ya uhuru na usalama wa utu wake. Hakuna mtu atakayefungwa kiholela au kuwekwa kizuizini. Hakuna mtu anayepaswa kunyimwa uhuru wake ila kwa sababu na masharti yaliyobainishwa na sheria.*

Mkufunzi anaweza kuwaelekeza washiriki wakae katika makundi mawili kutegemea na ukubwa wa kundi (kama halizidi watu ishirini na tano) wakiwa katika makundi wapewe zoezi lifuatalo:

1. **KUNDI LA KWANZA**
Andaa igizo fupi linaloonesha wizi wa kutumia nguvu uliofanyika katika manispaa fulani. Mkuu wa Polisi wa mkoa anatoa amri kwa Polisi wengi kiasi kukamata kijana yeyote wa kiume atakayekutwa hana kazi hapo mjini. Msako huu wa polisi unawabughudhi vijana katika mji huo na wanaamua kuwapiga polisi popote wanapowaona na kuharibu mali za polisi kila inapowezekana.

2. **KUNDI LA PILI**
Kwa kufuata igizo la kundi la kwanza, tayarisha kipindi cha radio au runinga chenye lengo la kuelimisha mamlaka ya watekelezaji wa sheria jinsi ambavyo kukamata kiholela kunavyoweza kuathiri sifa ya polisi na jinsi pia kukamata huko kunavyokiuka haki za binadamu.

Mwishoni mwa mrejesho huo mkufunzi aongezee maelezo katika majadiliano akitoa msisitizo katika masuala muhimu yaliyojitokeza.

**ZOEZI LA TATU**

**Taratibu za kukamata**
Mkufunzi awatake washiriki kuingia katika makundi madogo. Maswali yafuatayo yatolewe kwa kila kundi kwa majadiliano na mrejesho:

1. Polisi anawezaje kumkamata mtu ?
2. Ni haki gani alizonazo mtu anapokamatwa ?
3. Ni wajibu gani alio nao mtu anayekamatwa?

Baada ya mrejesho, mkufunzi awasomee washiriki kisa mkasa kinachafuata:

## KISA MKASA

Halmashauri ya jiji la Bongo katika miaka ya karibuni imefanya kazi nzuri hasa katika kuboresha huduma za jamii na utunzaji wa mazingira. Shule kadhaa zimejengwa na nyingine zimekarabatiwa, barabara zimejengwa, hospitali na vituo vya afya zimeboreshwa. Wakazi wa Bongo hawana cha ziada katika furaha yao kwa Halmashauri ya jiji lao.

Katika jitihada zake za kufanya mji wa Bongo kuwa mji wa mfano katika Jamhuri ya Takania, Halmashauri ya jiji la Bongo iko katika mpango mzito wa mradi wa mipango

miji. Chini ya mradi huu, wafanyabiashara wadogo wadogo ambao wanafanya shughuli zao katika mitaa yote ya mji na katika baraza zote za majumba mjini hapo wanatakiwa kufukuzwa na wapatiwe sehemu maalum nje ya jiji. Halmashauri ya jiji imetunga sheria ndogo ndogo zinazofanya tendo la kufanya biashara kwenye sehemu isiyo maalum kuwa kosa la jinai. Zaidi ya hapo, sheria hiyo inasemekana imeshinikizwa na wafanyabiashara wenye asili ya kiasia ambao wanawaona wafanya biashara wadogo wadogo kama wapinzani, ambao wanavutia wateja kiasi kikubwa kwa vile wao huuza mali zao kwa bei rahisi zaidi na zaidi kufanya wafanya biashara waasia kukosa wateja.

Koja na Huseni waliathirika na mpango huo wa Halmashauri. Watu hawa wawili walipokuwa wanauza doti za kanga katika mtaa wa Kango walikamatwa na polisi bila kuelezwa kosa lao na hawakuoneshwa hati ya kukamatwa. Walipodai walikusanywa wakatupwa katika karandinga la polisi na wakaambiwa wanapelekwa kituo cha polisi ambapo wataelezewa tuhuma dhidi yao. Walipofika kituo cha polisi walitakiwa kutoa mali zao kwa polisi mkuu wa kituo na wakaongozwa kwenye mahabusu ambapo walikaa kwa siku tatu kabla ya kufunguliwa mashtaka kwa kosa la kufanya biashara katika sehemu zisizoainishwa kinyume na kifungu cha 11 cha sheria ndogo ndogo za mipango miji ya mwaka 1998.

Watuhumiwa hao wawili walipatikana na hatia kwa mujibu wa mashtaka dhidi yao na walihukumiwa kulipa faini ya shilingi elfu 10,000 kila mmoja au kwenda jela miezi sita.

Mkufunzi awatake washiriki kukaa katika makundi madogo na awaelekeze kuainisha masharti yaliyokiukwa na polisi wakati walipokuwa wanakamata watu katika kisa hicho hapo juu.

Baada ya zoezi hilo, mkufunzi awaongoze washiriki kujadili masharti na taratibu za kukamata kama yalivyo kwenye sanduku hapa chini.

## SANDUKU HABARI 2:3

**MASHARTI NA TARATIBU ZA KUKAMATA**

**SHERIA ZA NCHI:**

***Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai namba 9 / 1985***

*Kifungu cha 11 (1) cha sheria: katika kukamata mtuhumiwa wa uhalifu, polisi anayehusika au mtu yeyote anayekamata anapaswa kumgusa au kumzuia mtu*

anayekamatwa labda kuwepo kujisalimisha kwa neno au tendo.

1. *Kifungu cha 13* Kuacha makosa yalioainishwa katika kifungu cha 14 kila mtekelezaji wa sheria anapaswa kuwa na hati ya kukamata iliyotolewa na hakimu mtendaji wa kata au mtendaji wa serikali ya kijiji ili aweze kukamata mtuhumiwa.
2 *Kifungu cha 23 (1)* Mtu atakayemkamata mtu mwingine anapaswa wakati wa kumkamata amueleze huyo mtu anayemkamata kosa linalosababisha akamatwe.
3. *Kifungu 23 (2)* Mtu anayemkamata mtu mwingine atahesabika kutimiza masharti ya kifungu (1) kama atamtaarifu huyo anayemkamata vipengele vinavyohusu kosa analokamatiwa na si lazima mtu huyo afanye hivyo kwa kutumia lugha ya kitaalamu.
4. *Kifungu cha 12:21.* Nguvu kupita kiasi isitumike wakati wa kukamata au kumfungia mtuhumiwa. Pingu na njia nyingine za nguvu zitumike tu pale ambapo ni lazima.
5. *Kifungu cha 13 (1)* Polisi anayekamata mtuhumiwa bila hati ya kukamata bila kupoteza muda na kwa kulingana na vifungu vinavyohusiana na dhamana anapaswa amfikishe au ampeleke mtuhumiwa aliyemkamata mbele ya mahakama iliyo katika eneo la kituo cha polisi alikomkamatia.

## VIWANGO VYA KIMATAIFA

1. **Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa: Ibara ya 9**

   (2) *Yeyote atakayekamatwa lazima aelezwe wakati anakamatwa sababu zilizopelekea kukamatwa kwake na aelezwe mara moja tuhuma dhidi yake.*

   (3) *Inabidi yeyote atakayekamatwa au kuwekwa ndani kwa tuhuma za kosa la jinai afikishwe mbele ya jaji au afisa mwingine mwenye mamlaka ya kisheria kufikishiwa mashtaka hayo mara moja na ana haki ya kesi yake kusikilizwa katika muda mfupi iwezekanavyo au aachiwe. Haitakuwa kanuni ya kawaida kwa watu wanaosubiri kesi kuwekwa rumande, lakini kuachiwa kwao kunatakiwa kundamane na kidhibiti kwamba watafika kwenye kesi na katika hatua zifuatazo za kesi hiyo na kama kutatokea suala la kutekeleza hukumu.*

2. **Kundi la kanuni za kulinda Watu Wote Dhidi ya Aina Yoyote ya Kizuizi au Kifungo.**

   *Kanuni ya (2) Kukamata kufanyike kwa mujibu wa sheria na maafisa wenye uwezo au waliopewa mamlaka hayo.*

*Kanuni ya 10: Wakati wa kukamatwa lazima watu waelezwe sababu za kukamatwa. Wanapaswa kuelezwa mara moja juu ya tuhuma dhidi yao.*

*Kanuni ya 12: Kumbukumbu lazima iwekwe ya sababu za kukamata, muda wa kukamata, wakati wa kuwasili katika kituo chenye rumande na mara ya kwanza alipofikishwa mbele ya mahakama au mamlaka nyingine, kitambulisho cha mtekelezaji wa sheria anayehusika na habari kamili juu ya mahali alipofungiwa.*

*Kanuni ya 13: Watu wanaokamatwa wanapaswa kupewa maelezo juu ya haki zao na jinsi ya kuzipata haki hizo.*

## ZOEZI LA NNE

### Kukamata watoto

Wagawe washiriki katika makundi kadhaa. Wape maswali yafuatayo:

(i) Mtoto ni nani kwa mujibu wa sheria za Tanzania?
(ii) Kwa nini mfumo wa utekelezaji wa sheria utoe upendeleo maalum kwa watoto?
(iii) Iwapo ungekua mkuu wa kituo cha polisi na lalamiko likaja mbele yako dhidi ya uhalifu uliotendwa na watoto na una mashaka na uelewa wa sheria na haki za binadamu wa maafisa wako kuhusu sheria ya jinai kwa watoto, je utawatahadharisha vipi kabla hujawatuma kwenda kuwakamata vijana hao wadogo?

## SANDUKU HABARI 2:4

**SHERIA ZA NCHI**

Sheria ya Watoto na Vijana Wadogo - Sura ya 13 ya sheria za nchi

**VIWANGO VYA KIMATAIFA**

1. **Viwango vya masharti ya Chini ya Umoja wa Mataifa katika Kutekeleza Sheria na Haki kwa Watoto: Masharti ya Beijing: Sharti la 10.**
   *(a) Wazazi au walezi wa mtoto aliye kamatwa wataarifiwa mara moja juu ya kukamatwa kwa mtoto*
   *(b) Jaji au afisa yeyote mwenye mamlaka au chombo husika kitafakari bila kuchelewa suala la kuachiwa*

(c) *Mawasiliano kati ya watekelezaji wa sheria na watoto wahalifu yawe katika hali ya kuheshimu hadhi ya mtoto kisheria na yaepuke madhara kwa mtoto kulingana na hali halisi ya kesi husika.*

2. **Mkataba wa Haki za Mtoto: Ibara ya 37 (b)**
*Hakuna mtoto atakayenyimwa uhuru wake kinyume cha sheria au kiholela. Kukamatwa, kuwekwa kizuizini au kifungo cha mtoto lazima iwe ni kwa mujibu wa sheria na itatumiwa kama njia ya mwisho kabisa na kwa muda mfupi tu.*

## ZOEZI LA TANO

### Kukamata Kinyume cha Sheria

Sehemu zilizopita ziliwaruhusu washiriki kupata nafasi ya kuelewa ulingo wa haki za binadamu katika kukamata. Uelewa kiasi wa mambo muhimu, kama nani anaweza kukamata, haki za mtu aliyekamatwa, mazingira yanayoruhusu kukamata na taratibu zinazofaa wakati wa kukamata na njia maalum za kukamata watoto yameshaeleweka.

Kwa ujumla, washiriki sasa wanaelewa kukamata kihalali ni kupi. Hata hivyo katika ngazi hii ni muhimu kuelekeza dira kwenye matukio ya kukamata kinyume cha sheria. Sehemu hii, hasa ina nia ya kuwawezesha watekelezaji wa sheria kuelewa kuwa kama ikitokea mtu kukamatwa / kuwekwa kizuizini kinyume cha sheria yaani kumwondolea uhuru wake kinyume cha sheria basi afisa atahitaji kumlipa fidia mtu aliyekosewa uhuru wake.






Mkufunzi awaelekeze washiriki kukaa katika vikundi na kujadili maswali yafuatayo:

1. Kukamata kinyume cha sheria ni nini? (au vipi)
2. Ni vigezo gani vinavyoonesha kukamata kinyume cha sheria.
3. Ni fidia gani inayoweza kuwepo kwa kukamatwa kinyume cha sheria.
4. Andaa igizo kuonesha jinsi kukamatwa kunavyoweza kuwa kinyume cha sheria.

Baada ya mrejesho washiriki wasaidiwe kujadili vifungu vilivyomo katika masanduku habari hapo chini.

SANDUKU HABARI 2:5

**1. Tendo la kumkamata mtu kinyume cha sheria ni kosa la daawa dhidi ya aliyekamatwa na linapelekea shauri dhidi ya ofisa aliyekamata, jeshi la polisi na serikali kulipa fidia kwa aliyeathirika.**

**2. Kumkamata mtu bila sababu za msingi ina maana kumnyima mtu uhuru wake kinyume na Haki za Kikatiba zilizoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 (kama ilivyorekebishwa) kwa mujibu wa Ibara ya 30 ya katiba mtu atakayetendewa hivyo anaweza kufungua madai ya fidia katika mahakama kuu.**

VIWANGO VYA KIMATAIFA

3. **Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa Ibara ya 9 (4)**
Mtu yeyote aliyeathirika kwa kukamatwa kinyume cha sheria atakuwa na haki ya kulipwa fidia.
4. **Kundi la kanuni za kimataifa iliyojengwa Kulinda Watu Wote Dhidi ya Kuwekwa Kizuizini**
Kanuni ya 35 (1)
Madhara yoyote yatakayotokea kwa matendo au kwa kutotenda kwa afisa wa umma kinyume na haki zilizomo katika kanuni hizi lazima yalipiwe fidia kulingana na masharti yaliyoainishwa kwenye sheria za nchi.

## REJEO

1. Kila mtu ana haki ya kuishi kama mtu huru.
2. Kukamata kunaweza tu kufanyika katika mazingira maalum na kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na sheria.
3. Kukamata kinyume cha sheria ni kosa la daawa na linapelekea madai ya fidia dhidi ya afisa aliyekamata, jeshi la polisi na serikali.
4. Mtoto akikamatwa lazima wazazi / walezi wake wataarifiwe, kuachiwa mara moja lazima kufikiriwe na hadhi yake kama mtoto lazima izingatiwe kuzuia madhara yoyote kwake.

## REJEA

Kwa ufafanuzi zaidi unaweza kurejea:


1. U.N. High Commission for **Human Rights; Human Rights and law enforcement, A manual on Human Rights Training for Police** (professional training services) Geneva Switzerland 1997.
2. Das D and Peter C, **Human Rights and law Enforcement: Lesson Plan**, Dar es Salaam, 1999.

## SURA YA TATU

# UPELELEZI WA POLISI

### Utangulizi

Upelelezi wa makosa ya jinai ni mhimili katika utekelezaji mzima wa usawa na haki katika masuala ya jinai. Kwa hali hiyo basi upelelezi wa makosa ya jinai ni kazi ya msingi katika usimamizi wa usawa na haki. Jinsi upelelezi unavyofanyika inaonesha namna taarifa zinavyopatikana ambazo zitahusisha ukosefu au kutokosa kwa mtuhumiwa ili watekelezaji wa sheria waweze kumfungulia mashtaka. Madhumini ya upelelezi kama kazi mahsusi ya Polisi ni kupata ushahidi, kutambua mtuhumiwa wa uhalifu na kuufikisha ushahidi uliopatikana mahakamani ili iamuliwe iwapo mtuhumiwa ni mhalifu ama sivyo.

Upelelezi wa polisi unaweza kujumuisha kukamata, kupekua, kuweka ndani na kuhoji. Hata hivyo watekelezaji wa sheria wanatakiwa kutumia uwezo huu pale tu inapolazimu na iwapo wana mamlaka kisheria.

### MATARAJIO

Mwishoni mwa sura hii washiriki wanatarajiwa waweze:

1. Kutambua misingi ya kitaalam katika upelelezi
2. Kutambua kwamba heshima na uangalizi wa haki za binadamu katika kufanya upelelezi ni lazima katika kufanikisha matokeo mazuri ya kutambua makosa ya jinai.
3. Kutambua kuwa mtuhumiwa hana hatia na inabidi atendewe kama asiye na hatia hadi itakavyothibitika vinginevyo.

## ZOEZI LA KWANZA

### Upekuzi

Mkufunzi awagawe washiriki katika makundi madogo na kila kundi alipatie kazi ya kuainisha aina za upekuzi na mambo ya kuzingatia kisheria katika kila aina ya upekuzi. Kila kundi lichague mwakilishi atakayefanya mrejesho mbele ya darasa. Mwishoni mwa mrejesho, mkufunzi awaongoze washiriki kujadili misingi ya sheria kama ilivyo katika sanduku habari hapo chini.

**SANDUKU HABARI 3:1**

**Kifungu cha 25 (1) sheria ya Mwenendo wa Makosa ya jinai.**

1. *Polisi ana uwezo wa kusimamisha na kupekua chombo chochote cha majini, mashua, ndege au gari pale ambapo kuna sababu ya kushuku kuwa kuna mali iliyoibiwa, au kuna kitu kilichotumika au kinachoweza kutumika kufanya uhalifu ama kuna silaha au kitu chochote kilichokatazwa kisheria.*

**Kifungu cha 38**

2. *Polisi anatakiwa awe na hati ya kupekua wakati wa kufanya upekuzi. Hati hii inaweza kutolewa na hakimu, mkuu wa kituo cha polisi, afisa yeyote wa polisi mwenye cheo cha msaidizi wa Inspekta au zaidi au afisa yeyote anayekaimu mkuu wa kituo cha polisi.*

**Kifungu cha 40**

3. *Hati ya upekuzi inaweza kutolewa na kutekelezwa siku yeyote (pamoja na Jumapili) na inaweza kutekelezwa katika saa za mchana lakini kwa maombi yanayoweza kutolewa na polisi au mtu mwingine ,mahakama inaweza kuruhusu upelelezi ufanyike saa yoyote.*

**Kifungu cha 26 na PGO Nambari 357 aya ya 5**

4. *Watuhumiwa wanawake watapekuliwa na polisi wanawake au wapekuzi wanawake kwa faragha na kwa staha na heshima.*

5. *Mtu yeyote anaweza kudai kumpekua polisi anayetaka kumpekua kabla ya yeye kuanza kupekuliwa*

**PGO No. 53**

6. *Mfungwa yeyote atakayeingizwa katika mahabusu ya polisi ni lazima apekuliwe vilivyo. Mali zake zitaondolewa kwake ila mavazi tu na atapatiwa stakabadhi (Fomu ya Polisi Nambari 63) inayothibitisha kuwa mali zake zipo mikononi mwa polisi .*

Washiriki waelekezwe kukaa katika makundi madogo na wapewe nakala ya taarifa ya gazeti iliyopo hapa chini, wasome na kujaribu kuainisha mapungufu katika upekuzi uliofanywa na polisi. Vinginevyo mkufunzi anaweza kuwasomea taarifa hiyo.

**THE HERALD 6 Jumatano, January 1999**

POLISI DHIDI YA WAFANYA VURUGU WA MWEMBE KAHAWA

**Polisi "wavamia" nyumba ya Imam**

Na Mwandishi wetu

Wakazi wa eneo la Magengeni nchini Bongo jana wakiwa bado na kumbukumbu ya mauaji ya Mwembekahawa waligutushwa walipoona zaidi ya Polisi 10 wenye silaha wakishuka ndani ya gari lao na kuivamia nyumba ya Shehe Sadiqu Gonga Imam wa msikiti wa Mwembekahawa, Bongo.

Polisi hao wenye silaha wa kikosi cha kuzuia fujo wakiongozwa na Inspekta John Cheche walifanya upekuzi katika nyumba ya Imam huyo majira ya saa tatu asubuhi baada ya mabishano kadhaa na Imam huyo waliposhindwa kumwonesha hati ya upekuzi. Imam huyo alipowaachia waendelee na upekuzi, polisi hao waliamuru watu wote waliomo kwenye nyumba hiyo watoke nje. Karibu askari nusu dazani walisimama mlangoni, wote wakiwa wanaume na walimpekua kwa makini kila aliyetoka ndani. Baadaye polisi hao walipekua kila sehemu ya nyumba na kila kilichokuwa humo ndani. Bila kutaja sababu ya upekuzi huo walitoka ndani ya nyumba hiyo na wakachukua vipande vitano vya chuma ndipo wakamruhusu Imam na familia yake kurudi ndani.

Juhudi zetu za kutaka kumhoji Mkuu wa Polisi wa mkoa hapa Bongo kuhusiana na tukio hili hazikufanikiwa. Katibu Muhtasi wake aliturudisha akisema kuwa mkuu wake hakuwa tayari kuongea na waandishi wa habari kuhusiana na tukio la Mwembekahawa mpaka hapo baadaye itakapotaarifiwa.

Siku ya Ijumaa tarehe mosi Januari vijana wa Kiislam wenye msimamo mkali waliifunga barabara kuu karibu na Mwembekahawa na kuchoma moto magari ya serikali yaliyokuwa yameegeshwa sehemu hiyo. Pia walipambana na Polisi kwa masaa kadhaa. Habari zilizopatikana zinaeleza kuwa vijana watano waliuawa kwa risasi na wengine thelathini waliumizwa vibaya.

## ZOEZI LA PILI

**Mahojiano ya polisi**

**Igizo.**

Mkufunzi agawe washiriki katika makundi mawili. Kundi la kwanza lielekezwe kuandaa igizo fupi linaloonesha hali ambayo pametokea wizi wa kutumia silaha sehemu fulani. Vijana wawili wanashukiwa kuwa wamehusika hivyo wamewekwa chini ya ulinzi wa

polisi. Zaidi ya hapo inasemekana kuna watu waliowatambua vijana hao kwa kuwaona wakitenda kosa hilo. Polisi wawili wanawahoji watuhumiwa hao wawili na watu wengine katika juhudi za kupata ushahidi dhidi ya watuhumiwa hao.

Kundi la pili liandae somo kuelezea Polisi wanavyopaswa kuchukua maelezo kuhusiana na kosa walilotaarifiwa.

Hatimaye, mkufunzi awaongoze washiriki katika kufanya mjadala wa njia inayofaa kufuatwa na watekelezaji wa sheria wakiwa wanawahoji watu kuhusiana na tuhuma za makosa ya jinai, atumie maelezo yaliyo katika sanduku habari hapo chini.

**Sanduku Habari 3:2**

Mahojiano hufanywa na watekelezaji wa sheria ili wapate kufahamu habari na mazingira ya shauri kwa nia ya kuwezesha haki na usawa kuchukua mkondo wake.

**Sheria ya mwenendo wa kesi za jinai**

1. Kifungu 10 (2). Polisi wana uwezo wa kumwita mtu yeyote anayehusika aliyeko katika mipaka ya kituo chao cha polisi au kwenye kituo kilichopo karibu nao kwa nia ya kufanya uchunguzi wa habari na mazingira ya kesi.

2. Kifungu cha 10 (3) Mtu huyo atakapofika kituoni polisi anayefanya uchunguzi anatakiwa kuandika maelezo yoyote yatakayotolewa na mtu anayemuuliza pamoja na ufafanuzi wowote atakaoutoa.

3. Kifungu cha 10 (4) Kabla ya kumuuliza maswali ya uchunguzi, yule Polisi anayefanya uchunguzi anatakiwa amueleze mtu anayehojiwa wajibu alio nao wa kujibu kwa ukweli maswali yote atakayoulizwa kuhusiana na kesi husika, amweleze pia haki yake ya kukataa kujibu swali lolote asilotaka kujibu.

4. Kifungu cha 10 (6) Anayeulizwa aelezewe kwamba maelezo yake yanaweza kutumika kama ushahidi mahakamani katika kesi inayohusika lakini sio kwa kuthibitisha ushahidi wa mtu huyo mahakamani.




## ZOEZI LA TATU

**Kanuni za Haki za Binadamu katika mtiririko wa upelelezi**

Mkufunzi aongoze somo fupi kuhusu kanuni za Haki za Binadamu zinazohusiana na upelelezi wa makosa ya jinai.

- Mtuhumiwa yeyote kuhesabiwa kuwa hana hatia hadi itakapothibitishwa.
- Heshima ya utu, kuthaminiwa na faragha kwa watu wote.

Kama ilivyo katika sheria za nchi na vyombo vya kimataifa

**SANDUKU HABARI 3:3**

## SHERIA ZA NCHI

*Kutokuhesabiwa na Hatia*

**Katiba Ibara 13 (6) (b)**

*Ni marufuku kwa mtu aliyeshtakiwa kwa kosa la jinai kutendewa kama mtu mwenye hatia kabla haijathibitika kuwa ana hatia ya kutenda kosa hilo.*

**Haki ya usawa wakati wa kesi:**

*Katiba Ibara 13 (6)*

*Kwa madhumuni ya kuhakikisha usawa mbele ya sheria mamlaka ya nchi itaweka taratibu zinazofaa au zinazozingatia yafuatayo:-*

*(a)...:.. Mtu kuwa na fursa ya kusikilizwa kwa ukamilifu na pia haki ya kukata rufaa au kupata nafuu nyingine ya kisheria kutokana na maamuzi ya mahakama au chombo kingine chochote kinachohusika.*

*Heshima ya utu wa mtu, uthamani wake na faragha.*

*Katiba Ibara 13 (6)*

*(d).......kwa ajili ya kuhifadhi haki ya usawa wa binadamu, heshima ya mtu itatunzwa katika shughuli zote zinazohusu upelelezi na uendeshaji wa mambo ya jinai na katika shughuli nyinginezo ambazo mtu atakuwa chini ya ulinzi bila uhuru, au katika kuhakikisha utekelezaji wa adhabu.*

*(e).......Ni marufuku kwa mtu kuteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazomtweza au kumdhalilisha.*

## HATI RASMI ZA KIMATAIFA

***1. Kutokuhesabiwa Hatia***

**Tamko la kimataifa la Haki za Binadamu Ibara 11:**

*Mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kosa la jinai atahesabiwa kuwa hana hatia mpaka pale itakapothibitika kisheria mbele ya sheria kwenye mahakama ya wazi akiwa amepata fursa ya kujitetea. Hii pia imeelezwa katika Mkataba wa **Kiafrika wa Haki za Watu na Haki za Binadamu Ibara ya 14 (2)***

***2. Haki ya Kesi Kusikilizwa kwa Haki na Usawa***

***Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu: Ibara ya 10:** Kila mtu anastahili kusikilizwa kwa haki na usawa mbele ya vyombo vya sheria visivyo vya kibaguzi katika kuamua haki na wajibu wake na kwenye kusikilizwa kwa kosa la jinai analoshtakiwa.*

*Yaliyomo katika ibara hii pia yapo vivyo hivyo katika Mkataba wa Kiafrika wa Haki za Watu na Haki za Binadamu Ibara ya 7 na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa ibara ya 14.*

*Mambo ya msingi yanayohakikishwa katika kusikilizwa kwa haki na usawa*

*(a) Ibara ya 9 (2) Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa. Kuelezwa mara moja na kwa ufasaha kosa analotuhumiwa.*

*(b) Ibara ya 9 (2) Kushitakiwa na kesi kuendeshwa bila kucheleweshwa kusikokuwa na sababu.*

*(c) Kupewa nafasi na uwezo wa kuandaa utetezi.*

*(d) Kuwahoji mashahidi dhidi yake.*

*(e) Tamko la Haki za Bindadamu Sura ya 71*

***Ibara ya 14 (3) (9)** Kuwa na uhuru wa kutolazimishwa kutoa ushahidi dhidi yake au kulazimishwa kukiri kosa.*

**3. Heshima ya faragha, kuthaminiwa na Hadhi ya utu.**

**Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu**

**Ibara 12** 'Hakuna mtu atakayeingiliwa katika faragha yake, familia, nyumbani kwake au mawasiliano yake, wala hakuna mtu atakayeshambuliwa hadhi yake au heshima aliyo nayo. Kila mtu ana haki ya kulindwa na sheria dhidi ya kuingiliwa au kushambuliwa huko'.

**Taratibu za Mienendo kwa Maafisa Watekelezaji wa Sheria.**

***Ibara 4** Mambo ambayo ni siri, yaliyo mikononi mwa watekelezaji wa sheria, yanapaswa kuendelea kuwa siri labda pale ambapo katika kutimiza wajibu au kwa ajili ya kutenda haki na usawa itahitajika vinginevyo.*

Baada ya mjadala huu wagawe washiriki katika makundi na uwapatie zoezi lifuatalo:

## ZOEZI LA NNE

### KUNDI LA KWANZA

Hebu fikiri kama ungekuwa afisa wa Polisi katika idara ya upelelezi wa makosa ya Jinai. Amri imetolewa kwako kutoka kwa mkuu wa upelelezi wa makosa ya Jinai wa mkoa ukafanye upelelezi eneo fulani ili kuwakamata na kuwafungulia mashtaka wasafirishaji wa madawa ya kulevya ambao inasemekana wanafanya mipango yao ya madawa katika eneo hilo. Elezea hatua kwa hatua jinsi utakavyofanya upelelezi huo ukizingatia viwango vya kimataifa vya Haki za Binadamu.

**KUNDI LA PILI**

Fikiria kuwa wewe ni mkuu wa kikosi maalum cha Polisi kilichoundwa kupambana na rushwa nchini. Tayarisha taratibu za utekelezaji ili ziwe mwongozo wa wapelelezi katika kufanya upelelezi kwa njia inayokubalika kimaadili.

**KUNDI LA TATU**

Eleza sababu za kuwepo na misingi ifuatayo:

(i) Kutokuhesabiwa hatia kabla ya kuthibitika
(ii) Haki ya kusikilizwa kwa haki na usawa
(iii) Heshima ya faragha ya mtu
(iv) Uangalizi wa haki ya utu na thamani ya hadhi yake.

## REJEO

1. Mtuhumiwa anabaki kuwa hana hatia katika ngazi zote za upelelezi mpaka hapo atakapothibitishwa na mahakama kuwa na hatia.

2. Kila mtu kwa usawa anapaswa kupata haki na usawa mbele ya vyombo vya sheria wakati wa kushtakiwa hivyo ana haki ya kuelezewa kosa dhidi yake, anapaswa afunguliwe mashtaka na kesi yake iendeshwe bila kucheleweshwa, kujitetea, kuhoji mashahidi na awe huru kwa kutolazimishwa kutoa ushahidi dhidi yake au dhidi ya wengine.

3. Haki ya faragha na utu wa mtu lazima vilindwe kwa hali yoyote ile.

## REJEA

Kwa kupata ufafanuzi zaidi unaweza kurejea yafuatayo:


1. UN Commission for Human Rights:

   **Human Rights and Law Enforcement: A manual on Human Rights training for Police (Proffesional training series No. 5) Geneva Switzerland, 1997)**

2. Das D and Peter C. **Human Rights and law enforcement: Lesson Plan, Dar es Salaam 1999.**

## SURA YA NNE

# KUWEKA KIZUIZINI

### Utangulizi

Ili watekelezaji wa sheria waweze kufanya baadhi ya kazi ya upelelezi ikiwemo kuhoji, ni lazima uhuru wa kutembea tembea wa mtuhumiwa uzuiliwe. Ili kufanikisha hili, mfumo wa kisheria Tanzania unaruhusu watekelezaji wa sheria kumweka chini ya ulinzi mtu yeyote ili waweze kufanikisha upelelezi wa kosa linalotuhumiwa.

Sura hii inalenga watu walio chini ya ulinzi wa polisi. Ili mtu awe chini ya ulinzi wa polisi lazima awe ameongozana na polisi au yuko na polisi kuhusiana na kosa linalotuhumiwa, kiasi kwamba haruhusiwi kuondoka hata kama angetaka kufanya hivyo. Kifungu cha 5 (1) cha sheria ya Mwenendo wa makosa ya jinai.

Hii pia inamhusu mtu aliyeko sehemu fulani kwa amri ya Polisi akisubiri, kuhusiana na kosa lililotokea. Hata hivyo kwa vile aliye chini ya ulinzi amenyimwa uhuru wake (na kwa hali hii bado hajapatikana na hatia) yupo katika hatari ya kutendewa vibaya.

Kwa uelewa huu, sura hii inajaribu kuwahamasisha watekelezaji wa sheria kuwatendea watu walio chini ya ulinzi wao kabla hawajapatikana na hatia kwa hali ya kiutu wakiongozwa na sheria zinazohusu jinsi ya kuwatendea watu walio chini ya ulinzi wa polisi.



## MATARAJIO

Mwishoni mwa sura hii washiriki wataweza.

1. Kuelewa kwamba kumweka mtu chini ya ulinzi kuna mwondolea haki yake ya kuishi kama mtu huru hivyo mamlaka ya kuweka mtu chini ya ulinzi yatumiwe katika mipaka ya sheria au kulingana na sheria.
2. Kuelewa kwamba watekelezaji wa sheria wanapaswa kuwatendea walio chini ya ulinzi kiutu.
3. Kuelewa kwamba kutesa watu kumekatazwa kabisa.
4. Walio chini ya ulinzi wanatakiwa kufikishwa mahakamani mara moja au waachiliwe.

## ZOEZI LA KWANZA

Mkufunzi awagawe washiriki katika makundi madogo madogo. Awapatie kila kundi mahojiano yaliyo katika kisanduku hapo chini na awaelekeze kusoma na kujadili na kujibu maswali chini yake.

Haya ni maongezi kati ya Mabula ambaye ni Mkuu wa Kituo cha Polisi Chambuzi na Koplo Lugoye walipokuwa wakinywa kwenye klabu ya VIP huko Tanga:

**Mabula:** Nilitaka kukuuliza swali moja.

**Lugoye:** Swali gani afande?

**Mabula:** Ngoja kwanza niagize kinywaji. Aloo! Shangazi, hebu tupatie Safari moja na Kilimanjaro moja zote baridi.

**Mhudumu:** Sawa mzee, Nitaleta mara moja

**Mabula:** Sasa Lugoye! Hivi wale makonstebo walikuletea yule mkorofi Kanoti.

**Lugoye:** Ndio afande. Walimleta na nimemweka ndani. Hivi tunapoongea yuko ndani.

**Mabula:** Vizuri. Unajua yule mtu mkorofi sana. Amekopa fedha kutoka kwa rafiki yangu John na hataki kulipa hilo deni. Tukapanga na John tumsweke ndani kwa siku kama tano hivi; akitoka hapo ataelewa maana ya wajibu alio nao wa kulipa deni.

**Lugoye:** Kwa hiyo afande hiyo ndio sababu ya kumweka ndani? Unajua niliwauliza wale makonstebo kwa nini wamemkamata wakasema tu afande kasema awekwe ndani.

**Mabula:** Ndio, na nakwambia hakikisha anakaa siku tano. Na akileta ukorofi wake mpatie kibano kidogo si ndio! Nina maana mpige akileta usumbufu.

**Luyoye:** Sawa afande!

| | |
|---|---|
| **Mabula:** | Nakwambia usimwachie mpaka usikie toka kwangu. |
| **Lugoye:** | Sawa afande! |

**SWALI LA KUJADILI**

Fikiri kuwa wewe ni Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Haki za Binadamu na bahati ulikuwepo katika klabu hiyo ya VIP Tanga. Na ikatokea kuwa uliyasikia mazungumzo ya Polisi hao wawili, Lugoye na Mabula. Baadaye suala hili linaletwa kwako kiofisi na mlalamikaji kwamba kweli aliwekwa ndani siku tano na kuachiwa baadaye. Sasa unataka kuandika lalamiko kwa Mkuu wa Polisi wa Taifa kuhusu tabia ya Polisi wa kituo cha Polisi Chambuzi kwa vile umeona wamekiuka sheria za Polisi na viwango vya Haki za Binadamu. Je utayawekaje malalamiko hayo?

Mkufunzi waongoze washiriki kujadili misingi ya sheria na Haki za Binadamu kama yalivyowekwa katika sanduku hapo chini.

**Sanduku Habari 4:1**

**SHERIA ZA NCHI**

*Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kifungu cha 5 (1)*

*Ili mtu aweze kuwa chini ya ulinzi ni lazima aandamane au awe na polisi kuhusiana na kosa la jinai kiasi kwamba polisi asimruhusu kuondoka hata kama angetaka kuondoka.*

**KIFUNGU CHA 5 (3)**

*Mtu pia atakuwa chini ya ulinzi wa polisi ikiwa kwa amri ya afisa polisi ametakiwa asubiri sehemu fulani kwa sababu zinazohusiana na kosa la jinai.*

**KIFUNGU CHA 5 (2)**

*Kuwekwa ndani kihalali ni pale ambapo ni matokeo ya kukamatwa kwa mujibu wa sheria au kuitwa mbele ya chombo cha sheria kwa mujibu wa sheria.*

**KIFUNGU CHA 32**

*Mtu hatakiwi kuwekwa ndani kwa zaidi ya masaa 24 kwa makosa aliyokamatiwa labda tu akiwekwa ndani kuhusiana na kosa lenye adhabu ya kifo.*

**KIFUNGU CHA 49**

*Mtu hapaswi kuwekwa chini ya ulinzi kwa kosa lile lile ambalo alishawekwa tena chini ya ulinzi labda tu kwa mambo ambayo yanahusiana na kosa hilo na hayakuwa*

*wazi au kujulikana na polisi wakati alipowekwa chini ya ulinzi mara ya kwanza au ikiwa muda wa kutosha umepita tangu mtu huyo alipoachiwa mara ya mwisho.*

**KIFUNGU CHA 50 (1)**
*Mtu aliyewekwa chini ya ulinzi hatakiwi kuhojiwa na polisi kwa zaidi ya masaa manane labda muda uongezwe kufikia masaa manane kwa sababu maalumu au kwa masaa ambayo hakimu anaweza kuongeza kama anavyoona inafaa baada ya kupewa maombi maalumu.*

**KIFUNGU 50 (3)**
*Hakimu hapaswi kukubali maombi ya kuongeza muda wa kumweka mtu rumande ila pale ambapo ataridhika kuwa kuwekwa huko ndani ni kwa mujibu wa sheria, na kwamba upelelezi umefanywa na unaendelea kufanyika kwa haraka iwezekanavyo na ni lazima kuongeza huo muda. Mtu anayehojiwa yeye binafsi au kwa kupitia mwana sheria wake atapewa nafasi ya kujibu hoja za maombi ya kuongeza muda.*

**KIFUNGU CHA 50 (2)**
*Muda wa kuwekwa ndani ukiongezwa na polisi kwa sababu zisizo za kimsingi aliyewekwa ndani anaweza kufungua mashtaka kudai fidia dhidi ya muda huo ulioongezwa.*

**KIFUNGU CHA 52**
*Katika hali ambayo hakuna kumkamata mtu bila hati ya kukamatia na imekuwa kwamba kuna kosa kubwa la jinai limefanyika na kuna watu wanaotuhumiwa kwa kosa hilo, afisa wa polisi akikamata mtu hatakiwi kumwuuliza maswali yoyote mtuhumiwa huyo labda tu awe amemtahadharisha kuwa ana haki ya kutokujibu maswali watakayomwuliza.*

**KIFUNGU CHA 46 (2)**
*Polisi atatakiwa kumweleza aliyetiwa nguvuni kuwa, kisheria ni lazima atoe maelezo kuhusiana na jina lake na anuani yake na akikataa kufanya hivyo au akitoa maelezo ya uongo ataadhibiwa kwa mujibu wa sheria.*

**KIFUNGU CHA 52 (2)**
*Baada ya kuarifiwa kuwa ana uwezo wa kukaa kimya, aliyewekwa chini ya ulinzi anapaswa kuelezea katika fomu maalumu kwamba alipewa taarifa hiyo. Maelezo yake lazima yawe na tarehe, muda na maelezo aliyopewa, kinyume na hivi itafanya maelezo yote aliyotoa yasipokelewe kama ushahidi kwa mujibu wa (kifungu cha 169).*

**KIFUNGU CHA 53**
*Ikiwa aliyewekwa ndani hatatoa maelezo ya kupewa taarifa katika fomu husika kama kutatokea ubishi katika suala hilo, itachukuliwa kuwa mtuhumiwa hakuwa amepewa taarifa hiyo.*

**KIFUNGU CHA 53 (4)**
*Kama itaamuliwa kwamba anayetuhumiwa kufanya kosa afunguliwe mashtaka, basi polisi anayehusika baada ya kumfungulia mashtaka lazima amtahadharishe mtuhumiwa kwa maneno au kwa maandishi, kumwelezea kwamba sasa ameshafunguliwa mashtaka kwa kosa fulani na kwamba ana haki ya kutojibu swali lolote atakaloulizwa zaidi ya swali litakalohusu jina au anuani yake.*

**KIFUNGU CHA 52 (4)**
*Polisi lazima amweleze mtuhumiwa hatari ya kushindwa au kukataa kujibu maswali kwa usahihi au kuelezea jambo ambalo linahusiana na mashtaka dhidi yake kwa kuwa kukataa au kushindwa huko kunaweza kuleta athari mbaya dhidi ya mtuhumiwa.*

**KIFUNGU CHA 63 (a) NA (c) (1) KIFUNGU CHA 54**
*Baada ya tahadhari hiyo swali lolote lisiulizwe mpaka mtuhumiwa aambiwe jina na cheo cha polisi anayehusika na haki yake yenye masharti ya kuwasiliana na jamaa, rafiki au mwanasheria wake.*

**KIFUNGU CHA 54**
*Labda ikionekana kuwa kuna hofu ya msingi kwamba mtuhumiwa anaweza kutoroka, kupoteza ushahidi au kutunga ushahidi anaweza kuzuiwa kuwasiliana na jamaa zake. Vinginevyo, polisi anatakiwa akiombwa na mtuhumiwa amruhusu na kumwezesha kuwasiliana na ndugu, rafiki, au mwanasheria wake.*

**KIFUNGU CHA 58**
*Ikiwa ni suala la mtoto, polisi anayehusika na upelelezi wa kosa atatakiwa kuwataarifu wazazi au walezi wa mtoto aliyewekwa ndani kuhusu kuwekwa huko ndani na sababu zake.*

**KIFUNGU CHA 55**
*Iwapo aliyewekwa ndani ataugua, matibabu, ushauri na msaada wa kiafya lazima utolewe kwake. Mtu akiwekwa ndani anapaswa atendewe kiutu na kwa kuheshimu utu wake. Hakuna mtu atakayestahili kufanyiwa ukatili au kutendewa kinyama na kudhalilishwa akiwa amewekwa ndani.*

**KIFUNGU CHA 64 (1)**

*Aliyetuhumiwa itabidi aachiwe mara moja pale itakapodhihirika kuwa hakutenda kosa au hakuna sababu za msingi za kuendelea kumshikilia au aliyewekwa ndani siyo mwenye tuhuma au masaa ishirini na nne yamepita kabla mashtaka hayajafunguliwa dhidi yake, labda tu kosa analotuhumiwa liwe ni zito sana.*

**KIFUNGU CHA 64 (2)**

*Hata kama aliyeshikiliwa na polisi atakuwa amefunguliwa mashtaka anapaswa kuachiliwa pale ambapo atachukua mdhamana wa polisi wenye udhamini au hata bila udhamini pale ambapo mtu huyo alikamatwa bila hati na kosa lenyewe si zito au iwapo upelelezi ambao haujakamilika katika muda mfupi umekwishafanyika.*

**KIFUNGU CHA 64 (3)**

*Kwa suala linalohusu mtoto, ataachiliwa mara atakapojitokeza mzazi au mlezi au jamaa yake au mtu mwingine anayeaminika.*

**KIFUNGU CHA 64 (4)**

*Hakuna ada au ushuru utakaotozwa kwa dhamana za makosa ya jinai.*

**KIFUNGU CHA 64 (5)**

*Polisi yeyote anayemkamata mtu anayeshukiwa kutenda kosa anapaswa amtaarifu mtu huyo haki aliyo nayo ya dhamana chini ya kifungu hiki cha sheria.*

## VIWANGO VYA KIMATAIFA VYA HAKI ZA BINADAMU

**Kuzuia utesaji**

- **Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu ibara (5)**

  *Hakuna mtu anayepaswa kupata mateso au kufanyiwa ukatili au kutendewa katika hali ambayo itamdhalilisha au kumshushia hadhi yake au kuadhibiwa.*

  *Kifungu kama hiki pia kipo katika Mkataba wa Kiafrika Kuhusu Haki za Watu na Haki za Binadamu (ibara ya 5) Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ibara ya 7).*

- **Tamko la Kulinda Watu Wote Dhidi ya Kuteswa na Matendo Mengine ya Kikatili, Udhalilishaji au Adhabu.**

  *Utesaji ni maumivu makali au mateso yawe ya kimwili au kiakili yanayofanyiwa au yanayoamriwa kufanyiwa mtu kwa nia ya kupata kutoka kwake au kwa mtu mwingine habari, au kukiri jambo, kumwamdhibu kwa jambo fulani alilotenda au analoshukiwa kutenda au kumdhahlilisha yeye au mtu mwingine.*

**Ibara ya 2**
*Kila nchi iliyo mwanachama inapaswa kuchukua hatua za kufaa za kisheria, kiutawala na kimahakama au hatua nyingine zozote, kuzuia matendo ya utesaji katika eneo lolote ndani ya mipaka ya nchi yake.*

*Hakuna sababu zozote zitakazotolewa, iwe ni vita, hofu ya vita, hali ya wasiwasi kisiasa, kimataifa au hali nyingine yeyote ya dharura ili kuhalalisha utesaji. Amri kutoka kwa mkuu au kwa mamlaka ya juu haiwezi kutumiwa kuwa kinga ya kuhalalisha utesaji. Hii pia imeelezwa katika Taratibu za Mienendo Kwa Maafisa Watekelezaji wa Sheria (ibara ya 5).*

- **Kuwatendea walio ndani kwa hali ya kiutu.**

  *Watu wote walionyimwa uhuru wao watendewe kwa hali ya kiutu na kwa heshima ya utu wao kama binadamu. Watuhumiwa watenganishwe na wahalifu na watendewe kwa hali tofauti kulingana na hadhi zao kama watuhumiwa. Watoto wanotuhumiwa wawekwe sehemu tofauti na watu wazima.*

**Kundi la kanuni za kuwalinda Watu Walio Chini ya Aina Yoyote ya Kifungo au Kizuizini inaelezea ifuatavyo.**

*(a) Ukaguzi wa kisheria wa mahabusu/wafungwa*
*(b) Haki ya kuwasiliana na mwanasheria.*
*(c) Haki ya kuwasiliana na kuwa na mawasiliano na familia.*
*(d) Waliowekwa ndani wapatiwe huduma za Afya/matibabu*
*(e) Maelezo yeyote yanayohusu mahojiano na mtuhumiwa yaandikwe.*

**3. Watoto waliowekwa ndani.**

**Vipimo vya msingi vya Umoja wa Mataifa kuhusu Masharti ya Kuendesha Masuala ya Haki na Usawa Kwa Watoto (masharti ya Beijing).**

**Sharti la 5.**
*Mfumo wa haki na usawa kwa watoto lazima usisitize usalama wa mtoto na uhakikisho kuwa kushughulikia watoto wahalifu lazima kila mara kulingane na hali halisi ya watuhumiwa hao na kosa lenyewe.*

**Sharti la 10.1 na 10.2**
*Wazazi na walezi wa mtoto lazima waarifiwe mara moja anapokamatwa na chombo kilichomkamata lazima kififikirie suala la kumwachia mtoto bila kuchelewa.*

**Sharti 11.**

*Polisi wenye mamlaka maalumu wanaweza kulimaliza suala linalomhusu mtoto bila kulipeleka mbele kila inapowezekana.*

**Sharti la 12**

*Ni polisi wenye ujuzi wa kushughulikia watoto na vituo maalumu vya kushughulikia watoto tu wanaopaswa kushughulika na watoto na makosa yanayofanywa na watoto. Haya yameelezewa pia katika Masharti ya Umoja wa Mataifa ya Kuwalinda Watoto Walionyimwa Uhuru na pia kwenye Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto.*

**Wanawake waliowekwa ndani**

**Viwango vya msingi vya Masharti ya Jinsi ya Kuwatendea Wafungwa**

Makundi tofauti ya wafungwa yatawekwa mahali tofauti au sehemu tofauti katika eneo moja kulingana na jinsia, umri na taarifa za uhalifu n.k. Wanaume na wanawake kwa kadiri itakavyowezekana wawekwe jela tofauti. Katika jela inayopokea wanawake na wanaume sehemu watakazokaa ziwe tofauti.

Mwisho wa majadiliano, mkufunzi awagawe washiriki katika makundi madogo na awagawie kadi moja kwa kila kundi.

Kadi 1

**Mary ana miaka arobaini. Ni mjane mwenye watoto watano. Anauza pombe haramu ya gongo ili apate fedha za kuitunza familia yake. Siku moja anakamatwa na polisi. Anaamriwa abebe vifaa anavyotumia katika biashara yake ambavyo ni vizito sana kwake. Akiwa njiani kuelekea Kituo cha polisi anaanguka mara kadhaa. Kila mara polisi aliye naye anamtukana, anampiga mateke na kumwamuru kusimama na kubeba msalaba wake kuelekea kalvare.**

Kadi 2

**Mashavu ni Mbunge wa chama cha upinzani kiitwacho FCU. Panatokea njama za kutaka kuiangusha serikali iliyoko madarakani ya chama cha MCM. Mashavu anatuhumiwa kwa njama hizo na kukamatwa. Anapelekwa Kituo cha Polisi cha Kahawani kwa mahojiano. Ananyang'anywa miwani yake jambo ambalo linamsababishia maumivu ya kichwa. Hapo hapo anaambiwa kuwa binti yake ambaye anatakiwa kuondoka kesho yake kwenda masomoni Uingereza (na ndege ya siku hiyo hiyo) amekamatwa na yuko kwenye Kituo kingine cha Polisi. Anaambiwa kwamba kama asipotoa habari ya jinsi alivyohusika katika**

**njama hizo, na alioshirikiana nao hatapewa miwani yake na binti yake hataondoka kwenda Uingereza.**

**Kadi 3**

**Mwamba ni mtoto wa mtaani. Ana umri wa miaka 14. Amekamatwa na polisi akivuta bangi. Amepelekwa Kituo cha Polisi Ostabai. Hapo anazungumza kwa furaha na watu wazima wanaoshikiliwa na polisi. Maongezi yao yanachekesha angalau wanaweza kubadilishana mawazo juu ya uzoefu wao katika uhalifu.**

**Kadi 4**

**Kimaro yupo Kituo cha Polisi Ostabai Amekamatwa kwa tuhuma za kusafirisha madawa ya kulevya. Anaomba aongee na mwanasheria wake kabla hajajibu swali lolote. Polisi wanasita kumpa ruhusa ya kuwasiliana kwa hofu kuwa ushahidi unaweza kupotezwa na akaandaa njia ya kutoroka.**

**Kadi 5**

**Rasheed amekamatwa na polisi kwa maelezo yake mwenyewe kwamba ametega bomu sehemu fulani hapo jijini. Kwa maelezo yake hilo bomu litalipuka saa yoyote kuanzia sasa. Ameapa kuwa hatatoa taarifa ya lilipo hilo bomu. Polisi mmoja anampiga mateke mara kadhaa kwenye sehemu zake za siri. Analia kwa uchungu na anakubali kutoa taarifa ambayo inasaidia kugundua bomu kabla halijalipuka.**

## Zoezi la pamoja

1. Watake washiriki waoneshe haki za binadamu zilizokiukwa katika kila kadi. Kila kundi lichague mwakilishi atoe maelezo yao mbele ya washiriki wengine.

2. Wasaidie washiriki kuandaa kipindi cha Runinga kama ifuatavyo;

Mchague mshiriki mmoja atakayechukua nafasi ya mtangazaji wa mtandao wa Taifa wa Runinga. Kisha wagawe washiriki katika makundi. Elekeza kila kundi kujadili msingi mmoja wa haki za binadamu na kuangalia maana au ulazima wake. Kila kundi limchague mwakilishi atakayekwenda kwenye mahojiano ya Runinga katika kipindi "Maongezi ya wiki".

**Ifuatayo ndio misingi**

1. Kwa walio chini ya ulinzi wa Polisi;
2. Uhuru wa kutoteswa
3. Kutendewa kiutu
4. Kutokuwekwa ndani kwa muda mrefu bila sababu

5. Haja ya kuwatendea watoto katika hali maalum
6. Haja ya wanawake kushughulikiwa na polisi wanawake.

## REJEO

1. Uhuru wa kutoteswa ni haki ya lazima
2. Watu wote walionyimwa uhuru lazima watendewe kwa heshima ya utu wao kama binadamu.
3. Watoto wanaowekwa ndani wapatiwe matunzo maalum kwa mujibu wa sheria na kwa viwango vya kimataifa vya haki za binadamu.
4. Muda wa mtu kuwa chini ya ulinzi wa polisi uwe mfupi kiasi inavyowezekana.

5. Wanawake waliofungwa washughulikiwe na polisi wanawake.

## REJEA

Kwa ufafanuzi zaidi unaweza kurejea yafuatayo.


1. UN High Commission for Human Rights: **Human Rights and law Enforcement: A manual on human rights training for police (Professional training series No. 5)** Geneva Switzerland.
2. Das D and Peter C, **Human Rights and Law Enforcement: Lesson plan, Dar Es Salaam 1999.**

## SURA YA TANO

# MATUMIZI YA NGUVU NA SILAHA

**Utangulizi**

Mamlaka makuu ya polisi yanaelezewa kuwa ni kulinda amani, kusimamia sheria na utulivu, kuzuia uhalifu na kuchunguza ili kugundua uhalifu kabla haujatokea, kukamata na kuweka wahalifu rumande na kulinda mali za raia.

Kwa vile Polisi wamepewa uwezo mkubwa sana juu ya raia, inabidi waangalie sana pasije kuwa na uwezekano wa kutumia uwezo wao huo vibaya. Ni wazi kuwa wakati mwingine polisi wana uwezo wa kutumia nguvu, kama uwezo huu ukitumika vibaya unaweza kuathiri haki za watu. Sura hii ina nia ya kutathmini uwezo wa polisi wa kutumia nguvu na mipaka yake. Pia ina madhumuni ya kutoa kwa uwazi ufafanuzi wa hali ambayo nguvu inaweza kutumika. Vile vile ina kusudi la kuwapatia polisi wajibu mkubwa wa kuhakikisha kuwa mamlaka walio nayo ya kutumia nguvu yatumike kwa mujibu wa sheria na kwa manufaa fulani.

### MATARAJIO

Mwishoni mwa sura hii washiriki watakuwa wametambua:-

1. Mazingira yanayoruhusu utumiaji wa nguvu.
2. Wajibu wa Polisi kuhakikisha kuwa matumizi ya nguvu yanafanyika kwa mujibu wa sheria.
3. Viwango katika kutumia nguvu na silaha.

## ZOEZI LA KWANZA

**Mwongozo na njia mbali mbali za kutumia silaha**

Mkufunzi awaongoze washiriki kujadili misingi ya kisheria ifuatayo na awaelekeze kujibu maswali yanayofuata:-

**Misingi ya kisheria.**

1. Silaha zitumike tu katika mazingira ambayo ni ya lazima sana.
2. Silaha zitumike kwa kujitetea binafsi au kutetea wengine dhidi ya tishio la kifo au madhara makubwa, au
3. Kuzuia uhalifu fulani ambao unahusu tishio la kupoteza maisha.

4. Kukamata au kuzuia mtu anayetishia maisha, kutotoroka akiwa anakataa kuacha tishio hilo hata baada ya juhudi kufanyika na
5. Katika kila hali silaha itatumika pale tu ambapo njia nyingine hazifai.
6. Kutumia nguvu na silaha kwa makusudi kutaruhusiwa pale tu ambapo kumetumiwa kulinda uhai wa binadamu na hapakuwa na njia nyingine.
7. Polisi atoe tahadhari ya wazi kabla hajaamua kutumia nguvu.

## SANDUKU HABARI 5.1

### HATI RASMI ZA KIMATAIFA

**Kanuni za Msingi Katika Matumizi ya Nguvu na Silaha**

**Mazingira yaliyovuka mpaka (kutisha)**

*Ibara ya 45 inawataka watekelezaji wa sheria kutumia njia za kawaida kabla ya kuamua kutumia nguvu au silaha. Wanaweza kutumia nguvu au silaha ikiwa tu njia nyingine hazifai au hazitaleta matokeo yaliyokusudiwa.*

**Kujihami na kuokoa maisha.**
*Ibara ya 9 inawataka watekelezaji wa sheria kutumia silaha dhidi ya mtu kwa kujihami au kuzuia wengine walio katika hatari ya kifo au madhara makubwa.*

**Kutoa tahadhari**
*Ibara ya 10 inawataka watekelezaji wa sheria kujitambulisha na kutoa onyo au tahadhari ya nia yao ya kutumia silaha.*

### SHERIA ZA NCHI.

Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (Na. 9 ya 1985).

**Kujihami/kuokoa maisha.**

**Kifungu cha 21 (2) kinaelezea:**
*Bila kupunguza uwezo wa kutumika kwa kifungu kidogo cha (1) wakati wa kumkamata mtu polisi hatakiwi kufanya kitendo kinachoweza kusababisha kifo cha mtu huyo, labda kama polisi huyo anaamnini kwa sababu za msingi kwamba kwa kutenda tendo hilo ni muhimu katika kuokoa maisha na kuzuia madhara makubwa kwa watu wengine.*

**Sheria ya Polisi (Sura ya 322)**

**Kifungu cha 29 kinaeleza:**

*Matumizi ya silaha yatafanywa na polisi pale tu mtu aliye chini ya ulinzi wa polisi kwa kutuhumiwa au kwa kutiwa hatiani anapotoroka au anapojaribu kutoroka. Polisi akiwa na sababu za kufaa za kuamini kuwa hana njia nyingine ya kuzuia utoro huo na amekwisha toa tahadhari kwa huyo mtu kuwa atatumia silaha na huyo mhusika hakutii.*

**au**

*Inaweza kutumika dhidi ya mtu ambaye kwa nguvu anamuokoa au anajaribu kuzuia kukamatwa kihalali kwa mtu mwingine na pale ambapo polisi ana sababu za kufaa za kuamini kuwa yeye au mtu mwingine yuko katika hatari ya kupata madhara makubwa ya mwili.*

**Maswali ya kufanyia kazi.**

1. Kwa nini pawe na taratibu za matumizi ya silaha.
2. Je! Unajua/kumbuka tukio la utumiaji wa silaha kwa polisi wa Tanzania ? Je! Utumiaji huo uliangukia katika mazingira yanayokubalika? Athari gani za moja kwa moja au za papo kwa papo zilizogusa haki za watu? Je! Wanasiasa, watu wa madhehebu ya dini na jumuiya kwa ujumla walichukuliaje hali hiyo?
3. Je! Inawezekana kuzuia polisi kutumia silaha?
4. Orodhesha haki za binadamu zinazoweza kukiukwa ikiwa Polisi watatumia silaha.

## ZOEZI LA PILI

**Matumizi sahihi ya nguvu na silaha.**



**Misingi ya Uwiano na mantiki.**

Pitia misingi na sheria katika masanduku ya habari. Wagawe washiriki katika makundi matatu. Waelekeze kila kundi kujadili msingi mmoja na kuonesha kwa vipi msingi huo unatimizwa hapa Tanzania. Mkufunzi apitie kila kundi na kuwasaidia kuchangia uzoefu wao. Kama msingi haufuatwi ni kwa nini? Na katika hali hiyo je! Kuna ukiukwaji wa haki?

**Msingi wa uwiano**

Msingi huu wa uwiano unahitaji matumizi ya nguvu yawe kwa uwiano yaani nguvu itumike kwa kadri inavyoweza kukubalika katika kutekeleza sheria na kuhakikisha utulivu wa umma. Kinachotakiwa ni matumizi ya wastani kulingana au kwa uwiano na upinzani unaotolewa na mtuhumiwa.




**Msingi wa Kimantiki**

Ni suala la mjadala kutegemeana na hali halisi ya kila tukio iwapo kiasi cha nguvu kilichotumika kilikuwa ni sahihi au sivyo. Kwa mfano kukamata kunaweza kuwa ni kwa mujibu wa sheria, lakini kukawa na dosari ya kuwa kinyume na sheria kwa kutumia nguvu isivyostahili. Hii iliamuliwa katika kesi ya Mbui dhidi ya Dyer (1967) E. A. 315. Uamuzi wa aina hiyo hiyo ulitolewa na Mahakama hiyo hiyo ya Afrika Mashariki katika kesi ya Musembi Kikoma na wengine dhidi ya Serikali ( 1957) E. A. 422.

## SANDUKU LA HABARI 5:2

*Vyombo vya kimataifa na hata sheria za nchi zinakataza Polisi kufanya matumizi ya nguvu kupita kiasi na matumizi ya nguvu yasiyo ya lazima.*

**Msingi wa uwiano.**

**Taratibu za Mienendo Kwa Maafisa Watekelezaji wa Sheria – Ibara ya 3**

*"Watekelezaji wa sheria wanaweza kutumia nguvu pale tu ambapo ni lazima sana kufanya hivyo na kwa kiasi kinachohitajika katika kutekeleza wajibu wao".*

**Ibara ya 5 (a) inaeleza:**
*Kila inapolazimika kutumia nguvu au silaha kwa mujibu wa sheria, watekelezaji wa sheria lazima watumie kiasi katika matumizi hayo ya nguvu au silaha na wafanye kwa uwiano kulingana na uzito wa kosa na madhumuni ya kisheria yanayotegemewa kupatikana kwa tukio hilo.*

*Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (namba 9/1985 kifungu cha 1 (1) inaelezea kuwa inatosha kwa polisi kumgusa mwili mtuhumiwa wakati polisi akiwa katika kutekeleza wajibu wake wa kumkamata mtuhumiwa.*

**Kifungu cha 21 (1)**
*Polisi au mtu mwingine yeyote haruhusiwi kutumia nguvu zaidi ya inavyolazimu au kumdhalilisha mtuhumiwa wakati wa kumkamata au kumzuia mtu aliyekwisha kamatwa.*

**Mantiki**
Wajibu wa polisi wa kuhakikisha kuwa mamlaka yao ya kuzuia uhalifu hayawapi uwezo wa kutumia nguvu isivyostahili yameelezewa pia katika:-

1. **Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, kifungu cha 21 (1)**

2. **Sheria ya Kanuni za Adhabu (kifungu cha 18 B (1).**

*Katika kutumia haki ya kujihami au kulinda wengine au mtu mwingine au kulinda mali, mtu anaweza kuruhusiwa tu kutumia nguvu zinazostahili na zitakazolazimu katika ulinzi huo.*

**Angalizo**
**Nguvu ya kuzidi inayostahili itaweza kutumika tu, katika hali mbaya sana hasa mahali ambapo kuna vurugu zinazopelekea mtu kujihami. Vinginevyo, polisi anaweza kupatikana na hatia kwa kosa la jinai au daawa.**

**Kanuni za Adhabu (Sura ya 16) kifungu cha 18 B (2)**

1. *Kila mtu atapatikana na hatia kwa kosa la jinai linalotokana na matumizi ya nguvu ya kupita kiasi wakati akijihami au akimtetea mtu mwingine au akitetea mali.*

2. *Mtu yeyote atakayesababisha kifo cha mtu mwingine kutokana na matumizi ya nguvu kupita kiasi aliyotumia kujihami atapatikana na hatia ya kuua bila kukusudia.*

## ZOEZI LA TATU

**Amri zisizo halali na matumizi ya nguvu na silaha.**

Wapatie washiriki maelezo yaliyo kwenye sanduku. Hakikisha kila mmoja ameelewa maelezo hayo. Wagawe washiriki katika makundi madogo na uwaelekeze kujadili maswali yafuatayo.

1. Kwa nini sheria za kimataifa na hata sheria za nchi hazikubali amri isiyo halali kutoka kwa mkuu kama kigezo cha kukiuka haki za binadamu? Je! Polisi anayekataa kutii amri isiyo halali toka kwa mkuu wake ya kutumia nguvu au silaha analindwa au ana kinga katika sheria za Tanzania?

2. Ni ugumu gani unaoweza kumpata polisi katika Jeshi la Polisi Tanzania ikiwa atakataa kutii amri isiyo halali ya mkuu wake. Je! Ugumu huo unaweza kutatuliwaje?

3. Ni kwa jinsi gani Jeshi la Polisi linaweza kurahisisha hali ya polisi anayekataa kutii amri isiyo halali ambayo inaweza kupelekea ukiukwaji wa haki za binadamu?

**SANDUKU LA HABARI 5:3**

## HATI RASMI ZA KIMATAIFA

1. **Kanuni za Mienendo ya Watekelezaji wa Sheria:** Ibara ya 5 inaeleza "Hakuna mtekelezaji wa sheria atakayejitetea kwa kutumia sababu ya amri toka juu kwa kumtesa au kufanya matendo mengine ya kinyama au ya kiudhalilishaji au adhabu."

2. **Misingi Muhimu katika Matumizi ya Nguvu na Silaha kwa watekelezaji wa sheira.**

**Msingi wa 24**

*Maafisa wakuu watawajibika kama wakijua au walipaswa kujua kwamba polisi aliye chini yake ameamua au ametumia nguvu isivyo halali au silaha na mkuu huyo hakuchukua hatua yoyote katika uwezo wake kuzuia, kukataza au kutoa taarifa.*

**Msingi wa 25**

*Hapatakuwa na hatia au kuwajibishwa kinidhamu kwa polisi ambaye kwa mujibu wa Kanuni za Mienendo ya Watekelezaji wa Sheria na misingi muhimu atakataa kutii amri ya kutumia nguvu au silaha.*

**Msingi wa 26.**

Kutii amri toka kwa mkuu haitakuwa kinga katika utetezi kama polisi alijua kwamba amri ya kutumia nguvu au silaha iliyosababisha kifo au madhara makubwa kwa mtu ilikuwa si halali na alikuwa na wasaa muafaka wa kukataa kutii amri hiyo. Kwa hali yoyote ile mkuu aliyetoa amri hiyo pia anawajibika.

## SHERIA ZA NCHI

1. **Sheria ya Jeshi la Polisi (Sura ya 322 kifungu cha 27.**
   Kila afisa wa polisi atatumia uwezo na kutimiza wajibu wake kama ilivyoelekezwa kisheria au atakavyotakiwa na atatii maelekezo yote yaliyo halali kisheria katika kutimiza wajibu wake ambao mara kwa mara ataelekezwa na wakuu wake katika Jeshi la Polisi.

2. **Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

(i) Katiba inaweka taratibu, haki na vizuizi ambavyo nchi inaongozwa navyo. Katiba ni Sheria kuu ya nchi, na sheria yoyote au amri inayopingana na Katiba itakuwa ni batili.

(ii) Ibara ya 26 (l)

Kila mtu anawajibu wa kufuata na kutii Katiba hii na sheria za Jamhuri ya Muungano.

## ZOEZI LA NNE

**Matumizi ya nguvu na haki ya kuishi na Uhuru dhidi ya kupotea.**

Waoneshe washiriki yaliyomo katika sanduku habari 5.4 na uwaelekeze kujadili na kujibu maswali yafuatayo katika vikundi vya watu wawili au watatu.

1. Je! Unajua tukio lolote la upoteaji wa mtu Tanzania?
2. Jadili iwapo katiba ya nchi au sheria yoyote nchini inafaa katika hali iliyoelezewa katika habari liliyo kwenye sanduku.
3. Ni sheria gani ya jinai ingekuwa inakiukwa kama matendo kama hayo yangekuwa yanatendeka?
4. Ni hali zipi za kupotea kwa kupangwa au kwa kulazimishwa kunahusu ukiukwaji wa haki za binadamu.

**Sanduku Habari 5:4**

> Ni nini upoteaji wa kupangwa au wa kulazimishwa?
>
> Upoteaji wa kupangwa au wa kulazimishwa unatafsiriwa na **Kituo cha Haki za Binaadamu cha Umoja wa Mataifa katika taarifa yao namba 6 (1)** ambayo inahusika na somo hili kwa njia ifuatayo. Ukurasa wake wa pili:-
> .... mtu anakamatwa, anawekwa kizuizini au vinginevyo ananyimwa uhuru wake na maafisa wa matawi tofauti au ngazi mbalimbali za Serikali, au na kikundi kilichojiandaa au watu binafsi kwa niaba yao wenyewe au wakiungwa mkono ikifuatiwa na kukataa kueleza hatima ya huyo mtu au alipo huyo mhusika au kukataa kukubali kumfanya mtu huyo kuwa nje ya ulinzi wa sheria.

## REJEO

1. Utesaji haukubaliki kwa hali yoyote ile.

2. Silaha zinaweza kutumika tu katika kujihami au kutetea maisha ya wengine katika kuzuia kosa kubwa la jinai ambalo linatishia maisha ya wengine katika kumkamata mtu anayetishia maisha au anayekataa juhudi za kujaribu kusimamisha vitisho.

3. Kama ikibidi nguvu itumike, basi lazima iwe na uwiano kwa kiasi kinachohitajika kisheria na utunzaji wa usalama wa umma.

4. Kiasi cha nguvu kitakachotumika kiwe kile kinachoweza kukubalika kwa hali yoyote ile kulingana na mazingira ya tukio lenyewe.

5. Kabla ya kuamua kutumia silaha onyo/tahadhari itolewe kwa uwazi na muda maalumu uwekwe wa kutii onyo.

6. Msaada wa matibabu utolewe kwa waathirika.

7. Taarifa ya tukio lazima itolewe ikihitajika.

## REJEA

Kwa ufafanuzi zaidi unaweza kurejea:-


1. UN High Commission for Human Rights; **Human Rights and law Enforcement: A manual on human rights training for Police (professsional training series No. 5** Geneva, Switzerland 1997).

2. Das D. and Peter C. **Human Rights and Law Enforcement: Lesson Plan,** Dar Es Salaam 1999.

# SURA YA SITA

## POLISI NA USALAMA WA UMMA

### Utangulizi

Nchi nyingi duniani zimetingishwa na vita, vurugu za kijamii, vita vya kikabila, hali za hatari na matatizo mengine yanayohusiana na machafuko ya kutumia silaha. Sura hii ina madhumuni ya kutafuta, kuchangia na kukusanya mawazo na mbinu ambazo polisi wanaweza kutumia na kuwa nazo wakati wa hali kama hizo. Umuhimu wa haya upo kwenye ukweli kwamba ukiukwaji wa haki za binadamu ni jambo la kawaida katika hali kama hizi na kwa hali hiyo watu wanahitaji mifumo ya kuwalinda.

Ukiukwaji wa hali ya juu hutokea pale unapotokea uamuzi wa kutumia nguvu kupita kiasi na silaha, hata kama vitendo hivyo vinafanywa dhidi ya vyombo vya serikali au makundi ya raia.

### MATARAJIO

Mwishoni mwa sura hii washiriki wataweza kuelewa yafuatayo:

1. Maana ya ghasia za kiraia na hali ya hatari
2. Mazingira yanayoweza kusababisha kuwepo kwa hali ya hatari
3. Vipimo vya haki za binadamu vinavyohitajika wakati wa hali za ghasia za raia

## ZOEZI LA KWANZA

1. Wasilisha vifungu vya vyombo vya haki za binadamu vilivyo kwenye sanduku habari kwa washiriki. Vipo vigezo / tabia zinazohusiana na migogoro ya silaha na ghasia za raia. Katika kipindi hiki mkufunzi awatake washiriki kutaja vigezo vya migogoro ya silaha upande mmoja na vya ghasia za raia upande mwingine.
2. Mkufunzi anaweza kumtaka kila mshiriki kufafanua au kuelezea kila kigezo alichotoa. Wanaweza kutoa mfano kutokana na uzoefu wao na kufafanua kila kigezo.
3. Mkufunzi ahakikishe kwamba washiriki wanaelewa na wanaweza kutofautisha migogoro ya silaha na ghasia za raia.

**SANDUKU HABARI 6:1**

Machafuko ya silaha

- **Mkataba wa Geneva (1940)** hautafsiri maana ya ìmigogoro ya silahaî Yafuatayo hata hivyo ni viashirio:
  (i) Ni tangazo la vita kati ya nchi mbili (hata kama nchi moja haitambui hali hiyo ya vita)
  (ii) Hali nyingine yoyote kati ya nchi au ndani ya nchi ambayo itafanya nguvu itumike (hata kusababisha ulinzi kama unavyoeleweka katika mkataba)

*Hali ya migogoro ya silaha inasemekana ipo pale ambapo kuna matumizi ya nguvu ama ya nchi moja dhidi ya nyingine au ndani ya nchi na waasi, magaidi au kwenye hali ambayo kundi linadai haki ya kujitawala (kwa mujibu wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa au katiba ya nchi)*

- **Nyongeza ya II ya Mkataba wa Geneva** ambayo hasa inashughulika na migogoro ya ndani ya silaha haitoi tafsiri ya maana ya migogoro, ila inatafsiri mazingira ambayo vifungu vyake vinaweza kutumika.

  *(i) Migogoro ya silaha kati ya majeshi ya serikali na majeshi ya waasi*
  *(ii) Makundi yaliyojiunda yenye silaha ambayo yana mwamrishaji anayewajibika na wanatumia uwezo huo dhidi ya sehemu fulani ya nchi ili waweze kufanya mpango wao wa kijeshi.*

**Angalizo:**
Ingawa nyongeza ya II haijumuishi matumizi yake katika hali za machafuko ya ndani na hali ya wasiwasi ni vigumu kutofautisha kati ya wakati wa hali ya wasiwasi na mapigano hasa. Kiwango cha kutokuwa na uhakika na hali ya wasiwasi kabla ya mapigano kuanza au mashambulizi yanakaribiana kabisa kama sehemu ya migogoro kamili.

**GHASIA ZA RAIA**
Aina za vurugu zilizoainishwa na Ibara I aya ya 2 ya Nyongeza namba II ni:
*Hali ya machafuko au hali ya wasiwasi wa ndani ya nchi, kama kufanya fujo, matendo ya vurugu ambayo ni moja moja au yanatokea kwa ghafla mara moja, na matendo mengine ya aina hiyo ambayo si migogoro ya silaha. Kamati ya kimataifa ya msalaba mwekundu imependekeza tafsiri ya vigezo vya ghasia za raia (machafuko ya ndani na hali ya wasiwasi)*

"Hali ambayo hakuna migogoro ya silaha hasa, lakini kuna mapambano ndani ya nchi yenye sura ya hali fulani ya kutisha au ya muda mrefu au inayohusisha vitendo vya vurugu. Hizi baadaye zinapata sura mpya kutoka matendo ya mitafaruku kuingia katika mapambano kati ya makundi yaliyojipanga vizuri au kidogo na wasio madarakani. Katika hali kama hii ambayo si lazima izae migongano ya wazi, mamlaka iliyopo huita nguvu za jeshi la Polisi wenye silaha na kurudisha hali ya utulivu na idadi kubwa ya waathirika imefanya ulazima kutumia masharti ya kibinadamu. (Angalia International review of the Red Cross (Geneva) 28th year No. 262 (January - February 1998) p. 12.

## KISA MKASA

Mkufunzi awaelekeze washiriki kwa kuwasaidia kupata kisa mkasa hapa chini na baadaye awaelekeze kwenye maswali yafuatayo:

A. Wanawake wana shirika lao linaloitwa WRPA yaani Umoja wa Kulinda Haki za Wanawake. Hili ni kundi ambalo uanachama wake ni kwa wanawake tu. Madhumuni yake makuu ni kusimamia haki za wanawake nchini. Shirika hilo linataka kuandaa maadamano kupinga ubaguzi wa kijinsia na wanataka waandamane hadi kwa Waziri Mkuu wakiwa na mabango yenye ujumbe huu:

1. **Wanawake waruhusiwe kufanya kazi nje ya nyumbani kwao. Wao si walinzi wa nyumba**
2. **Wakiwa nje, wanawake wasilazimishwe kufunika sehemu zote za miili yao, mitandio iondolewe nyusoni mwao.**
3. **Wanawake sio vyombo vya biashara. Wanaume wasiruhusiwe kuoa wanawake wengi kadri wapendavyo, Mke mmoja, mume mmoja.**
4. **Wanawake ni wajanja kama wanaume. Wasikubali kila kitu wanachoambiwa na wanaume.**

Yamekuwepo mawasiliano kati ya Polisi na waandaaji wa maandamano. Kibali cha kufanya maandamano kimeshapatikana na imefahamika kuwa kutakuwa na washiriki wapatao 20,000 wakiwemo wanaume wanaounga mkono. Nia yao ni kufanya maandamano ya amani yasiyo na vurugu.

Njia ambayo maandamano yatapitia imeshakubalika. Itawapasa washiriki kupitia katikati ya jiji hadi kwenye ofisi ya Waziri Mkuu ambapo watawasilisha madai yao. Maandamano hayo yatasindikizwa na polisi wenye bunduki. Wamekubaliana pia kwamba shughuli ya polisi itakuwa ya staha na hawatajitokeza sana.

Masaa mawili kabla mandamano kuanza, viongozi wa polisi wanapata habari za kutia wasiwasi sana kutoka kwa wapelelezi wao kwamba, kuna baadhi ya makundi ya kidini yenye msimamo mkali wanaopinga maandamano hayo na wanatarajia kukabiliana na waandamanaji watakapokuwa wanakaribia ofisi za Waziri Mkuu ili kuwazuia. Wamepania kufanya vurugu za uhakika ili kuharibu nia ya maandamano hayo. Hao wapinzani hawataki mjadala na polisi wanadai kuwa hao wanawake wanaotaka kuandamana wanadhalilisha kitabu chao kitakatifu.

Imeamuliwa kuwa kama suala la kisera maandamano lazima yakubaliwe kuendelea na haki ya waandamanaji ya kuwa na mkusanyiko wa amani ilindwe. Wakati waandamanaji wanakaribia katikati ya jiji, wanakabiliana na hilo kundi la wenye msimamo mkali wa kidini. Wenye msimamo mkali wameziba njia kwa mawe. Polisi wako tayari kuwakabili hao wenye msimamo mkali.

## KAZI YA KUJADILI

Waelekeze washiriki wakae katika makundi madogo na wajadili maswali yafuatayo:

1. Je tukio katika kisa hiki ni mgogoro wa silaha au ghasia za raia?
2. Ukiangalia hali halisi ya tukio unadhani polisi walikuwa na sababu ya kuruhusu maandamano kuendelea?
3. Elezea mbinu za kiutekelezaji na kipolisi ambazo ungeweza kutumia katika hali hiyo na jinsi ambavyo mbinu hizo zingeweza kutimiza madhumuni ya kazi ya polisi
4. Tayarisha muhtasari wa mhadhara ambao ungewapa polisi kuhusu kutumia nguvu katika kukamata na misingi ya ujumla ya Haki za Binadamu.

Baada ya mrejesho washiriki wasaidiwe kupitia vipimo vya haki za binadamu kwenye sanduku hapa chini.

### SANDUKU HABARI 6:2

### MIGOGORO YA SILAHA

**Hati rasmi za Kimataifa:**

**(a) Ulinzi kwa walioumia, wagonjwa na walioharibikiwa na mali:**

*Ibara ya 10 ya Nyongeza ya I katika Mkataba wa Geneva unaelekeza watu wote walioumia, wagonjwa na walioharibikiwa na mali wa upande wowote waheshimiwe na walindwe.*

**(b) Ulinzi kwa mateka wa vita:**

*Ibara ya 12 ya Mkataba wa Tatu wa Geneva unaelezea kuwa mamlaka inayoteka ina wajibu wa kuangalia watakavyohudumiwa mateka wa vita. Kwa vile ibara za mkataba huu zinagusia masuala ya kutoroka na kukamatwa kwa mateka wa vita, kwa makosa ya jinai wanayofanya au kufanyiwa wakati wa taratibu za kisheria, itawezekana kuwa majeshi ya polisi wa nchi iliyoteka kuhusishwa. Ibara ya 14 ya Mkataba wa Tatu wa Geneva pia inaelezea kuwa mateka wa vita wanastahili heshima katika mazingira yoyote yale.*

**(c) Ulinzi kwa raia.**

*Ibara ya 51 aya ya 2 ya Nyongeza ya 1 inaelezea kuwa raia kwa ujumla na raia mmoja mmoja wasifanyiwe mashambulizi. Zaidi ya hapo, matendo au vitisho vya vurugu yenye nia ya kusambaza hofu kwa raia yanakatazwa.*

**Sehemu ya (iv) kifungu cha I Sura (vi) ya Nyongeza ya I kinahusiana na kujihami kwa raia.** *Hii imetafsiriwa katika Ibara ya 61 kama utendaji wa matendo ya kiutu yanayokusudiwa kulinda umma wa raia dhidi ya hatari na kuwasaidia kutokana na athari za papo kwa papo za ukatili.*

*Wakati wa vita, polisi watategemewa kufanya baadhi ya kazi hizi kama kutoa tahadhari, kuhamisha watu, kutambua sehemu za kuokoa na kuweka alama sehemu zenye hatari, kudhibiti na kusimamia utulivu katika maeneo yaliyo athirika.*

**(d) Polisi chini ya mamlaka ya walioteka nchi:**

*Ibara 43 ya Miongozo iliyoambatanishwa kwenye Mkataba wa Hague wa 1907 unahitaji nchi iliyoteka kurejesha na kuhakikisha utulivu wa umma na usalama katika nchi iliyoiteka.*

## VURUGU ZA KIRAIA

Sheria za kimataifa za Haki za binadamu zinatumika kisheria

- Uangalifu maalum lazima utumike inapobidi polisi kutumia nguvu wakati wa vurugu za kiraia. Kutumia nguvu iwe ni pale inapobidi na iwiane na hali halisi iliyopo.
- Kwa hali hii misingi iliyotolewa kwenye Misingi Muhimu ya Jinsi ya Kutumia Nguvu na Silaha kwa Watekelezaji wa Sheria lazima itiliwe mkazo.
- Kifungu cha 12. Kwa vile kila mtu anaruhusiwa kushiriki katika mikusanyiko iliyokubalika kisheria na ya amani kwa mujibu wa misingi iliyowekwa kwenye Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu, Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na kisiasa, hivyo basi serikali, vyombo vya utekelezaji wa sheria lazima watambue kwamba matumizi ya nguvu na silaha hayana budi yatumike kulingana na misingi namba 13 na 14.

- Kifungu cha 13. Katika kutawanya mkusanyiko usio wa kihalali lakini usio na vurugu inabidi watekelezaji wa sheria waepuke kutumia nguvu au kama hii haiendani na hali hiyo, watumie nguvu kwa kiasi kidogo sana kitakachohitajika.
- Kifungu cha 14. Katika kutawanya mikusanyiko yenye vurugu, watekelezaji wa sheria wanaweza kutumia silaha pale ambapo matumizi ya vyombo vingine visivyo hatari hayafai na watumie silaha kwa kiasi kidogo iwezekanavyo. Watekelezaji wa sheria wasitumie silaha bali katika hali zilizoainishwa katika msingi wa 9.

## ZOEZI LA PILI

Matumizi mabaya ya silaha wakati wa hali ya hatari na amri ya kutotembea ovyo. Mchague mshiriki mmoja asome kwa sauti kisa mkasa kifuatacho.

## KISA MKASA

Hebu fikiri askari mmoja mlevi anayejiita Kapteni Simba anaitingisha nchi kwa tangazo kupitia redio ya Taifa kwamba amefanya mapinduzi ya kijeshi. Anailaumu serikali kwa rushwa. Kapteni Simba akiwa amefuatana na Kapteni Mbogo na wengine wanasikika redioni kwa dakika kadhaa. Tukio hili linaandamana na milio kadhaa vya risasi lakini hamna mapigano. Kapteni Simba anaonesha kwamba ikulu imezingirwa na askari ambao wanamuunga mkono. Muda mchache baadaye maaskari waaminifu kwa serikali wanarejesha mambo katika hali ya kawaida na papo hapo wanamtia nguvuni Kapteni Simba na wenzake. Dakika thelathini baada ya Kapteni Simba kukamatwa, Rais wa nchi analihutubia taifa na kueleza kwamba juhudi za Kapteni Simba za kuiangusha serikali zimeshindwa na serikali ipo imara. Rais anatamka hali ya hatari na kutotembea ovyo. Anaamuru polisi kumkamata na kumweka kizuizini mtu yeyote atakayekutwa mitaani baada ya saa moja usiku.




Juma moja kabla, mashirika kadhaa yasiyo ya kiserikali yaliandaa maadhimisho ya siku ya Haki za Binadamu kwa maandamano ya amani kuzunguka mji. Viongozi kadhaa wa mashirika ya kiraia walipangiwa kutoa hotuba kwenye suala la haki za binadamu na walishapata kibali cha polisi cha maandamano. Hata hivyo siku ya maandamano, polisi wakakifuta kibali kwa njia ya kushangaza na kuwaamuru wote waliokusanyika kutawanyika. Polisi waliwaambia waandalizi wa maandamano kuwa haitawezekana kuandamana kwa vile nchi iko chini ya hali ya hatari. Vyanzo vya habari huko polisi pia viliwaambia waandalizi kuwa inahofiwa kuwa maandamano ya Haki za Binadamu yanaweza kugeuzwa kuwa maandamano ya kisiasa. Serikali haitaki hasa wanachama wa vyama vya upinzani washiriki




SANDUKU HABARI 6:3

**Misingi inayosimamia hali ya hatari**
**Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (Ibara ya 4)**

- *Hali ya hatari inaweza kutangazwa tu kwa mujibu wa sheria.*
- *Hali ya hatari inaweza kutangazwa pale tu panapoonekana kuna tishio la maisha kwa taifa na njia nyingine za kawaida zinaonekana kutofaa kushughulikia hali hiyo.*
- *Hali ya hatari lazima itangazwe rasmi kabla hatua tofauti hazijachukuliwa.*
- *Hatua zozote zisizo za kawaida zitahitajika hasa katika kuikabili hali halisi*
- *Hatua zozote zisizo za kawaida zisitumike kibaguzi kwa misingi ya asili, rangi, jinsia, lugha, dini au kabila.*

- *Hatua nyinginezo hazitaruhusiwa kuhusiana na haki ya kuishi, kuzuia mateso au matendo mengine ya kikatili na ya kiudhalilishaji, kuzuia utumwa, kuzuia kifungo kwa mtu aliyeshindwa kutimiza masharti ya mkataba. Kuzuia sheria zilizoishapitwa na wakati, kumtambua kila mtu kuwa sawa mbele ya sheria au haki ya uhuru wa kufikiri, dhamira, kujumuika na dini.*

**Mkataba wa Kiafrika kuhusu Haki za watu na Haki za Binadamu**

- *Mkataba wa Kiafrika wa Haki za Binadamu na Haki za watu hauruhusu kuweka pembeni haki zilizoainishwa ndani ya huo mkataba hata kama ni wakati wa hali ya hatari. Tume ya Kiafrika ya Haki za Binadamu inaeleza:*

*Mkataba wa Kiafrika tofauti na mikataba mingine ya haki za Binadamu hauruhusu nchi iliyo mwanachama kutoa sababu za kutotimiza wajibu wake kwa kuweka pembeni sehemu ya haki wakati wa hali ya hatari.*

**SERIKALI ZA NCHI**

**Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Ibara ya 32)**

- Raisi anaweza kutangaza hali ya hatari katika Jamhuri ya Muungano au sehemu yake yoyote katika hali zifuatazo:

(a) Jamhuri ya Muungano iko katika vita au

(b) Kuna hatari hasa kwamba Jamhuri ya Muungano inakaribia kuvamiwa na kuingia katika hali ya vita.

(c) Kuna hali halisi ya kuvurugika kwa amani ya jamii au kutoweka kwa usalama wa jamii katika Jamhuri ya Muungano

(d) Kuna hatari dhahiri na kubwa kiasi kwamba amani ya jamii itavurugika na usalama wa raia kutoweka.

(e) Kunaelekea kutokea tukio la hatari au tukio la balaa au la baa la kimazingira.

## KAZI YA PAMOJA

Wagawe washiriki katika makundi. Wape kazi ifuatayo:

1. Hali ya Hatari ni nini? Je unaweza kutoa uzoefu wako wa hali ya hatari iliyoshawahi kutokea Tanzania au nchi nyingine? Watekelezaji wa sheria waliikabili vipi hali hii?
2. Kwa kuzingatia maelezo katika kisa mkasa, je kutangazwa kwa hali ya hatari kulikuwa na ulazima? Ni haki gani za muhimu za binadamu zisizostahili kuwekwa pembeni zilizokiukwa na polisi wakati wa hali ya hatari? Kwa nini haki hizi zilikiukwa ?

3. Ni kwa njia gani polisi wangeweza kuwasaidia watu kutumia haki yao ya uhuru wa kwenda watakako na kukusanyika kwa amani katika hali iliyoelezewa katika kisa mkasa?
4. Kuna sheria ya Tanzania inayohusu hali ya Hatari? Kama ndio unaifahamu kiasi gani? Kama sio ungependa iwepo? Elezea inavyofaa iwe.

## REJEO

1. Nchi au mamlaka iliyovamia nchi nyingine inapaswa kuhakikisha utulivu na usalama wa umma wa nchi iliyoiingilia.
2. Hali ya Hatari inaweza kutangazwa tu kwa mujibu wa sheria na pale ambapo kuna hatari inayotishia maisha ya taifa na pale ambapo njia za kawaida zimeshindwa kuikabili hali hiyo.
3. Hatua za tofauti zitakazochukuliwa wakati wa hali ya hatari hazipaswi kuwa za kibaguzi kwa misingi ya rangi, asili, jinsia, dini au anakotoka mtu.
4. Hali ya hatari isiwe kigezo cha kukiuka haki zifuatazo, haki ya kuishi, uhuru dhidi ya mateso na ukatili, unyama au matendo mengine ya udhalilishaji na adhabu, kuzuia utumwa, uhuru wa haki mbele ya sheria, uhuru wa mawazo, dhamira na dini.

## REJEA

Kwa ufafanuzi zaidi unaweza kurejea:

1. UN High Commission for Human Rights and Law Enforcement: **A Manual on Human Rights training for Police (proffessional training series No. 5)** Geneva Switzerland 1997.
2. Das D. na Peter C. **Human Rights and Law Enforcement: Lesson Plan,** Dar es Salaam 1999.

# SURA YA SABA

# UPOLISI NA HAKI ZA MAKUNDI MAALUM NA WAATHIRIKA WA UKIUKWAJI WA HAKI ZA BINADAMU

## Utangulizi

Wanawake na watoto wanaangukia katika kundi la watu maalum. Sababu maalum za kuwaweka katika kundi hili ni uwezo wao mdogo wa kuweza kudai haki zao za msingi na uhuru. Wakati watoto wanazuiwa na umri katika kuhakikisha wanapata haki na uhuru wao hivyo kuwabidi kupitia kwa watu wazima, uwezo wa wanawake unazuiwa na taasisi na mazoea ya kijamii na kiufahamu. Bado wanawake na watoto ni binadamu wanaostahili heshima ya utu wao kama binadamu. Hakuna sababu yoyote ya kuwabagua.

Hata hivyo mifumo ya kijamii, kisheria na kiutamaduni inapaswa kuwa na ulinzi maalum wa makundi haya. Hatua maalum zichukuliwe kuhakikisha kutendewa sawa kwa wanawake katika ushiriki wao kwenye siasa, ajira, umiliki wa mali, mirathi ndoa n.k. Vile vile jitihada maalum zielekezwe kwa watoto kuhakikisha wanafaidi haki zao za binadamu.

Waathirika wa makosa ya jinai nao ni kundi jingine la watu litakalogusiwa katika sura hii. Angalizo ni kwamba kundi hili la watu kwa kiasi kikubwa limekuwa linakatishwa tamaa na polisi Tanzania. Wakiwa katika hali ya masikitiko, kuchanganyikiwa wanahitaji huruma kutoka kwa watekelezaji wa sheria. Kinachoelezewa hapa ni kuwa kama polisi haitatoa msaada unaohitajika kwa waathirika wa makosa ya jinai wananchi wanaweza wakahusisha na matendo ya rushwa kwa watekelezaji wa sheria na hivyo kutotoa ushirikiano unaohitajika.

## MATARAJIO

Mwishoni mwa sura hii washiriki wataweza kuyaona bayana yafuatayo:

1. Ulinzi maalum utolewe kwa wanawake na watoto katika utekelezaji wa haki na usawa wa sheria zinazohusu jinai.
2. Hatua maalum zinazotumika kuwasaidia makundi maalum katika jamii sio ubaguzi.
3. Chombo cha Polisi kina wajibu usio na mipaka wa kuwasaidia waathirika wa makosa ya jinai.
4. Kuingilia kati kwa polisi katika hali za uhalifu sio tu kunatoa suluhisho bali pia kunazuia.

## ZOEZI LA KWANZA

**Polisi na ulinzi wa watoto**

- Mkufunzi awaongoze washiriki kujadili habari iliyoko kwenye sanduku habari 7.1. Awapatie maswali hapa na pale kuhakikisha wanaelewa vizuri habari hiyo.

- Watake washiriki katika kundi wasome kadi na waigize yaliyomo kama wapendavyo. Wakimaliza kuigiza, jadili na kila kundi namna ambavyo wangemalizia hilo igizo na walivyo ona ingefaa washiriki kufanya katika hali halisi. Rudia kwa kila kundi. Jaribu kupata washiriki tofauti kuigiza kila onesho.

## KADI I

Beno: **Ehe Poro! Mambo vipi!**

Poro: **Rafiki yangu, mambo magumu. Hivi nimetoka kwa mama Ruta nakwambia siamini, maana mama wa watu analia ajabu. Mtoto wake pekee mvulana wa miaka 15 yuko rumande kwa siku kumi sasa kwenye kituo cha Polisi Kirugu.**

Beno: **Maskini mtoto, maskini mama wa watu kwani tatizo nini? Huyo mtoto alifanya nini?**

Poro: **Hujui kilichotokea? Lakini si jirani yako? Inasemekana huyo mtoto aliiba shilingi mia nyumbani kwa mkuu wa kituo cha polisi. Polisi wamemnyima dhamana. Na unajua nini: nadhani polisi wanamwogopa mkuu wao.**

Beno: **Hii inanikumbusha kesi nyingine iliyotokea miezi miwili iliyopita. Mvulana wa miaka 16 ambaye ametoka kwenye familia maskini pale kijijini kwetu aliiba kuku wa mwenyekiti wa kijiji. Alipopelekwa kituo cha polisi Kirugu, polisi walimvamia na kumpiga vilivyo wakidai kuwa wanafanya hivyo kumsaidia kwa sababu sasa hivi nchi yetu imekumbwa na tabia mbaya sana za vijana. Hebu mfikirie huyo mtoto mdogo mwizi!**

Poro: **Lakini kulikuwa na uhalali wowote wa kumfanyia hivyo?**

Beno: Sidhani. Nadhani kuwashughulikia watoto wahalifu kusitegemee tu ukubwa wa kosa bali hata mazingira yaliyopelekea kufanya kosa.

Poro: Kwa kweli mambo mengine ya polisi hayafai

## KADI 2:

Mugi: Mama Kulwa kuna tatizo gani? Unaonekana una huzuni

Mama Kulwa: Unamjua Kulwa, mtoto wangu yule wa kiume wa miaka 13. Walikamatwa na polisi yeye na wenzie wanaocheza nae. Anadaiwa kuwa alishuhudia ugomvi uliosababisha kifo huko kijiweni.

Mugi: Sasa wewe umefanyaje?

Mama Kulwa: Nilienda Polisi Kati nikakuta amefungwa rumande na watu wazima. Wamemkatalia dhamana. Ati anaisaidia Polisi.

Mugi: Nadhani wako sawa. Hilo shtaka ni la mauaji. Ni muhimu kumlinda huyo mtoto na kumweka mbali na hasira za ndugu wa marehemu. Polisi pia wanaogopa kuwa wakimwachia inaweza kuathiri upatikanaji wa haki.

Mama Kulwa: Lakini si haki. Mwanangu nakwambia ni shahidi tu. Najua mwanangu hahusiki.

Mugi: Mh! Hilo ni tatizo. Ni vigumu kumwachia mwanao kwa sababu nilizoishakwambia. Hata hivyo huyo mtoto angewekwa tofauti na hao wafungwa watu wazima, au apelekwe mahali pengine. Hii ni haki yake ya msingi unaelewa.

## KADI YA 3

Konstebo wa Polisi: Ndio mzee, nikusaidie?

Mzee: Nimekuwa nikimtafuta mwanangu, mvulana wa miaka 15, anyeaitwa Ibra. Leo siku ya kumi sijamtia machoni. Nimeambiwa amekamatwa na polisi na wamemweka rumande. Ndio nimekuja kumtambua na kumwekea dhamana. Hiki hapa

kitambulisho changu na barua toka kwa mjumbe.

| | |
|---|---|
| Polisi: | Lakini hizi barua zinaonesha wewe si baba mzazi wa huyu mtoto. Wewe utamuwekeaje dhamana na si baba mzazi wala mlezi wake? |
| Mzee: | Mimi bwana ni jirani yao na ananihusu. Wazazi wao wote wako safari waliniachia maagizo niwaangalizie watoto. Ni wajibu wangu. Yaani mpaka baba yake mzazi awepo ndio umpe dhamana? |
| Polisi: | Oh mzee ni baba yake tu aliyetakiwa aje. |
| Mzee: | Lakini mi.............. |
| Polisi: | Nasikitika mzee bila baba yake kuja hapa siwezi kukusaidia. Haya yako kwenye uwezo wangu na ni uamuzi wangu pia. |

## KADI YA 4:

| | |
|---|---|
| Tukutu: | Polisi wanakiuka haki zetu. Hebu tufanye mgomo wa kula. Hebu tuoneshe kuwa tuko sawa mbele ya sheria. |
| Tundu: | Kwa nini unasema polisi wanatunyima Haki? Ninajua hawatuambii kosa letu na tukiwauliza wanatupiga wakati hatuna kosa, lakini nafikiri .............. |
| Tukutu: | Hilo ndio neno! Haki yetu je ya kuongea na mwanasheria? Haki ya kukaa kimya, haki ya kuwa na mzazi au mlezi na haki ya kuuliza maswali kwa mashahidi, ah! Na haki ya kukata rufaa. |
| Tundu: | Nadhani tugome. Tususie kula. Tuache kula kabisa mpaka watutendee haki. |

## SANDUKU HABARI 7:1

### HATI RASMI ZA KIMATAIFA

1. **Mkataba wa Haki za Mtoto**

   **Ibara ya 2: inaeleza kwamba,** *nchi wanachama zitachukua hatua zote zinazofaa kuhakikisha kwamba mtoto analindwa dhidi ya aina zote za ubaguzi na adhabu zinazotolewa kwa sababu ya hadhi yake, matendo, mawazo yaliyotolewa au imani ya wazazi wa mtoto au walezi wake kisheria au jamaa yake.*

   **Ibara ya 5 inasema kwamba:** *kwa matendo yote yatakayomhusu mtoto, ama yakiwa yanachukuliwa na taasisi za umma au za kibinafsi za ustawi wa jamii, mahakama, mamlaka za kiutawala au vyombo vya sheria maslahi makuu ya mtoto yanapaswa kuwa ndio msingi wa kutiliwa maanani.*

**Ibara ya 37:** ina aya 4

*(a) Mtoto awe huru dhidi ya mateso, au aina nyingine ya ukatili, unyama, au matendo ya kiudhalilishaji au adhabu na adhabu ya kifo au kifungo cha maisha.*

*(b) Mtoto awe huru dhidi ya kukamatwa kinyume cha sheria au kiholela.*

*(c) Watoto wanapaswa kutendewa kiutu na kwa heshima ya hadhi yao ya asili ya utu na kwa kutilia maanani mahitaji yao maalum, wakiwa rumande watengwe na watu wazima na wawezeshwe kuwasiliana na jamaa zao.*

*(d) Pale ambapo mtoto atanyimwa uhuru wake itabidi apate mara moja haki ya kupata msaada wa kisheria na haki ya kupinga uhalali wa yeye kuwepo ndani.*

2. **Vipimo vya Msingi vya Masharti ya Uendeshaji wa Haki kwa Watoto. (Masharti ya Beijing)**

   (i) *Sharti la 5: Mfumo wa haki na usawa kwa watoto lazima usisitize hali nzuri ya watoto na ihakikishe kuwa kuwashughulikia watoto wahalifu kunawiana na mazingira ya mhalifu na kosa lenyewe.*

   *(ii) Sharti la (7) Linafafanua taratibu za kimsingi za kulinda kama vile kutohesabiwa kuwa na hatia hadi ithibitike, haki ya kuelezwa mashtaka dhidi yake, haki ya kukaa kimya (kutojibu), haki ya kuwakilishwa na haki ya kuwepo wazazi au walezi.*

   *(iii) Sharti la 10:1 na 10:2 Yanaeleza kwamba wakati wa kumkamata mtoto wazazi au walezi wake wataarifiwe mara moja kuhusu kukamatwa huko na mahakama au chombo kingine kinachohusika kifikirie kumwachia mara moja*

   *(iv) Sharti la 10:13 linahitaji mikataba kati ya watekelezaji na watoto wahalifu iangaliwe katika hali ambayo itaheshimu hadhi ya kisheria ya*

*mtoto na kuzuia madhara kwa mtoto kulingana na mazingira ya kesi.*

(v) *Sharti la 11:1 Kila inapobidi wakati wa kumshughulikia mtoto mhalifu iangaliwe uwezekano wa kutompeleka mtoto mahakamani kufanyiwa kesi za kawaida.*

(vi) *Sharti la I linahitaji maafisa polisi wanaoshughulika mara kwa mara na masuala ya watoto au wanaohusika na kuzuia uhalifu wa watoto wawe na maelekezo ya kutosha na wapatiwe mafunzo maalum.*

(vii) *Sharti 13: Linahitaji kuwekwa ndani kabla ya mashtaka kutumike kama njia ya mwisho kabisa na kwa muda mfupi iwezekanavyo. Wakiwa rumande watoto wawekwe tofauti na watu wazima na wapatiwe huduma, ulinzi na msaada unaohitajika kulingana na umri na hadhi yao. (Angalizo: Pia soma sharti la 18 la masharti ya Umoja wa Mataifa ya Kulinda Watoto Walionyimwa uhuru).*

3. **Mkataba wa Nchi Huru za Kiafrika wa Haki na Maslahi ya Mtoto: Ibara ya 17 (1) inasema:**
*Kila mtoto atakayeshutumiwa au kupatikana na kosa la jinai atakua na haki ya kupata uangalizi maalum kulingana na hadhi ya mtoto ya utu na stahili yake.*

4. *Nchi wanachama ....... watahakikisha kwamba hakuna mtoto ambaye amefungwa au amenyimwa uhuru wake atakayeachiwa kupata mateso au kutendewa kinyama au kudhalilishwa au kupewa adhabu na kwamba watoto watenganishwe na watu wazima na pia mtoto yeyote atakaye shutumiwa kwa kosa la jinai ahesabike hana hatia hadi itakapothibitika kisheria, aelezwe mara moja mashtaka yake, apatiwe msaada wa kisheria na msaada mwingine wowote.*

## SHERIA ZA NCHI

1. **Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kifungu cha 56.**
*Polisi atakayekuwa anahusika na upelelezi wa kosa ambalo mtoto amewekwa ndani atatakiwa mara moja baada ya mtoto huyo kuwekwa ndani, kuwaarifu wazazi au walezi wa mtoto kwamba mtoto yuko ndani na kosa ambalo limefanya awekwe ndani.*

*Kifungu cha 64 (2) kinasema kwamba pale ambapo mtoto yuko chini ya miaka 15, mtoto huyo anaweza kuachiwa mara wazazi, walezi au jamaa zake au mtu yeyote anayeaminika atakapofika kujitambulisha kwa niaba yake, awe na dhamana au la. (vile vile soma kifungu cha 4 cha sheria ya watoto na vijana wadogo sura ya 13 ya sheria za nchi)*

2. **Sheria ya watoto na vijana wadogo sura ya 13 ya sheria za nchi**

*Kifungu cha 22 (3) kinaelezea kwamba watoto wadogo wawekwe tofauti na watu wazima wanapokuwa ndani:*

*(i)* *Polisi au afisa utawala anaweza kufanya maombi kwenye mahakama ya watoto kuomba amri ya mtoto kuwa chini ya ulinzi wa jamaa zake.*

*(ii)* *Pia soma kifungu cha Sheria za Magereza Namba 34 ya 1967*

3. **Masharti ya jumla ya Polisi (PGO)**

<u>Sharti la 17</u>

*Mtoto hatakiwi kuandamana na mtu mzima aliyeshtakiwa au aliyepatikana na hatia labda tu kama wameshtakiwa pamoja kwa kosa moja au kutiwa hatiani pamoja.*

# POLISI NA HAKI ZA WANAWAKE




## ZOEZI LA PILI

### Upolisi na Misingi ya Kutobagua

Waeleweshe washiriki wakae katika makundi matatu. Wagawie kazi kwa kila kundi. Washiriki wajadili na kujaribu kuainisha misingi ya Haki za binadamu zilizokiukwa katika kila kadi.

### KADI NA. I

**Mimi ni Dorothy. Nina miaka 14. Sikutaka kufanyiwa mila ya kukeketwa (tohara kwa wasichana). Shangazi yangu akawaambia wanawake wengine kijijini kwetu wanikamate na kunifanyia tendo hilo. Kidonda bado hakijapona. Daktari kaniambia nimepata ugonjwa wa pepopunda. Nimeshtaki polisi. Polisi wameniambia wao hawawezi kuingilia mambo ya mila.**

**KADI NA 2**

**Mimi ni Mary: Nimeolewa na Mwakyoma. Jana mume wangu aliporudi kazini, aliniambia kasikia kuwa nimetembea na jirani yetu kimapenzi na akaanza kunipiga na matokeo yake mimba yangu ikatoka. Nilienda Polisi leo asubuhi wakaniambia bora niwaeleze wazazi wa mume wangu.**

**KADI NA. 3**

**Mimi Ana. Nina miaka kumi na tano na ninaishi katika mitaa mjini Dar es Salaam. Wazazi wangu walifariki miaka kadhaa iliyopita na sina mtu wa kunitunza. Jana nilipewa shilingi elfu tano (5,000l) na mfanya biashara wa kihindi nilipomwomba. Wavulana wa mitaani wakaiona na kuninyang'anya muda mfupi baadaye. Nilitoa taarifa polisi lakini yule polisi pale kituoni alinitaka kimapenzi kwanza kabla hajaanza kwenda kuwatafuta hao wavulana. Niliogopa na sikuthubutu kukubaliana na polisi hivyo akanifukuza.**

Wasaidie washiriki kujadili misingi iliyokuwa kwenye sanduku hapa chini.

**SANDUKU HABARI 7:2**

**Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu Ibara ya 2**

*Kila mtu anastahili kupata haki na uhuru ulioelezwa katika tamko hili bila kujali tofauti za kiasili, rangi, jinsia, lugha, dini, siasa au maoni mengine, utaifa, au asili ya kijamii, mahali pa kuzaliwa au hali nyingine yoyote.*

**Tafsiri ya ubaguzi dhidi ya wanawake**

*Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake - Ibara ya I*

*Kwa minajili ya mkataba huu neno "Ubaguzi dhidi ya wanawake" litamaanisha* ***tofauti, kutengwa au katazo litakalofanywa*** *kwa misingi ya jinsia likiwa na athari au madhumuni ya kuathiri wanawake wasifaidike na utambuzi, manufaa au matumizi ya usawa, uhuru na haki za kimsingi za binadamu katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kiraia, bila kujali kama wameolewa au hawajaolewa.*

**Tamko la kimataifa la Haki za Binadamu Ibara ya 7**

*Watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanapaswa kulindwa na sheria bila ubaguzi. Wote wanapaswa kulindwa sawa dhidi ya ubaguzi ambao utapingana na tamko hili au uchochezi utakaopelekea kuleta ubaguzi wa aina hiyo.*

**Angalizo:**
*Misingi ya haki ya usawa mbele ya sheria na ulinzi sawa mbele ya sheria imewekwa pia katika mkataba wa Kiafirika Kuhusu Haki za Watu na Haki za Binadamu na mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa.*

**Kanuni za Mienendo ya Watekelezaji wa Sheria ibara ya I**
*Watekelezaji wa sheria mara zote wanatakiwa kutumia wajibu wao kwa mujibu wa sheria kwa kuhudumia jamii na kuwalinda watu wote dhidi ya matendo yaliyo kinyume cha sheria sambamba na wajibu mkubwa unaotakiwa kitaalam.*

## ZOEZI LA TATU

### Wajibu wa polisi dhidi ya ukatili majumbani

Mkufunzi aanze kwa kuwauliza washiriki wanavyoelewa ukatili majumbani. Anaweza kuuliza mmoja mmoja au baadhi yao. Vinginevyo anaweza kuwagawia kadi kila mmoja wao na kumtaka kila mshiriki kuandika tafsiri ya ukatili majumbani katika kadi. Mwishoni kadi zikusanywe na kubandikwa ukutani. Kila tafsiri isomwe na mkufunzi asawazishe tafsiri hizo na tafsiri ifuatayo:

*Ukatili majumbani hasa unamaanisha kuumizwa kimwili au kiakili kwa mwanamke na mwenzi mume. Matukio ya ukatili majumbani yanaanzia kwenye maumivu kidogo hadi kifo (mauaji)*

Mkufunzi awaeleze washiriki kwamba ukatili majumbani ni jambo linalofanyika Tanzania. Na takwimu zifuatazo zioneshwe kwa washiriki

| Ukatili | Taarifa za kesi |
|---|---|
| Muda | 1990 -1995 |
| Mauaji | 70 |
| Kipigo | 1922 |

**Imetolewa kwenye:**

1. Domestic violence survey na TAMWA 1990 - 1995 (utafiti wa ukatili majumbani, TAMWA 1990 - 95)
2. Report of a Pilot Study on intimate femicide in Tanzania by WiLADF (Tz) 1996 (Ripoti ya utafiti wa awali kuhusu vifo vya wnawake Tanzania na WiLDAF (Tz) 1996).

Kusisitiza ukubwa wa kutisha wa tatizo hili mkufunzi asome vichwa vya habari kutoka taarifa za magazeti kuhusu matukio tofauti ya ukalili majumbani uliotokea katika miezi miwili tu.

1. MTANZANIA 27 January 1999
   Mlokole ashukiwa kumwua mkewe
2. MTANZANIA 26 January 1999
   Mume ashutumiwa kumpiga teke mkewe na kumsababishia kuharibu mimba.
3. Daily News 22 - January 1999 - Amuua rafiki wake wa kike.
4. Daily News 19 - January 1999 - Mwanamke alazwa baada ya kupata kipigo toka kwa mumewe.
5. The Guardian 3 - February 1999 - Mahakamani kwa kutishia kumuua mkewe.
6. Mtanzania 5 - February 1999 - Mume ampiga mkewe hadi kumuua.
7. Mtanzania 8 February 1999 - Mkulima atiwa mbaroni kwa kuhisiwa kumuua mkewe.
8. Mtanzania 16 February 1999 - Mke awashwa moto na mumewe kwa madai ya ugumba
9. Mtanzania 20 Februay 1999 - ameshtakiwa baada ya kujisalimisha kwa kumuua mkewe.

Wakiwa katika makundi washiriki waelekezwe kufanya yafuatayo:-

(i) Kutoa mifano ya ukatili majumbani
(ii) Kuainisha sababu za ukatili
(iii) Kuchambua athari za ukatili majumbani
(iv) Kupendekeza jinsi polisi wanavyoweza kushughulikia matukio ya ukatili majumbani.

Kama kawaida kila kundi lichague mmoja kati yao kurejesha maoni yao kwa darasa zima. Mwishoni mkufunzi aruhusu washiriki kuongezea hoja nyingine zozote.

## ZOEZI LA NNE

### Mapendekezo ya sera za polisi za kukabili ukatili majumbani

Ni wazi kuwa hali ya kutisha ya ongezeko la ukatili majumbani haitaweza kumalizwa kwa kutumia ukali wa sheria za jinai tu. Baadhi ya hatua za kisheria zikizingatia utamaduni wa kijamii wa jamii yetu lazima zichukuliwe. Washiriki waelekezwe kwenye mapendekezo ya sera za polisi yaliyopo kwenye sanduku.

**SANDUKU HABARI 7:3**

1. Pawepo na idara ya huduma za polisi kwa jamii katika jeshi la Polisi Tanzania.
2. Watendaji wa idara hii wapewe mafunzo yatakayowapatia ujuzi wa kutoa ushauri nasaha.
3. Idara hii ambayo vitengo vyake vitaundwa katika kila kituo cha polisi zitoe huduma kwa masaa 24. Hii itakua ni kimbilio pale migogoro ya majumbani itakapotokea. Itatoa huduma ya dharura ya makazi kwa wanawake na watoto.
4. Kituo cha ushauri nasaha kichukue wajibu wa kutoa ushauri nasaha kwa wanaume wanaowafanyia ukatili wanawake (ikiwa ni hatua ya ziada baada ya kufunguliwa mashtaka).
5. Pale hali itakapodai kuingizwa kwa sheria ya jinai, polisi watawafungulia mashtaka watuhumiwa wa jinai wakitumia ushahidi uliopo.
6. Ukitilia maanani jinsi ukatili majumbani ulivyoenea na haja ya polisi kushughulikia, inapendekezwa kwamba maafisa wa polisi wawe na miongozo ya sera itakayojumuisha;

   (a) Tafsiri inayotoa maana ya ukatili majumbani
   (b) Miongozo ya namna polisi wanavyopaswa kushughulikia ukatili majumbani.
   (c) Taratibu za kuwalinda waathirika wa ukatili majumbani.
   (d) Wajibu kwa polisi kumwelekeza mwathirika huduma za msaada zinazofaa na hitaji la jumla kwa polisi kushirikiana na mashirika mengine ya kijamii yanayotoa msaada katika kushughulikia kesi za ukatili majumbani .

## ZOEZI LA TANO

**Wajibu wa polisi na waathirika wa kubakwa na makosa mengine ya kujamiiana**

Waathirika wa makosa ya kujamiiana kawaida wanakutana na hali za kuona aibu na kujisikia vibaya sana. Wanakutana na changamoto gumu sana kuamua kujitokeza ili kutumia sheria iwasaidie. Kwa ajili ya hali hii isiyovutia, waathirika wengi wa kubakwa wanawaachia wahalifu hao kuiponyoka mikono ya sheria ili wao waokoe nyuso zao na aibu. Hali hii inatokana na dhana potofu ya jamii kwamba mara nyingi waathirika wa ubakaji wamejitakia wenyewe. Cha kusikitisha zaidi, waathirika wa kubakwa ndio wanaoadhibiwa na jamii badala ya kuhurumiwa.

## KAZI YA PAMOJA

Washiriki wakae katika makundi na maswali yafuatayo yawasilishwe kwao.

1. Serikali pamoja na jamii ya kiraia wanalalamika kuwa kiwango cha uhalifu wa makosa ya kujamiiana kunaongezeka siku hadi siku Tanzania. Hatua gani serikali na mashirika ya kijamii wamechukua kupiga vita aina hii ya ukiukwaji wa haki za binadamu.
2. Kwa vile polisi ni chombo cha dola kilichopewa jukumu la kulinda utulivu, sheria na usalama katika nchi; unadhani polisi wachukue hatua gani kuwasaidia waathirika wa makosa ya kujamiiana ?
3. Je! Unadhani tuhuma kwamba chombo cha utekelezaji wa sheria Tanzania kimeshindwa kupambana na makosa ya kujamiiana ni za kweli? Kama ndio, elezea. Kama sio, toa sababu.

**Mapendekezo ya hatua za sera.**

Washiriki wapewe fursa ya kujadili mapendekezo ya sera yaliyoko hapa chini.

### SANDUKU HABARI 7:4

1. Polisi wahame kutoka kwenye mifumo ya kutibu kwenda kwenye uwakala wa kuzuia uhalifu. Hivyo yafuatayo yafanyike.

   (i) Kitengo cha huduma ya Polisi kwa jamii (kama ilivyopendekezwa katika somo lililopita) wachukue jukumu la kuwashauri wanawake namna ya kujilinda dhidi ya ubakaji.

(ii) Kitengo hicho hicho kiandae mipango ya kuifundisha jamii haja ya kuziheshimu sheria za nchi kama vile kutojihusisha katika uvunjaji wa sheria.

(iii) Polisi waainishe hatari zinazoweza kutokea na kupelekea watendaji kuhakikisha usalama wa wanawake.

(iv) Polisi waongeze juhudi katika kupambana na madawa ya kulevya ambayo ndio yanadaiwa kuwa sababu ya ongezeko la makosa ya kujamiiana.

2. Kitengo cha huduma ya polisi kwa jamii kipewe jukumu la kufanya uchunguzi wa makosa ya kujamiiana. Hii inapendekezwa kwa sababu watakuwa na ujuzi maalumu wa kuwahoji waathirika, mashahidi na majirani katika kuchukua na kutunza ushahidi na pia kuwahoji watuhumiwa. Njia ya kiutu na ya huruma itumike katika kuwashughulikia waathirika wa makosa ya kujamiiana. Yafuatayo yafanyike:-

(i) Polisi wanaoshughulikia makosa ya kujamiiana wapewe mafunzo maalumu.

(ii) Wawahakikishie waathirika kuwa wanawaamini wakati wa mahojiano.

(iii) Wamsaidie mwathirika kupata matibabu.

(iv) Wawe katika nafasi ya kuweza kumpatia mwathirika huduma ya ushauri nasaha. Hii itamrudishia mwathirika hali ya kujiamini na kujithamini.

## ZOEZI LA SITA

### Polisi na haki za wanawake wafungwa

Washiriki wagawanywe katika makundi madogo. Wapewe kazi ya kujibu maswali yafuatayo.

1. Kwa nini wanawake wafungwa wapatiwe huduma maalumu.
2. Je! Unakubaliana na hoja kwamba hatua zinazochukuliwa kulinda hadhi ya mwanamke hasa aliye mjamzito au anayenyonyesha zisichukuliwe kuwa ni ubaguzi?
3. Je! Unaridhika na ulinzi wanopatiwa wanawake kutoka kwa watekelezaji wa sheria Tanzania. Elezea jibu lako.
4. Ni hatua zipi katika sera unazoweza kupendekeza katika idara ya jeshi la polisi

za kuboresha uangalizi na heshima ya haki za binadamu za wanawake wafungwa Tanzania?

Baada ya kazi za vikundi wasaidie washiriki kujadili misingi iliyopo kwenye sanduku.

### SANDUKU HABARI 7.5

1. **Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu Ibara 2 - Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa ibara 2 Kanuni za Mienendo ya Watekelezaji wa Sheria Ibara 182, Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya wanawake Ibara ya 1 na 6. Misingi ya Kuweka Kizuizini au Kifungo ñ Msingi wa 6.**
   Wanawake waliofungwa au kuwekwa kizuizini wasipate tatizo la ubaguzi na walindwe dhidi ya aina zote za Ukatili na Unyonyaji.

2. **Vipimo vya Masharti ya Msingi ya Kuwatendea Wafungwa sharti la 53.**
   (i) Wanawake wafungwa wasimamiwe na kupekuliwa na wanawake maafisa wa polisi au wafanyakazi wa kike. Sharti la 53: Wanawake wajawazito na wanaonyonyesha wapatiwe huduma maalumu wakiwa kifungoni. Sharti la 53: Wanawake wafungwe tofauti na wanaume.

3. Kundi la Misingi ya Kuwalinda Watu Wote Walio Katika Hali ya Kuwa Kizuizini au Kifungoni aya ya 2: Hatua maalum zitakazochukuliwa kulinda haki na hadhi maalum ya wanawake hasa wajawazito na wanaonyonyesha . zisichukuliwe kuwa ni ubaguzi.

## ZOEZI LA SABA

Ulinzi na ufumbuzi kwa waathirika

Mkufunzi awaalike washiriki wawili mwanamke na mwanamume waingie katika mazungumzo kati ya Mary mwathirika wa ubakaji na Chacha, Mkuu wa Kituo kidogo cha Polisi.

**Mary:** (Akitoa taarifa kwenye meza ya polisi huku akilia) habari za jioni afande.

**Chacha:** Eh! Nini tatizo lako?

**Mary:** (anashindwa kujibu kwa sauti)

**Chacha:** Umekuja kutaka msaada halafu huwezi kujieleza. Unategemea tutakusaidiaje kama usipotuambia yaliyokupata?

**Mary:** (Akiwa bado analia) Ni vigumu kusema afande ........ lakini ........ lakini nitakuambia (anapiga makelele).

**Chacha:** Umebakwa nini mama?

**Mary:** Ndio ........ nilikuwa natembea kupita kiwanja cha mpira cha shule ya msingi Mwananyamala (anasita na kupiga kelele, lakini anajipa moyo na kuendelea) mtu mmoja mrefu mwenye nguvu akanifikia. Akanishika mkono, nikakataa lakini akanipiga ngwala nikaanguka (anapiga kelele).

**Chacha:** Acha kulia hebu endelea kunieleza.

**Mary:** Akaniangukia akanifunga mdomo kwa mkono wake. Akanikaba shingo nikadhani ninakufa.

**Chacha:** Alafu akafanyaje.

**Mary:** Ikabidi nifuate anavyotaka (anapiga ukelele kwa uchungu).

**Chacha:** We mwongo. Hujatumia vitu vyake wewe? Hujanywa bia au chochote?

**Mary:** Hapana jamani!

Chacha: Sijui, lakini nyie wasichana wa umri huu kawaida mnapokea vitu vya watu mnakubaliana muwape mapenzi baadae mnawageuka. Kama ulifanya hivyo ulijitegea mwenyewe. Hukufanya hivyo? (anamkazia macho).

**Mary:** (anapiga makelele)

**Chacha:** Nitakupa karatasi ya kupeleka kwa Daktari lakini chunga sana!

## MASWALI YA KUJADILI.

Wagawe washiriki katika makundi na uwape maswali yafuatayo.

1. Je! unadhani Majibu ya Chacha kwa Mary ni sawa? Kama ndio kwa nini? Kama sio toa sababu.

2. Hivi ni kweli kuwa watekelezaji wa sheria wana tabia kama hiyo kwa waathirika wa kosa hilo hapa Tanzania?

3. Kama ungekuwa Chacha ungefanyaje?

Kila kundi lichague atakayewasilisha majibu yao. Waongoze washiriki kujadili misingi ifuatayo katika sanduku.

## SANDUKU HABARI 7.6

TAFSIRI YA MAANA YA WAATHIRIKA WA UHALIFU

**Tamko la Misingi Muhimu ya Haki na Usawa wa Waathirika wa Uhalifu na Matumizi Mabaya ya Mamlaka.**

*Ibara1: Waathirika wa uhalifu wanatafsiriwa kumaanisha;*
*Watu ambao kibinafsi au kwa pamoja wamepata madhara yakiwemo kuumizwa kimwili au kiakili, maumivu ya kihisia, kupoteza mali au kupoteza kwa kiasi kikubwa haki za msingi kwa kupitia matendo au kutotendewa kwa jambo ambavyo ni ukiukaji wa sheria za jinai zinazotumika katika nchi, zikiwemo zile zinazofafanua* matumizi mabaya ya uwezo katika mashauri ya jinai.

**Ibara ya 2:**
*Waathirika wa uhalifu wanaweza kujumuisha (i) watu wanaomtegemea mwathirika moja kwa moja. (ii) Watu walioingilia na wakaumizwa katika kujaribu kuwalinda waathirika au kuzuia uhalifu.*

**Ibara ya 3:**
*Vifungu vya hili Tamko vinatumika sawa kwa waathirika wote bila kutofautisha katika sababu za kawaida kama vile asili, rangi, jinsia, umri, asili ya jamii na kabila.*

**Ibara ya 4:**
*Waathirika wa uhalifu watendewe kwa huruma na kwa heshima ya utu wao wanaostahili!*

(a) *Kuweza kupata vyombo vya sheria.*
(b) *Kupatiwa ufumbuzi wa tatizo lao.*
(c) *Kama ilivyo katika sheria za nchi.*

**Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu** *Ibara ya 8:*
*Kila mtu ana haki ya kupatiwa ufumbuzi unaofaa kwenye vyombo vya sheria vya taifa kwa matendo yoyote yanayokiuka haki zake za msingi zilizotolewa na katiba ya nchi au sheria.*

**Misingi Muhimu ya Haki na Usawa wa Waathirika wa Uhalifu na Matumizi Mabaya ya Mamlaka.**

**Ibara ya 5:**
*Mifumo ya kiutawala iundwe na kuboreshwa ili kuwawezesha waathirika kupata ufumbuzi kupitia njia za kawaida na zisizo za kawaida. Taratibu hizo ziwe ni za haraka, haki, zisizo na gharama kubwa na zinazopatikana.*

**Ibara ya 6:**
*Taratibu za kisheria na za kiutawala ziwe na jukumu la kuwataarifu waathirika;*
- *Wajibu wao katika mashtaka.*
- *Mipaka, muda na maendeleo ya mashtaka*
- *Hitimisho la kesi yao.*
- *Mawazo na wasiwasi wa waathirika yatolewe katika kila ngazi ya mashtaka.*
- *Waathirika wasaidiwe wakati wote kesi inapoendelea.*
- *Ucheleweshaji usio wa lazima wa kesi na utekelezaji wa maamuzi na amri kwa waathiriwa uepukwe.*

**Ibara ya 11:**
*Iwapo wakala wa dola anayetenda jambo kwa mamlaka ya kisheria au vinginevyo akikiuka sheria za jinai waathirika wapatiwe ufumbuzi kutoka kwenye dola.*

**Ibara ya 12:**
*Dola inapaswa kupanga uwezekano wa kumpatia fidia ya fedha mwathirika aliyeumizwa sana pale ambapo yule aliyepaswa kulipa fidia hawezi kutokana na kifo au kushindwa. Mwathirika apate fidia ya fedha toka serikalini.*

**Ibara ya 13:**
*Dola ifanye mpango wa kuanzisha fungu la taifa la kuwafidia waathirika.*

**Ibara ya 14:**
*Waathirika wanapaswa kupokea misaada ya lazima ya mali, matibabu, kisaikolojia au ya kijamii kutoka serikalini, mashirika ya kijamii na njia za kawaida..*

**Ibara ya 15:**
Waathirika waelezwe kuhusu huduma za afya na za kijamii zilizopo na wasaidiwe kuzifikia.

**Ibara ya 17:**
Uangalizi maalum utolewe kwa waathirika wenye mahitaji maalumu kutokana na hali ya madhara waliyoyapata au hali nyinginezo zinazoweza kuwaletea madhara kwa hali fulani.

## ZOEZI LA NANE

**Hatua za kiutendaji katika kutekeleza hatua za kulinda na kuwapatia ufumbuzi waathirika wa uhalifu.**

Wagawe washiriki katika makundi madogo na uwaelekeze kufanya kazi ifuatayo;

### KUNDI LA I
Orodhesha hatua zinazotekelezeka za kuchukua kuhakikisha waathirika wa uhalifu wanapatiwa ulinzi na ufumbuzi kama inavyotakiwa na sheria za kibinadamu za kimataifa..

### KUNDI LA II:
Kundi lijione kama watu walio katika mamlaka na uongozi. Waandae sera watakayoitumia kushawishi wizara husika kuhakikisha kwamba hatua za ulinzi na ufumbuzi wa waathirika zinapatikana.

### KUNDI LA III:
Tayarisha igizo fupi kuonesha hali halisi ambapo ulinzi na ufumbuzi kamili kwa waathirika utapatikana.

**Angalizo kwa Mkufunzi.**
Kwa hatua zinazotekelezeka, mkufunzi arejee kwenye mwongozo wa Umoja wa Mataifa (UN manual on Human Rights Uk. 143).

## REJEO

1. Watu wote bila kujali umri, jinsia, lugha, asili n.k. wako sawa mbele ya sheria, hivyo wanastahili heshima ya utu wao.

2. Mfumo wa utekelezaji wa sheria lazima utoe ulinzi maalumu kwa watoto na wanawake kwa mujibu wa sheria na vipimo vya kimatifa vya haki za binadamu.
3. Hatua zinazochukuliwa kuwalinda watoto na wanawake zisichukuliwe kuwa ni za kibaguzi.
4. Hatua maalum za sera zinapaswa kutekelezwa na jeshi la polisi kusaidia waathirika wa uhalifu.

## REJEA

**Kwa ufafanuzi zaidi rejea.**


1. UN High Commission for Human Rights: **Human rights and Law Enforcement: A manual on Human rights Training for Police (Professional traiing series No. 5)** Geneva Switzeland 1997).

2. Das D na Peter C. **Human Rights and law Enforcement: Lesson Plan:** Dar Es Salaam 1999.

# SURA YA NANE

## POLISI NA HAKI ZA WAKIMBIZI NA WAGENI.

### Utangulizi

Hakuna ubishi kwamba suala la wakimbizi ni mojawapo ya matatizo makubwa ulimwenguni. Hakika, tatizo la wakimbizi sio tu kwamba linazidi kuwa gumu kutatua bali ni ukweli kwamba linazidi kuongezeka kila siku, ndicho kinacholifanya liwe la kutisha zaidi. Wakati 1951 wakimbizi waliokuwa chini ya uangalizi wa Tume ya Umoja wa Mataifa ya Wakimbizi walikuwa hawazidi milioni moja, sasa wameongezeka kufikia zaidi ya milioni kumi na tano. Sababu za hali hiyo ni nyingi, lakini hasa zinazojitokeza ni zile za kijamii, kisiasa kama maafa, umaskini, mateso na mauaji yanayochochewa kisiasa. Tanzania ni nchi mojawapo iliyoathirika vibaya na tatizo hili. Tangu miaka ya sitini (1960) Tanzania imepokea wakimbizi kwa wingi toka Afrika Kusini, na majiriani zake wa maziwa makuu kama Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (DRC). Ingawaje hakuna wakimbizi zaidi toka Afrika Kusini bado Tanzania inapokea mamia ya wakimbizi toka Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (Zaire) na Rwanda kila siku.

Cha ajabu katika sura hii ni ukweli unaosikitisha kuwa, sababu nyingi zinazopelekea watu wakose makazi zinatokana na ukiukwaji wa haki za binadamu. Kwa ujumla hali hii ni matokeo ya utumiaji mbaya wa madaraka kwa upande wa serikali au kushindwa kulinda haki za raia wake. Watekelezaji wa sheria wanaingia moja kwa moja katika hali hii kwa vile wao ndio waangalizi wa haki za watu. Kwa upande mwingine ni ukweli kuwa wakimbizi wanaingia katika kundi la watu maalumu kuhusiana na ukiukwaji wa haki za binadamu. Katika nchi wanakopokelewa kuna uwezekano mkubwa wa wakimbizi kupata huduma katika hali ya kuchokwa na wananchi na hata serikali. Kutokana na haya basi, ni muhimu kuangalia katika mfumo wa sheria Tanzania na vipimo vya kimataifa vya haki za binadamu kwa wakimbizi na wasio raia (wageni).

### MATARAJIO

Mwishoni mwa sura hii washiriki wanategemewa wawe wameelewa;

1. Maana ya wakimbizi na wageni.
2. Haki za wakimbizi kwa mujibu wa vyombo vya Kimataifa vya Haki za Binadamu na sheria za nchi.
3. Wajibu wa kuwapokea wakimbizi na kuwatendea kiutu.

## ZOEZI LA KWANZA

**Maana ya mkimbizi na mgeni**

Mkufunzi, wagawe washiriki katika makundi madogo, wagawie kadi zilizopo hapo chini, kila kadi kundi moja. Waelekeze kuzisoma na kujadili, kuangalia iwapo anayetajwa ni mkimbizi au mgeni.

## KADI 1




Kaihatu ni raia wa Japan, anakimbia kwao kutokana na kutokuwa na kazi na anakuja Tanzania. Anadai kwamba serikali yao haiwezi kumlinda dhidi ya kukosa ajira.

## KADI YA 2



Ngedakumana ni Mnyarwanda. Amevuka mpaka na kuingia Tanzania kukimbia mauaji yanayofanywa na kikudi cha waasi wa Kihutu kiitwacho Interahamwe ambacho kipo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

## KADI YA 3



Kaluna ni raia wa Kongo. Yeye na wenzie wawili walipanga mpango wa kuiangusha serikali ya rais wa nchi yao. Mpango wao ukashindwa wamekimbilia Tanznaia kuokoa maisha yao.

## KADI YA 4



Muholangana ni raia wa Zambia. Yeye ni muumini wa kundi la wanaomwabudu shetani. Kundi hili linamwabudu shetani na waumini wake wanamwita shetani ni Bwana wao. Serikali ya Zambia imeipiga marufuku dini hii na kuwakamata waumini wake isipokuwa Muholangana ambaye amekimbilia Tanzania kwa hofu ya kuadhibiwa.



Baada ya kuwasilisha mkufunzi atoe ufafanuzi wa maana ya mkimbizi na mgeni kama ilivyo kwenye sanduku hapo chini.

### SANDUKU HABARI 8.1

**SHERIA YA WAKIMBIZI 1998**

***Kifungu cha 4 (a):*** *Mkimbizi kwa mujibu wa sheria hii ni mtu yeyote aliye nje ya nchi yake au nchi anakoishi kutokana na hofu ya kuuawa kwa ajili ya asili yake, dini, uraia, uanachama wa kundi fulani la kijamii (kabila) na hawezi au hayuko tayari kurudi nchini kwake au nchi anayaoishi kwa hofu hiyo.*

*b) Analazimika kuondoka katika nchi anakoishi kutafuta ulinzi mahali pengine nje ya nchi yake ya uraia kutokana na uvamizi kutoka nje, kuingiliwa au kutawaliwa na taifa la kigeni ambavyo vinatishia usalama wa umma katika nchi yake hiyo ya asili au aliko raia.*

*c) Yuko kwenye kundi la watu ambao kwa tangazo la serikali wametangazwa kuwa wakimbizi kwa sababu zilizoainishwa katika aya (a) na (b) hapo juu.*

**Kifungu cha 4 (3)** *kwa mujibu wa sheria hii, mtu atasemekana kuwa si mkimbizi tena iwapo:*

*(a) Kwa hiari yake amerudi nchini kwao.*
*(b) Baada ya kupoteza uraia ameupata tena kwa hiari yake.*
*(c) Amepata uraia mpya na anafaidi ulinzi katika uraia huo.*
*(d) Kwa hiari yake amejijenga katika nchi aliyoondoka au nje alikoamua kubaki.*
*(e) Iwapo hawezi tena kukataa kuwa chini ya uangalizi wa nchi alikotokea au alikokuwa anaishi kutokana na hali iliyomfanya kuwa mkimbizi kubadilika.*
*(f) Iwapo baada ya kupokelewa kama mkimbizi amefanya kosa kubwa lisilo la kisiasa nje ya nchi alikopewa ukimbizi.*
*(g) Amekiuka kwa kiwango kikubwa madhumuni ya Mkataba wa Wakimbizi wa mwaka 1969 wa Umoja wa nchi Huru za Afrika (OAU)*
*(h) Amejiingiza kwenye mambo ya kisiasa wakati anafaidi ukimbizi Tanzania.*

**Kifungu cha 4 (4)** *Kwa mujibu wa sheria hii mtu hatahesabika kuwa ni mkimbizi iwapo;*

*(a) Ametenda kosa la jinai dhidi ya amani, kosa la jinai la kivita au kosa la jinai dhidi ya utu.*
*(b) Ametenda kosa zito sana la jinai lisilo la kisiasa nje ya nchi yake ya ukimbizi kabla hajapokelewa kama mkimbizi Tanzania.*
*(c) Amepatikana na hatia kwa kosa alilotenda kinyume na madhumuni ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika au Umoja wa Mataifa.*
*(d) Alishapatiwa hadhi ya ukimbizi au makazi nchi nyingine kabla ya kuingia Tanzania.*
*(e) Alipitia nchi nyingine moja au zaidi kabla ya kufika Tanzania na ameshindwa kutoa sababu za kutotafuta makazi katika nchi hizo.*

**Mkataba wa Kimataifa kuhusu Hadhi ya Wakimbizi: Ibara ya 1 A (2).**

*Mkimbizi ni mtu ambaye kutokana na hofu ya msingi ya kuuawa kwa sababu ya asili, dini, uraia, kabila au maoni yake ya kisiasa ameshindwa au hayuko tayari kurudi nchini kwao (au kama hana nchi (uraia) kwenye nchi ambayo anaishi kawaida.*

**Wageni:**
Hawa ni watu ambao si raia wa nchi ambamo wapo.

## ZOEZI LA PILI

**Habari ya kubuni ya gazetini**

Mkufunzi awaelekeze washiriki kuangalia habari katika sanduku hapa chini. Inashauriwa kumtaka mmoja wao aisome kwa sauti mbele ya wengine.

Ukurasa 1: Daily Vision: Jumatatu 4 - January 1999.

### WAZIRI WA MAMBO YA NDANI ANATAKA POLISI WAWADHIBITI WAKIMBIZI

Na Mwandishi wetu.

Waziri wa Mambo ya Ndani Ndugu Austin Mrima jana aliwapa changamoto maafisa wa polisi nchini kuacha kuwatendea wakimbizi kilaini laini. Katika hotuba yake ya ufunguzi wa warsha ya siku mbili iliyoandaliwa na jeshi la polisi, katika ukumbi wa Karimjee alisema, idadi kubwa ya kutisha ya wakimbizi Tanzania imechangiwa kwa kiasi kikubwa na jinsi watekelezaji wa sheria wanavyowatendea wakimbizi hao.

Amri ilishatolewa tangu siku nyingi kwamba polisi wa mipakani wapokee idadi ndogo ya wakimbizi iwezekanavyo lakini polisi hawajaizingatia amri hii. Wanamruhusu kila mtu tu anayekimbilia Tanzania. Hii tabia lazima ikomeshwe alisisitiza Waziri. Akaongezea kwamba Tanzania inaathirika na uharibufu wa mazingira, kiwango kikubwa cha makosa ya jinai kwa sababu ya idadi kubwa ya wakimbizi iliyokosa udhibiti.

Alishangaa kwa nini hao wakimbizi wasikimbilie nchi nyingine zaidi ya Tanzania. Zaidi ya hapo Waziri aliwalaumu wakuu wa polisi kambini kwa kushindwa kudhibiti vitendo vya kisiasa katika kambi. Kwanza kwa nini polisi wawaruhusu wakimbizi kufanya mikutano? Mikutano ya aina yoyote isiruhusiwe kambini. Ni katika hiyo mikutano ndio wanapanga kwenda kupigana na serikali. Na sasa ninatoa amri kwa polisi kukamata viongozi wa vitendo hivyo. Hakikisha wakimbizi wanawataja viongozi wao. Mnajua jinsi ya kuwafanya waongee. Hili sio jambo la kichekesho.Tumia hata nguvu ili wasemeî. Alisema Waziri huku akicheka.

## KAZI YA PAMOJA

Sasa waongoze washiriki kujadili misingi ya Haki za Binadamu inayohusu wakimbizi na wageni.

## SANDUKU HABARI 8:2

### Mkataba wa Kimataifa wa Wakimbizi

**Ibara ya 2:**
Kila mkimbizi ana wajibu wa kutimiza/kufuata sheria, kanuni na hatua zote zinazochukuliwa kulinda usalama wa umma katika nchi alikopokelewa.

**Ibara ya 3:**
Yaliyomo katika Mkataba yatatumika kwa wakimbizi wote bila kujali asili, dini au nchi aliyotokea.

**Ibara ya 15:**
Wakimbizi wapatiwe huduma nzuri ya kufaa kama wanavyotendewa raia wa kigeni kuhusu vyama vya wafanyakazi au vyama visivyo vya kisiasa au vya kujitolea.

**Ibara 16:**
Wakimbizi walio katika nchi kihalali wana haki ya uhuru wa kwenda watakako na wa makazi.

**Ibara ya 16:**
Wakimbizi wana haki ya kupata huduma za mahakama na msaada wa kisheria.

**Ibara ya 27:**
Mkimbizi yeyote asiye na hati halali ya kusafiria lazima apatiwe kitambulisho.

**Ibara ya 28:**
Hati za kusafiria lazima zitolewe kwa mkimbizi yeyote ili kumwezesha kusafiri nje ya nchi aliyoko labda tu kwa sababu za usalama wa taifa.

**Ibara ya 31:**
Mkimbizi yeyote atakayekuwa kwenye nchi kinyume cha sheria na akiwa ametokea kwenye nchi ambayo ina mauaji akiisha kujitambulisha mara moja na ipasavyo kwenye mamlaka husika asiadhibiwe.

**Ibara ya 32:**
Mkimbizi yeyote asifukuzwe, labda tu kwa sababu za usalama wa taifa, utulivu wa umma na kwa uamuzi uliotolewa kwa mujibu wa sheria.

## Angalizo kwa mkufunzi

Mkufunzi awakumbushe washiriki kuwa haki zilizotajwa hapo juu pia zinapatikana katika vyombo vya sheria za kibinadamu kama;

Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu, Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa, Mkataba wa Kiafrika Kuhusu Haki za Watu na Haki za Binadamu. Washiriki pia wakumbushwe kwamba haki zifuatazo zilizopo kwenye Tamko la Haki za Binadamu, Katiba ya nchi na Mkataba wa Kiafrika wa Haki za Watu na Haki za Binaadamu pia zinatumika kwa hali ya wakimbizi.

- Haki ya kuishi na ulinzi binafsi.
- Uhuru wa kutoteswa au kutendewa maovu.
- Haki ya kutambuliwa kama mtu mbele ya sheria.
- Haki ya usawa mbele ya sheria na kupata ulinzi wa sheria kwa usawa.
- Uhuru wa kutokukamatwa ovyo na kuwekwa vizuizini.
- Haki ya kusikilizwa na kupatiwa maamuzi ya haki na wajibu na katika makosa ya jinai.
- Uhuru wa kutoingiliwa katika faragha, familia, nyumbani au mawasiliano.
- Haki ya Uhuru wa kufikiri, dhamira na dini
- Haki ya uhuru wa kutoa maoni na kujieleza.
- Haki ya kujumuika kwa amani na kujiunga katika umoja wowote.

### KAZI ZA VIKUNDI

Wagawe washiriki katika makundi manne na uwapatie kazi ifuatayo.

**Kundi la 1**

Je! Ungekuwa ndio mkuu wa Polisi Tanzania na umegundua amri ya Waziri haiwezi kutekelezwa katika ujumla wake kwa vile kuna hatari ya kukiuka haki za msingi za baadhi ya wakimbizi na unafikiri kumwandikia Waziri kumshauri katika suala hilo. Je! ni mambo gani maalum ambayo ungemweleza?

**Kundi la 2**

Wewe ni Mkuu wa Idara ya upelelezi wa makosa ya Jinai katika Jeshi la Polisi Tanzania. Una wajibu wa kumshauri Waziri kuhusu masuala ya kisheria na ya kiutawala yanayohusu makosa ya jinai. Waziri amepokea barua kutoka shirika la Amnesty International wakimlaumu kuwa hotuba yake ilikuwa ikiwachochea Polisi kufanya matendo ya kukiuka haki za wakimbizi. Waziri anakujia akiwa amekata tamaa. Anakutaka umshauri kwa maandishi kiasi gani hotuba yake ilikuwa inakiuka haki za binadamu. Mshauri ipasavyo.

**Kundi la 3**

Wewe ni Afisa Mkuu wa Polisi mstaafu. Umesikia hotuba ya Waziri redioni na kuisoma kwenye gazeti. Unadhani Waziri hakuwa mwangalifu katika maneno yake. Unataka kumwandikia Waziri barua itoke kwenye gazeti la kila siku 'Daily vision' kwenye makala ya 'kusema ukweli' je, Ni mambo gani utayaibua?

**Kundi la 4**

Isome kwa makini hotuba ya Waziri na uamue ni kwa kiasi gani inaendana na misingi ya sheria na haki za binadamu na kwa kiasi gani inakiuka misingi hiyo. Chagueni watu wawili kutoka katika kundi lenu ambao watafanya mjadala mbele ya darasa. Mmoja aunge mkono hotuba ya Waziri mwingine aipinge kwa misingi ya Haki za Biandamu na Haki za Kikatiba.

## ZOEZI LA TATU

### Polisi na haki za wasio raia/wageni

Washiriki waelezwe tangu mwanzo kuwa kundi hili la watu katika sura hii ni tofauti na wakimbizi. Kuna watu ambao ni wageni katika nchi waliyomo au wanamoishi lakini sababu zilizowaleta zinawatofautisha na wakimbizi. Wageni wanaokuja kwa sababu za ajira, utalii, biashara, masomo n.k. ndio wanaohusu kundi hili.

**Waelekeze washiriki kutafakari hali iliyoko kupitia mfano huu.**

Kundi kubwa la watu kutoka nchi 'S' ambayo inapakana na nchi jirani na Tanzania kwa upande wa Kaskazini Mashariki wamehamia Tanzania. Watu wengi kati ya hao wameajiriwa katika sekta ya usafiri. Bahati mbaya wengi wa watu hao hawafuati au hawazingatii sheria. Wanajihusisha katika wizi wa kutumia silaha, usafirishaji wa madawa ya kulevya na wanajihusisha na wizi wa nyara za serikali. Hawa watu wanafahamika kwa vurugu zao na uharamia. Hivi karibuni watu hawa waliingia kinyume cha sheria katika mkoa wa kaskazini mashariki mwa Tanzania licha ya kufanya uwindaji haramu wa wanyama pori, waliwauawa wenyeji bila huruma.

Polisi waliingilia na katika tukio moja, walirushiana risasi kati ya kundi la wavamizi hao na Polisi. Mkuu wa polisi wa Wilaya hiyo aliuawa katika zoezi hilo. Hivi karibuni kundi hilo limetoa tishio la kumteka nyara Mkuu wa Wilaya hiyo iwapo serikali haitaacha kampeni dhidi yao. Katika nia ya kukabili uhalifu nchini kwa ujumla na hasa katika mkoa wa kaskazini mashariki, Mkuu wa polisi Tanzania ametoa amri kwa polisi kumkamata kila mtu anayetoka nchi S. Kwa mujibu wa amri hiyo, atakayekamatwa ahojiwe na kila inapowezekana makazi na magari yao yapekuliwe. Kazi yao ithibitishwe na pakiwa na wasiwasi wowote kuhusu mtu huyo apewe amri ya kuondoka nchini mara moja.

Zaidi ya hayo aliamuru kwamba wahamiaji hao wasiruhusiwe kutoka nje ya nchi hadi itakapotangazwa tena. Hii ni kuhusiana na vita vya serikali dhidi ya usafirishaji wa madawa ya kulevya na wizi wa nyara za serikali.

Sasa Wasaidie washiriki kujadili misingi ya haki za binadamu ifuatayo na wachambue kutoka kisa hicho hapo juu yapi yamezingatia haki na yapi hayakuzingatia.

## SANDUKU HABARI 8:3

**Tamko la Wageni (wasio raia) Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu, Mkataba wa Kiafrika kuhusu Haki za Watu na Haki za Binadamu.**

*Kila mtu anastahili kupata haki na uhuru ulioelezwa katika tamko hili bila kujali tofauti za kiasili, rangi, jinsia, dini, siasa au utaifa.*

*(i) Kila mtu ana haki ya kutambuliwa kama mtu mbele ya sheria. Watu wote ni sawa mbele ya sheira na wanastahili bila ubaguzi kulindwa na sheria na wanastahili ulinzi sawa dhidi ya ubaguzi. Ulinzi wa Haki za Binadamu na uhuru wa msingi unaotolewa na vyombo vya kimataifa utahakikishiwa watu ambao ni wageni katika nchi wanamoishi.*

(ii) Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa Ibara ya 13.

*Mgeni aliye kisheria katika nchi mwanachama wa Mkataba huu anaweza kufukuzwa katika nchi aliyoko pale tu ambapo uamuzi umefikiwa kwa mujibu wa sheria na ataruhusiwa kutoa sababu za kujitetea dhidi ya kufukuzwa huko na shauri lake kuangaliwa upya na chombo chenye uwezo kimamlaka na apatiwe uwakilishi wa kisheria akiwa mbele ya chombo hicho au mbele ya mtu aliyeteuliwa na chombo hicho. Inaweza iwe vinginevyo pale tu itakapothibitika kuna sababu za lazima za kiusalama wa Taifa zisizoweza kuruhusu hali hiyo.*

Mkataba wa Kiafrika kuhusu Haki za Watu na Haki za Binadamu, Ibara ya 12.

1. Kila mtu atakuwa na haki ya kujongea na kuwa na makazi ndani ya mipaka ya nchi ili mradi havunji sheria.
2. Kila mtu atakuwa na haki ya kuondoka nchini ikiwa ni pamoja na nchi yake na haki ya kurudi nchini mwake. Haki hii itategemea tu yale masharti yaliyowekwa kisheria kwa ajili ya kulinda usalama wa taifa, sheria na taratibu, afya ya jamii au maadili.
3. Kila mtu atakuwa na haki ya kutafuta hifadhi katika nchi nyingine kwa mujibu wa sheria za nchi hizo pamoja na mikataba ya kimataifa, pale anapokabiliwa na vitendo vya udhalimu.
4. Mwananchi anayepokelewa kama mgeni katika nchi ambayo ni mwanachama wa Mkataba huu anaweza kufukuzwa kutoka nchi alikopokelewa endapo tu uamuzi wa kumfukuza utafanyika kwa mujibu wa sheria.

5. Ufukuzaji wa kundi la wageni hautaruhusiwa. Ufukuzaji wa kundi kubwa una maana ya ule wenye kulenga utaifa, kabila au dini.

## REJEO

1. Wakimbizi ni binadamu kwa hiyo wanastahili heshima ya utu wao kama raia wengine.
2. Kila mtu anastahili haki zilizoainishwa katika Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu bila kujali asili, lugha rangi au nchi anayotokea.
3. Hairuhusiwi kuwarudisha wakimbizi makwao, labda wakubali kwa hiari yao wenyewe na baada ya kuhakikisha badiliko la hali iliyowafanya wawe wakimbizi.
4. Kila mtu ana haki ya uhuru wa kujongea kwenda atakako na makazi katika mipaka ya nchi atakapokaribishwa mradi azingatie sheria.
5. Mgeni aliyekaribishwa katika nchi hatafukuzwa labda tu kwa kufuata uamuzi uliotolewa na mahakama na uliofikiwa kwa mujibu wa sheria.

## REJEA

**Kwa ufafanuzi zaidi rejea:**


1. UN High Commissioner for Human Rights: **Human Rights and Law Enforcement: A manual on human rights trainig for police (professional training series No. 5).**
2. Das D na Peter C. **Human Rights and Law Enforcement, lesson plan Dar es Salaam 1999.**

# SURA YA TISA

# HAKI ZA BINADAMU KATIKA UTAWALA WA MAMLAKA ZA POLISI

## Utangulizi

Ni wazi kwamba chombo cha utekelezaji wa sheria ni muhimu sana katika vyombo vya serikali. Ndio njia inayotumiwa na serikali katika kutimiza wajibu wake wa kuhakikisha amani na usalama wa raia katika mipaka yake. Vile vile chombo cha utekelezaji wa sheira ni muhimu zaidi kwa serikali kwa vile kinatumika kuhakikisha ulinzi wa haki za binadamu za raia kwa mujibu wa wajibu wa nchi katika sheria za kimataifa.

Hata hivyo, polisi ni muhimu katika kazi za serikali kama ilivyo muhimu kwa serikali yenyewe katika kuhakikisha utawala na uongozi mzuri wa uwakala wa polisi. Kwa lugha nyingine serikali haiwezi kuwa na jeshi la polisi linaloheshimu haki za binadamu, demokrasia na utawala wa sheria iwapo haitilii maanani masuala ya utawala na uangalizi. Kwa maana hiyo hiyo juhudi zifanyike kuingiza mifumo ya usimamizi wa usalama katika utekelezaji wa sheria. Sura hii hasa inajaribu kuhamasisha maafisa wa polisi walio katika utawala na mamlaka ya jeshi la polisi kuhusu wajibu wao wa kulinda na kukuza heshima ya haki za binadamu katika kazi za kila siku za polisi.

## MATARAJIO

Mwishoni mwa sura hii washiriki wanatarajiwa waweze kutambua mahitaji ya haki za binadamu katika utawala na mamlaka.

## ZOEZI LA KWANZA

Kwa kutumia yaliyomo katika ukurasa wa 53 wa mwongozo wa kufundisha haki za binadamu (The human rights and law enforcement manual on human rights training for the police, 1997), ukurasa wa 39, wa mpango wa kufundishia (Lesson Plan 1999) mkufunzi awapatie washiriki mhadhara mfupi juu ya vipengele muhimu vya haki za binadamu na utawala na mamlaka ya polisi kama ilivyo hapa chini.

1. Utawala na amri za jeshi la polisi lazima vitilie maanani yaliyomo katika kanuni za mienendo kwa watekelezaji wa sheria.
   - (i) Kila chombo cha utekelezaji wa sheria kinapaswa kuwakilisha na kuitikia na kuwajibika kwa jamii kwa ujumla.
     - (ii) Maafisa watawajibika kibinafsi chini ya sheria kwa matendo yao au kwa kutotenda kwao.

2. Amri na utawala wa polisi lazima zizingatie misingi ifuatayo.

(i) **Nia na madhumuni.**

- Hizi lazima zielezwe kwa uwazi na mbele ya umma na zijumuishe;
- Kuzuia na kutambua uhalifu.
- Kulinda usalama wa umma
- Kutoa misaada ya kibinadamu wakati wa dharura
- Kukuza na kulinda haki za binadamu.

Hili Tamko la nia na madhumuni lazima liwekwe bayana kwa umma na juhudi zifanyike kulitangaza.

**(ii) Maadili ya kitaaluma**

Idara ya utawala na utoaji wa amri itayarishe kanuni za hali ya juu za maadili ya kazi. Hii ni kwa kuhakikisha uangalizi wa sheria ya polisi na miongozo. Lazima itilie maanani matatizo ya kimaadili na wajibu na ihusiane pia na madhumuni ya jeshi la polisi.

**Angalizo:**

a) Misisitizo maalumu katika kanuni lazima uelekezwe katika kuheshimu haki za binadamu.

(b) Kanuni hizo ziwekwe wazi kwa umma na juhudi zifanyike kuzitangaza ili zijulikane kwa wote

**(iii) Mpango wa utekelezaji na utendaji wa Polisi**

Huu ni mtiririko wa kuunda sera na mpango unaotarajiwa kupata madhumuni na nia ya jeshi la Polisi. Kwa hali yoyote mpango huu lazima katika mambo yote utafute kuendeleza ulinzi na kukuza utu wa mtu na Haki za binadamu. Mpango huo lazima uangalie mabadiliko ya kidemokrasia na kikatiba, kiwango cha makosa ya jinai, vurugu katika umma, maendeleo ya kiteknolojia na hisia za watu.

**(iv) Mifumo ya utawala na Amri za Polisi**

Mifumo ya utawala na amri za polisi zifanyiwe mabadiliko (zitazamwe upya mara kwa mara) kuendeleza uwajibikaji na utendaji wa polisi. Hii inaweza kutekelezwa kupitia sheria na njia za kutoa taarifa kwa serikali na kwa umma wa watu.

## KAZI ZA VIKUNDI

Mkufunzi awagawe washiriki katika vikundi vidogo, na awapatie kazi ifuatayo:

1. Kwa kuwa utawala na amri nzuri za polisi ndizo zinazowasiliana na ukweli wa mambo katika kazi za kila siku, tayarisha miongozo ya kazi kwa uongozi na waamrishaji (makamanda) katika Jeshi la Polisi Tanzania.
2. Pendekeza kanuni za maadili ya kitaaluma kwa watekelezaji wa sheria Tanzania.
3. Pendekeza njia ambazo viongozi na waamrishaji katika Jeshi la Polisi watazitumia kupata habari za mahitaji ya raia.
4. Pendekeza mfumo ambao utasaidia kuwawezesha wakuu wa polisi kufahamu polisi gani wa ngazi za chini, anakiuka haki za binadamu na nani anazifuata.

Mwisho wa mrejesho toka vikundi mkufunzi awaongoze washiriki kujadili masuala yaliyojitokeza wakati wanawasilisha hoja zao.

## REJEO

Utawala na amri za polisi kila mara lazima zizingatie na kuhakikisha uangalizi wa haki za binadamu unafanywa na Polisi watendaji. Hii inaweza kufanyika kwa kutoa tamko kwa raia (umma) la kanuni na nia ya Polisi. Kanuni ya hali ya juu ya maadili ya kitaaluma kwa polisi wote, kuingia katika utayarishaji mpango wa utekelezaji utakaohakikisha malengo yanatimizwa na kuangaliwa kwa upya na kubadilisha mifumo ya utawala na uamrishaji.

## REJEA

Kwa ufafanuzi zaidi rejea:


1. U.N High Commission for Human Rights
   **Human Rights and Law Enforcement:**
   **A manual on Human rights training for police** (Professional training series: No. 5. Geneva, Switzerland 1997)

2. **Das D na Peter C. Human Rights and Law Enforcement: Lesson Plan; Dar es Salaam 1999.**

## SEHEMU III

## SURA YA KUMI

# UFUATILIAJI NA TATHMINI

**Utangulizi**

Baada ya kuangalia masomo ya msingi katika mafunzo inashauriwa kwamba washiriki katika ngazi hii wajifunze jinsi ya kufuatilia na kutathmini mpango huu wa mafunzo. Ni kupitia ufuatiliaji na tathmini ya mpango wa mafunzo ya Haki za binadamu kutakakowezesha wakufunzi kupima matokeo, uwezo na kufaa kwa mpango.

## ZOEZI LA KWANZA

**Maana ya ufuatiliaji na tathmini.**

Kabla ya kutoa tafsiri ya maana ya maneno haya mawili kama yalivyoandikwa kwenye vitabu, kwanza washiriki wasukumwe kujaribu kutoa maana wanazozifahamu. Njia rahisi na itakayofaa zaidi katika zoezi hili ni kugawa kadi kwa washiriki katika makundi madogo. Kila kundi liandike maana waliyoifikiria, kwenye kadi moja maana ya ufuatiliaji na kadi nyingine tathmini. Waandishi wa kila kundi wasome mbele ya darasa maana zao. Mkufunzi akusanye kadi hizo na kuzibandika kwenye ukuta.

Washiriki waelezewe maana ya maneno hayo mawili, ufuatiliaji na tathmini kama yalivyo kwenye sanduku.

**SANDUKU HABARI 10:1**

> Tathmini ina maanisha zoezi linalofanyika wakati au baada ya kutekeleza jambo lililokuwa limepangwa ili kuhakikisha iwapo madhumuni yake au kiwango kilichokusudiwa kumefikiwa pia kuwezesha utaratibu wa kujifunza ili utekelezaji uboreshwe hapo baadaye. (Donald Kirk Partick. (Supervisory Training and Development 1970).
>
> Ufuatiliaji unamaanisha zoezi la vipindi la kuchunguza tendo au mpango unaoendelea linalofanywa na watekelezaji wa mpango huo kwa nia ya kuhakikisha kama mpango au jambo hilo liko katika mstari kulingana na madhumuni yaliyokusudiwa.

## ZOEZI LA PILI

**Umuhimu wa kufanya mpango wa ufuatiliaji na tathmini.**

Wagawe washiriki katika makundi madogo. Waelekeze wajaribu kuainisha faida za mpango wa ufuatiliaji na tathmini. Majibu yao yaandikwe katika karatasi kubwa la ubaoni na yawasilishwe kwa kundi lote kubwa.

Mwishoni mkufunzi aunganishe majibu ya washiriki na haya yaliyopo kwenye sanduku hapo chini.

### SANDUKU HABARI 10:2

**Sababu za ufuatiliaji wa mpango**

Kuhakikisha mradi hautoki nje ya madhumuni yaliyokusudiwa na njia zilizokubaliwa

(i) Kuhakikisha utekelzaji mzuri wa mradi au tukio
(ii) Kuhakikisha matumizi mazuri ya nyenzo na gharama nafuu
(iii) Kushughulikia masuala yanayojitokeza na kuyaangalia mambo ambayo labda hayakutiliwa maanani wakati wa kupanga
(iv) Kuwa na sababu ya kubadili na kusahihisha.

**Sababu za kutathmini mpango**

(i) Kuboresha utekelezaji wa mpango
(ii) Kupata mwanga wa kuandaa sera katika ngazi zote
(iii) Kupata uelewa wa jinsi mpango unavyoendeshwa
(iv) Kuongoza ugawaji wa nyenzo na kuboresha matumizi mazuri ya nyenzo
(v) Kuhakikisha ubora wa mpango
(vi) Kufanya mapitio ya madhumuni na kazi katika mradi au mpango kwa ajili ya umaana wa kuendelea.

**Angalizo:**
Iwekwe wazi kuwa tathmini na ufuatiliaji vinahitajika na wenye dau wote katika mpango kama vile wakufunzi, wanafunzi wafadhili n.k.

# ZOEZI LA TATU

**Viashirio vya kufaulu, kushindwa na ubora wa mradi;**
**Viashirio vya thamani**

Washiriki waagizwe kuainisha viashirio vya kufaulu na ubora wa mafunzo ya haki za binadamu kwa upande mmoja, na viashirio vya udhaifu (kushindwa) katika upande mwingine. Kisha waongoze washiriki kujadili viashirio vilivyo katika sanduku hapa chini.

**Viashirio vya wingi (idadi)**

Mafunzo: Vyuo vingapi vya polisi vina somo la haki za Binadamu katika mtaala wao, ni vituo vingapi vya polisi vina polisi waliopata mafunzo? Ni mikoa mingapi Tanzania imefaidika na mafunzo ya haki za Binadamu?

## SANDUKU HABARI 10:3

1. **MREJESHO – MTAZAMO**
   Jamii inafikiriaje na walengwa wanafikiriaje juu ya mpango wa mafunzo?

2. **KUJIFUNZA**
   Je walengwa wana uelewa zaidi wa ujuzi uliopatikana wakati wa mafunzo ukilinganisha na wengine ambao hawakushiriki mafunzo? Hii inaweza kujaribiwa katika mitihani maalum. Dodoso kwa washiriki na mahojiano.

3. **TABIA**
   Kuna mabadiliko yoyote yanayoonekana ya tabia au mtazamo? Hii inaweza kujaribiwa kupitia:
   - Jaribio la kujichunguza kibinafsi
   - Kujitathmini kibinafsi
   - Mahojiano
   - Majadiliano yaliyolengwa kwa kundi maalum
   - Kuangalia utendaji

4. **MATOKEO**
   Faida gani zinaonekana kwa jeshi la polisi, mfano ongezeko la kuihudumia, jamii? Ushirikiano umepatikana kutoka kwa wana jamii. Mafanikio yameongezeka katika kugundua makosa na kufungua mashtaka. Haya yanaweza kujaribiwa kwa kutumia:
   - Dodoso na mahojiano
   - Kukagua ripoti za polisi

5. **YATOKANAYO**
   Matunda gani ya ziada yametokana na mpango mzima mfano mabadiliko ya Polisi na sheria.

### Kutathmini mpango wa mafunzo ya haki za binadamu

Tathmini inaweza kufanyika wakati wa kupanga mpango (ya awali) wakati wa kutekeleza mpango (ya kati) na wakati mpango unapofikia mwisho (ya mwisho)

**Taathmini wakati wa mpango (awali)**
Mafunzo ya Haki za Binadamu kwa watekelezaji wa sheria yanaweza kutathminiwa wakati yanaandaliwa. Hii inaweza kujumuisha kufanya uchambuzi wa mahitaji. Huu ni mchecheto ambao fedha na mikakati ya nyenzo inachunguzwa. Hii ni kama vile kuhakikisha gharama ya kupeleka kundi la wakufunzi, kuchagua vifaa vinavyohitajika kwa mafunzo ya watekelezaji wa sheria, mahali pa kufundishia panapofaa na muda wa mafunzo.

Katika ngazi hii hata washiriki watakaofaa kwa mafunzo wanaainishwa. Faida za hatua hii ni nyingi. Hasa itasaidia kupanga nyenzo vizuri, kuandaa vifaa vya kufundishia na kuwaandaa watekelezaji wanaofaa. Aina hii ya tathmini itawaongoza wanaotunga sera na wanaofanya mahesabu ya fedha kufanya mipango yenye uhakika.

Tathmini ya kati – wakati wa utekelezaji mpango wa mafunzo ya Haki za binadamu unaweza kutathminiwa wakati wowote wakati mpango unaendelea.

Hii inaweza kufanyika ili kujihakikishia iwapo mpango bado uko katika mstari wa madhumuni yaliyokusudiwa, kuhakikisha matumizi mazuri ya nyenzo, na kushughulikia masuala yanayoibuka ambayo hayakutarajiwa wakati wa kupanga.

**Tathmini mwishoni mwa utekelezaji wa mpango (ya mwisho)**
Mpango wa mafunzo ya Haki za Binadamu yanaweza pia kutathminiwa mwishoni. Hii inaweza kufanyika hasa kuchunguza matokeo na mafanikio yaliyopatikana, yaani kuhakikisha ni kwa kiasi gani mafunzo hayo yametimiza malengo yaliyotarajiwa, ya kujenga utamaduni wa haki za binadamu na heshima kati ya watekelezaji wa sheria. Tathmini ya aina hii inaweza kuwa na madhumuni ya kujifunza utekelezaji wa mpango uliopita kwa nia ya kutengeneza vigezo vya sehemu inayofuata ya mpango wa mafunzo.

## REJEA

Kwa ufafanuzi zaidi wa ufuatiliaji na tathmini rejea:


1. Donald Kirk Patrick: **Supervisory Training and Evelopment. 1970**

## SEHEMU YA IV

**Kiambatanisho I**

# ORODHA YA HATI RASMI ZA KIMATAIFA ZA HAKI ZA BINADAMU (INTERNATIONAL INSTRUMENTS) NA SHERIA ZA NCHI

**Hati rasmi za kisheria zilivyonukuliwa katika mwongozo huu.**

Kwa zile zisizo na tafsiri ya kiswahili zitaandikwa kwa lugha ya kiingereza kwa vile vitapatikana kwa lugha hiyo. Kwa zile zenye tafsiri vitaandikwa kwa kiswahili au lugha zote zitatumika:-

- Tamko la Kimataifa la haki za Binadamu - Azimio la Umoja wa Mataifa 217 A III ya 10 Desemba 1948
- Mkataba wa Kimataifa wa haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni.
- (International Covenant on Economic Social and Cultural Rights, G. A. Resolution 2200A (XXI) of 16 December 1996.
- Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa. International Covenant on Civil and Political Rights G A resolution 2200 A (XXI) of 16th December 1966)
- Optional Protocal to the International Covenant on Civil and Political Rights - G A resolution 2200 (XXI) of 16 December 1966. (Mkataba Nyongeza)
- Tamko la Vienna na Mpango wa Utekelezaji
  25 June 1993 A Conf 157/24 Cap 111 (Vienna Declaration and Programme of Action)
- Vipimo vya Masharti Muhimu ya Jinsi ya Kuwatendea Wafungwa, Azimio la halmashauri ya kiuchumi na kijamii 663 (XXIV) ya 31 ñ Julai 1957 (Standard Minimum Rules for the Treatment of Prisoners, Economic and Social Council Resolution)
- Taratibu za utekelezaji unaofaa wa masharti muhimu ya jinsi ya kuwatendea wafungwa, Azimio la halmashauri ya kiuchumi na kijamii 1984 / 47 ya 25 Mei 1984. (Procedures for the effective implementation of the standard minimum rules for the treatment of prisoners, economic and social council resolution)
- Chombo cha Misingi ya Ulinzi kwa Watu Wote Walio Watika Aina Yeyote ya Ufungwa au Kuwekwa Kizuizini. Azimio la Baraza kuu 43 / 173 ya Desemba 1988. (Body of Principles for the Protection of all Persons under any Form of Detention or Imprisonment G. A Resolution 43 / 173 of December 1998)
- Misingi Muhimu ya Jinsi ya Kuwatendea Wafungwa. Azimio la Baraza Kuu 45 / 11 ya tarehe 14 Desemba 1990
- Azimio la Ulinzi kwa Watu Wote Dhidi ya Kuteswa na Kutendewa Ukatili, Unyama au Vitendo Vyovyote vya Udhalilishaji au Adhabu. Azimio la Baraza Kuu 39 / 46 ya Desemba 1984.
  (Declaration on the Protection of all Persons From Being Subjected to Torture and

Other Cruel, Inhuman or Degrading Treatment or Punishment G. A Resolution 39 / 44 of 10th December 1984)

- Mkataba wa Kimataifa Dhidi ya Mateso au Aina Nyingine ya Ukatili, Unyama au Udhalilishwaji au Adhabu Azimio la Umoja wa Mataifa 39 / 46 ya 10 Desemba 1984.
  (Convention Against Torture and Other Inhuman or Degrading Treatment on Punishment)
- Miongozo ya utekelezaji unaofaa wa kanuni za mienendo ya watekelezaji wa sheria. Taarifa ya nane ya kongamano Sura 1 kifungu B 2
  (Guidelines for the effective implementation of the Code of Conduct for law enforcement officials 8th Congress report)
- Vipimo vya Umoja wa Mataifa vya Masharti Muhimu Katika Utekelezaji wa sheria na haki kwa watoto. (Masharti ya beijing) Azimio la Baraza Kuu 40 / 33 ya 29 Novemba 1985.
- Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto
  Azimio la Baraza Kuu 44 / 25 Novemba 1989
- Masharti ya Umoja wa Mataifa ya Ulinzi kwa Watoto Walionyimwa Uhuru - Azimio la Baraza Kuu 45 / 113 ya 14 Desemba 1990.
  (United Nation Rules for the Protection of Juveniles Deprived of their Liberty - G.A Resolution 45 / 113 of 14th December 1990)
- Tamko la Misingi Muhimu ya Haki na Sheria kwa Waathirika wa Makosa ya Jinai na Matumizi Mabaya ya Mamlaka.
  Azimio la Baraza Kuu 40 / 34 ya 29 November 1985. (Declaration of Basic principle of Justice for victims of Crime and abuse of power G. A 40 / 34 of 29th November 1985)
- Azimio la Ulinzi kwa Watu Wote Wanaopotea kwa Mpango Maalum wa Utekelezaji. Azimio la Baraza Kuu 47 / 133 ya 18 Desemba 1992.
  (Declaration on the Protection of All Persons From Enforced Disappearance G. A resolution 47 / 133 of 18th December 1992.
- Mkataba Kuhusu Hadhi ya Wakimbizi, 28 July 1981
  (Convention Relating to the Status of Refugees New York 28th July 1981)
- Nyongeza ya Mkataba Kuhusu Hadhi ya Wakimbizi New York 28 September 1954
  (Protocol Relating to the Status of Refugees New York)
- Azimio Kuhusu Haki za Binadamu za Watu Ambao si Raia wa Nchi Wanamoishi. Azimio la Baraza Kuu 40 / 44 ya 13 Desemba 1985 (Declaration on the Human Rights of Individuals who are not nationals of the country in which they live. G. A Resolution 40 / 144 of 13th December 1985)
- Mkataba wa Kiafrika Kuhusu Haki za Watu na Haki za Binadamu. Makala ya Umoja wa nchi huru za kiafrika CAB / LEG 67 / 3 / REV.
  (African Charter on Human and Peopleís Rights OAU document CAB / LEG 67 / 3 REV)

## SHERIA ZA NCHI

- Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 (kama ilivyorekebishwa)
- Sheria ya Mienendo ya Makosa ya Jinai Na 9 ya 1985
- Sheria ya Watoto na Vijana Wadogo Sura 13
- Sheria ya Jeshi la Polisi Sura 332
- Amri za Jumla za Polisi (PGO)
- Sheria ya Kanuni za Adhabu Namba 16
- Sheria ya Magereza Tanzania Na 34 / 1967
- Miongozi ya Magereza (Utawala wa Magereza) 1968
- Sheria ya Wakimbizi 1998

# TAMKO LA KIMATAIFA LA HAKI ZA BINADAMU

*Ilikubaliwa na kutangazwa na baraza kuu la Umoja wa Mataifa kupitia Azimio 217 A (III) ya tarehe 10 Desemba 1948.*

## DIBAJI

***Kwa kuwa*** imetambulika kuwa utu wa asili na usawa na haki zisizoondosheka za watu wote wa familia ya kibinadamu ni msingi wa uhuru, haki na amani ulimbwenguni,

***Kwa kuwa*** kutotilia maanani na kudharau haki za binadamu kumesababisha matendo ya kikatili yaliyofedhehesha dhamira ya wanadamu na mwanzo wa ulimwengu ambao binadamu watafaidi uhuru wa kujieleza na imani na uhuru dhidi ya hofu na uhitaji vimetangazwa kama maazimio ya hali ya juu ya watu wa kawaida.

***Kwa kuwa*** pamoja na kwamba inamlazimu binadamu pale anapokosewa haki zake kwa udhalimu na ukandamizaji kuamua kupambana, bado ni lazima haki za binadamu zilindwe na sheria.

***Kwa kuwa*** ni muhimu kukuza maendeleo ya urafiki kati ya mataifa,

***Kwa kuwa*** watu wa Umoja wa Mataifa kwenye Mkataba unaounda Umoja huo wamethibitisha imani yao katika haki za Binadamu za msingi, katika utu na thamani ya utu na haki sawa kati ya wanaume na wanawake na wamethamiria kukuza maendeleo ya kijamii na vipimo vizuri zaidi vya maisha katika uhuru zaidi,

***Kwa kuwa*** uelewa wa pamoja wa haki hizi na uhuru ni wa muhimu sana ili kufanikisha kiapo hiki,

Kwa hiyo sasa,

**Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa**
Linatamka azimio hili la  Kimataifa la Haki za Binadamu kama kipimo cha pamoja cha kufanikisha kwa watu wote na mataifa yote matokeo kwamba kila mtu na kila chombo katika jamii, kikiweka tamko hili katika mawazo wakati wote watapigania kwa kufundisha na kuelimisha ili kukuza heshima ya haki hizi na uhuru na kwa hatua za kimaendeleo za kitaifa na kimataifa ili kupata utambuzi na ulinzi unaofaa kimataifa kati ya watu wa mataifa wanachama na kati ya watu walio ndani ya mataifa hayo.

## IBARA YA 1:

Binadamu wote wamezaliwa huru na kwa usawa katika hadhi na haki. Wametunukiwa ufahamu na hisia na wanapaswa kuchukuliana katika hali ya kindugu.

## IBARA YA 2

Kila mtu anastahili kupata haki na uhuru ulioelezwa katika tamko hili bila kujali tofauti za kiasili, rangi, jinsia, lugha, dini, siasa au maoni mengine, utaifa, au asili ya kijamii, mahali pa kuzaliwa au hali nyingine yeyote. Zaidi ya hapo hakuna ubaguzi utakaofanyika kwa sababu za kisiasa, mamlaka za kisheria au hadhi ya kimataifa ya nchi ambayo mtu anatoka, bila kujali kama hiyo nchi ni huru, au inatawaliwa bado.

## IBARA YA 3

Kila mtu ana haki ya kuishi, kuwa huru na kulindwa utu wake.

## IBARA YA 4:

Hakuna mtu atakayewekwa utumwa au katika hali ya kitumwa, utumwa na biashara ya utumwa vinakatazwa katika aina zake zote.

## IBARA YA 5:

Hakuna mtu anayepaswa kupata mateso au ukatili au kutendewa katika hali ambayo itamdhalilisha au kumshushia hadhi yake au kuadhibiwa.

## IBARA 6:

Kila mtu ana haki ya kutambuliwa kama binadamu mbele ya sheria.

## IBARA 7:

Watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanapaswa kulindwa na sheria bila ubaguzi. Wote wanapaswa kulindwa sawa dhidi ya ubaguzi ambao utapingana na tamko hili au uchochezi utakaopelekea kuleta ubaguzi wa aina hiyo.

## IBARA 8:

Kila mtu ana haki ya kupatiwa ufumbuzi kwenye vyombo vya sheria vya taifa kwa matendo yoyote yanayomnyima haki zake za msingi zilizotolewa na katiba ya nchi au sheria.

## IBARA 9:

Hakuna mtu atakayefungwa au kuwekwa kizuizini au kuhamishwa nchini kinyemela [ bila mpango] au [bila kufuatia sheria].

## IBARA 10:

Kila mtu anastahili kusikilizwa kwa haki na usawa mbele ya vyombo vya sheria visivyo

vya kibaguzi katika kuamua haki na wajibu wake na kwenye kusikilizwa kwa kosa la jinai analoshtakiwa.

### IBARA 11

1. Mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kosa la jinai atahesabiwa kuwa hana hatia mpaka pale itakapothibitika kishera mbele ya sheria kwenye mahakama ya wazi akiwa amejitetea.
2. Hakuna mtu atakayepatikana na hatia kwa jambo ambalo si kosa mbele ya sheria kwenye sheria za nchi au za kimataifa wakati alipotenda jambo hilo. Pia mtu yeyote hapaswi kupewa adhabu kubwa kuliko ile iliyotajwa kisheria wakati alipokosa.

### IBARA 12:

Hakuna mtu atakayeingiliwa katika faragha yake, familia, nyumbani kwake au mawasiliano yake wala hakuna mtu atakayeshambuliwa hadhi yake au heshima aliyonayo. Kila mtu ana haki ya kulindwa na sheria dhidi ya kuingiliwa au kushambuliwa huko.

### IBARA 13:

1. Kila mtu ana haki ya uhuru wa kwenda atakako na kuishi katika mipaka ya nchi yake.

2. Kila mtu ana haki ya kuondoka nchi yeyote hata nchi yake na pia haki ya kurejea katika nchi yake.

### IBARA 14:

1. Kila mtu ana haki ya kutafuta na kufaidi hifadhi dhidi ya kuuawa katika nchi nyingine.
2. Haki hii haitakuwepo pale ambapo mtu amehukumiwa kwa mujibu wa sheria kwa makosa yasiyo ya kisiasa au kwa matendo kinyume na malengo na misingi ya Umoja wa Mataifa.

### IBARA 15:

1. Kila mtu ana haki ya uraia.
2. Hakuna mtu atakayenyimwa uraia au haki ya kubadili uraia bila sababu.

### IBARA 16:

1. Wanaume na wanawake waliotimiza umri wa utu uzima, bila kujali asili, uraia au dini wana haki ya kuoa au kuolewa na kuanzisha familia, wanapaswa kuwa na haki sawa katika ndoa, wakati ndoa inaendelea na hata ikivunjika.
2. Ndoa itafungwa tu pale wanandoa watakapokuwa wamekubali kwa hiari yao wenyewe.

3. Familia ni kundi la msingi na la asili la jamii na inapaswa kulindwa na jamii pamoja na taifa.

## IBARA YA 17:

1. Kila mtu ana haki ya kumiliki mali yake binafsi au kwa pamoja na watu wengine.
2. Hakuna mtu atakayenyangíanywa mali yake bila sababu.

## IBARA YA 18:

Kila mtu ana haki ya uhuru wa kufikiri, hisia na dini, hii haki inajumuisha uhuru wa kubadili dini au imani, na uhuru wa kuielezea dini yake au imani kwa kufundisha kutenda au kuabudu na kuikiri iwapo ni kibinafsi au katika jumuiya na watu wengine.

## IBARA YA 19:

Kila mtu ana uhuru wa kutoa maoni yake na kujieleza. Haki hii inajumuisha uhuru wa kusimamia maoni yake bila kuingiliwa na kutafuta, kupokea na kutoa habari na mawazo kupitia vyombo vya habari vya aina yoyote bila kujali mipaka.

## IBARA YA 20:

1. Kila mtu ana haki ya uhuru wa kukutana na watu wengine na kujumuika kwa amani.
2. Hakuna mtu atakayelazimishwa kujiunga na umoja wowote.

## IBARA YA 21:

1. Kila mtu ana haki ya kushiriki katika serikali ya nchi yake moja kwa moja au kupitia wawakilishi waliochaguliwa kwa uhuru.
2. Kila mtu ana haki ya kupata kwa usawa huduma za umma katika nchi yake.
3. Matakwa ya watu ndio yatakuwa msingi wa mamlaka ya serikali, hii itajieleza katika chaguzi za vipindi na za kweli ambazo zitakuwa kwa wote na kwa haki na zitafanyika kwa kura ya siri au kwa njia huru za kura zinazofanana na hiyo.

## IBARA YA 22:

Kila mwana jamii, ana haki ya kupata hifadhi ya jamii na anapaswa kupokea kupitia juhudi za taifa na ushirikiano wa kimataifa na kulingna na shirika au rasilimali za kila taifa kwenye haki za uchumi, jamii na utamaduni ambazo ni lazima kwa hadhi yake na maendeleo dhahiri ya utu wake.

## IBARA YA 23:

1. Kila mtu ana haki ya kufanya kazi, uhuru wa kuchagua kazi, mazingira ya kazi yenye haki na ya mafao na kulindwa dhidi ya kutokuwa na kazi.
2. Kila mtu bila ubaguzi ana haki ya kulipwa sawa kwa kazi aliyoifanya.
3. Kila mtu aliyeajiriwa ana haki ya kupata malipo ya haki yatakayomhakikishia yeye na familia yake kuishi kama binadamu na kuongezewa ikibidi aina nyingine za hifadhi ya jamii.

4. Kila mtu ana haki ya kuanzisha au kujiunga katika vyama vya wafanyakazi kulinda maslahi yake.

## IBARA YA 24:

Kila mtu ana haki ya kupumzika na starehe pamoja na muda maalum wa saa za kazi na vipindi vya likizo zenye malipo.

## IBARA YA 25

1. Kila mtu ana haki ya kuwa na hali nzuri ya maisha inayofaa kiafya na maisha yake na ya familia yake kwa ujumla ikijumlishwa na chakula, mavazi, malazi na haki ya kupata tiba na hifadhi za jamii zilizo za lazima. Pia haki ya kuhifadhiwa anapokosa ajira, akiwa mgonjwa, mlemavu, mjane, mzee au hali nyingine yeyote itakayoyatishia maisha yake kwa kiasi asichoweza kujisaidia.
2. Hadhi ya kuwa mama na utoto vinapaswa kupewa uangalizi maalum na kusadiwa. Watoto wote hata kama wamezaliwa ndani au nje ya ndoa wafaidi sawa ulinzi wa kijamii.

## IBARA YA 26:

1. Kila mtu ana haki ya kupata elimu. Elimu itatolewa bure, angalau elimu ya msingi. Elimu ya msingi ni lazima kwa kila mtu. Elimu ya ufundi na elimu ya juu itakuwepo kwa ujumla na iwe inapatikana kwa wote kulingana na uwezo.
2. Elimu ielekezwe katika kumkuza mtu kufikia hadhi kamili kama binadamu na kuimarisha heshima ya haki za binadamu na misingi ya uhuru wa mtu. Ikuze maelewano, uvumilivu na urafiki kati ya mataifa, asili na vikundi vya dini na iendeleze hatua za Umoja wa Mataifa wa kulinda amani,
3. Wazazi wana haki ya mwanzo kuchagua aina ya elimu itakayotolewa kwa watoto wao.

## IBARA YA 27:

1. Kila mtu ana haki iwapo atapenda kushiriki katika masuala ya utamaduni katika jumuiya yake kufurahia sanaa na kushiriki katika maendeleo ya kisayansi na mafao yake.
2. Kila mtu ana haki ya ulinzi wa utu wake na vitu vyake anavyopendelea vinavyotokana na sayansi, fasihi, vitu vya sanaa ambavyo yeye ndio mwandishi wake.

## IBARA YA 28

Kila mtu anastahili utulivu katika jamii yake na kimataifa ambapo haki na uhuru wake uliotolewa katika tamko hili utapatikana.

## IBARA YA 29

1. Kila mtu ana wajibu kwa jumuia ya ambayo uhuru na maendeleo kamili ya utu wake yanaweza kupatikana.
2. Katika kufaidi haki na uhuru kila mtu atakuwa chini ya mipaka ya sheria kwa ajili ya kupata uwezo wa kuheshimiwa kwa haki hizo na uhuru wa watu wengine na pia kulingana na utu, taratibu za jamii nzima katika jamii ya kidemokrasia.
3. Hizi haki na uhuru uliotolewa zisitumiwe kinyume na misingi na malengo ya umoja wa mataifa.

## IBARA YA 30:

Hakuna chochote katika tamko hili kinachopaswa kutafsiriwa na nchi yeyote, kundi la watu au mtu yeyote ili kumaanisha kuharibu haki na uhuru uliotolewa.

# KANUNI ZA MIENENDO YA WATEKELEZAJI WA SHERIA

*Ilipitishwa na Azimio la Baraza Kuu Namba 34 / 169 ya 17 Desemba 1929*

## Ibara ya I

Watekelezaji wa sheria mara zote wanapaswa kutimiza wajibu waliopewa kwa kuzingatia sheria, kwa kuhudumia umma na kuwalinda watu wote dhidi ya matendo maovu, wakizingatia wajibu mkubwa unaohitajika katika taaluma yao.

*Ufafanuzi*

(a) Neno "watekelezaji wa Sheria" linajumuisha maafisa wote wa sheria walioteuliwa au kuchaguliwa ambao wanatekeleza mamlaka ya polisi hasa uwezo wa kukamata au kuweka watu kizuizini.

(b) Katiba ya nchi ambamo kazi za polisi zinatekelezwa na mamlaka ya kijeshi wakiwa katika sare au la, au na makundi ya usalama wa taifa, tafsiri ya 'watekelezaji wa sheria' itawajumuisha na maafisa kwenye ngazi hizo.

(c) Huduma kwa jamii inakusudiwa kujumuisha hasa kutoa huduma ya msaada kwa wana jamii au sababu nyingine za dharura zinazohitaji msaada wa haraka.

(d) Sehemu hii haikusudiwi kuhusika tu na vurugu, ukatili na matendo yenye kuleta madhara bali inakusudiwa katika uwanja mzima wa yanayokatazwa chini ya sheria ya jinai. Inagusa hata matendo ya watu ambao hawana uwezo wa kufanya makosa ya jinai.

## Ibara 2

Katika kutekeleza kazi zao watekelezaji wa sheria wanapaswa kuheshimu na kulinda utu wa watu na kuendeleza na kusimamia haki za binadamu za watu wote.

*Ufafanuzi*

(a) Haki za Binadamu zinazotajwa ni zile zilizoainishwa na kulindwa na sheria za nchi na za kimataifa. Katika vyombo vya kimataifa vinavyohusika ni Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu, Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na kisiasa, Tamko la Ulinzi kwa Watu Wote Dhidi ya Mateso, na Aina Nyingine za Ukatili au Kudhalilishwa au Adhabu. Tamko la Umoja wa Mataifa la Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi wa Rangi, Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi wa Rangi. Mkataba wa Kimataifa wa Kudidimiza na Adhabu za Makosa ya Ubaguzi wa Rangi, Mkataba wa Kuzuia na Adhabu za Makosa ya Jinai ya Uuaji wa Makundi, Vipimo vya Masharti Muhimu ya Jinsi ya Kuwatendea Wafungwa, na Mkataba wa Vienna wa Mahusiano ya Kibalozi.

(b) Ufafanuzi wa kitaifa wa Ibara hii lazima uoneshe vifungu vya kikanda au kitaifa vinavyoainisha na kulinda haki hizi.

## Ibara ya 3

Watekelezaji wa sheria watatumia nguvu pale tu ambapo ni lazima sana na kwa kiwango kinachohitajika katika utekelezaji wa kazi yao.

*Ufafanuzi*

(a) Ibara hii inasisitiza kwamba matumizi ya nguvu kwa watekelezaji wa sheria yawe ni suala lisilo la kawaida, Wakati Ibara hii inamaanisha kuwa watekelezaji wa sheria wanaweza kuruhusiwa kutumia nguvu kama jambo la lazima katika mazingira ya kuzuia uhalifu au katika kusaidia kwenye ukamataji wa wahalifu au watuhumiwa wa uhalifu kwa mujibu wa sheria, bado hakuna nguvu inayopaswa kutumika zaidi ya mipaka hii.

(b) Sheria za nchi kwa kawaida zinazuia matumizi ya nguvu kulingana na msingi wa uwiano. Ifahamike kwamba msingi huo wa sheria za nchi uheshimiwe katika kutafsiri ibara hii. Kwa vyovyote vile Ibara hii isitafsiriwe kuwa inaruhusu matumizi ya nguvu yasiyolingana na madhumuni halali yanayokusudiwa.

(c) Matumizi ya silaha yanahesabika ni hatua ya kuzidi mpaka. Kila jitihada zifanyike kuzuia matumizi ya silaha hasa dhidi ya watoto. Kwa ujumla silaha zisitumike labda tu pale ambapo mhalifu anatumia silaha kupinga au pale ambapo anahatarisha maisha ya watu wengine na njia nyingine hazitoshi kumzuia au kumkamata mtuhumiwa huyo. Kila mara ambapo silaha itatumika, taarifa lazima iandaliwe mara moja na ipelekwe kwa mamlaka inayohusika.

## Ibara ya 4

Masuala ya siri yanayojulikana na watekelezaji wa sheria yanapaswa kubaki siri isipokuwa pale tu ambapo ni lazima yatolewe kwa ajili ya utekelezaji au mahitaji ya lazima katika haki na sheria.

*Ufafanuzi*

Kwa mujibu wa kazi zao watekelezaji wa sheria wanaweza kupata taarifa ambayo inahusu maisha binafsi ya watu au inayoweza kuwa na madhara katika maslahi au heshima ya mtu. Tahadhari kubwa inapaswa ichukuliwe kuhusiana na matumizi ya taarifa kama hiyo. Itapasa ifichuliwe tu katika kutekeleza kazi na kwa haja ya kutimiza sheria na haki. Kuifichua habari hiyo kwa sababu nyingine si sahihi.

## Ibara ya 5

Mtekelezaji yeyote wa sheria hapaswi kumtesa, kumfanyia ukatili au kumdhalilisha au kumuadhibu mtu wala hapaswi kutoa amri au kutoa utetezi wa masuala kama hofu ya vita, usalama wa taifa, vurugu za kisiasa au dharura yoyote ya umma kama sababu ya kumtesa, kufanya ukatili, unyama au udhalilishaji au adhabu.

*Ufafanuzi*

(a) Hili zuio linatokana na Tamko kuhusu ulinzi wa watu wote dhidi ya kuteswa, kutendewa ukatili, kinyama au kudhalilishwa au kuadhibiwa, lililopitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa.
"[tendo kama hilo ni] kosa kwa utu wa mtu na lazima lilaaniwe kwa kukiuka madhumuni ya mkataba wa umoja wa mataifa na kama ukiukaji wa Haki za Binadamu na misingi mikuu ya uhuru yaliyoainishwa katika Tamko la Haki za Binadamu [Na vyombo vingine vya kimataifa vya Haki za Binadamu]."

(b) Tamko hilo linatafsiri mateso kuwa ni mateso ......... Ni tendo lolote ambalo linaleta uchungu na maumivu yawe ni ya kimwili au kiakili na tendo hilo limefanywa kwa makusudi na afisa wa umma au mtu aliyeamrishwa na afisa huyo kwa nia ya kupata habari kutoka kwa anayetendewa au mtu mwingine au kumlazimisha kukiri kosa alilofanya au analoshukiwa kufanya au kumdhalilisha yeye au mtu mwingine. Haijumuishi maumivu au machungu yanayotokana na hali halisi wakati wa utekelezaji wa sheria inayolingana na vipimo vya masharti muhimu ya jinsi ya kuwatendea wafungwa.

(c) Neno, unyama, au matendo ya udhalilishaji na adhabu hayajatafsiriwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lakini yanapaswa kupewa tafsiri pana iwezekanavyo katika kulinda ukiukaji unaoweza kuwa wa kimwili au kiakili.

## Ibara ya 6

Watekelezaji wa sheria wanapaswa kuhakikisha ulinzi wa kutosha wa afya ya watu walio chini ya ulinzi wao na hasa wanapaswa kuchukua hatua za haraka kuwapatia uangalizi wa afya pale zinapohitajika.

*Ufafanuzi*

(a) "Uangalizi wa Afya" ambao unamaanisha huduma zinazotolewa na mhudumu wa Afya ikiwa ni pamoja na mganga (Daktari au wenye ujuzi wa utibabu) na wanaotoa huduma za afya wasio madaktari lazima upatikane pale unapohitajika au unapoombwa.

(b) Ingawa wahudumu wa afya wanaweza kuwa ni sehemu katika mfumo wa utekelezaji wa sheria, watekelezaji wa sheria lazima watilie maanani maamuzi yao wanapopendekeza kuhusiana na mfungwa na apatiwe matibabu yanayofaa na ya kutosha au washauriane na watendaji wengine wa tiba kutoka nje ya mfumo wa utekelezaji wa sheria.

(c) Inaeleweka kuwa watekelezaji wa sheria watawapatia uangalizi wa afya waathirika wa ukiukwaji wa sheria au ajali zilizotokana na ukiukwaji wa sheria.

## Ibara ya 7

Watekelezaji wa sheria hawapaswi kutenda tendo lolote linalohusiana na rushwa. Na wanapaswa kwa nguvu zote kupinga na kupambana na vitendo vya aina hiyo.

*Ufafanuzi*

(a) Tendo lolote la rushwa kama yalivyo matendo yeyote ya kukiuka mamlaka ni kinyume cha taaluma ya watekelezaji wa sheria. Sheria lazima ichukue mkondo wake kikamilifu dhidi ya mtekelezaji wa sheria atakayetenda tendo la rushwa, kwa vile serikali haiwezi kutegemea kutekeleza sheria kati ya raia wake iwapo haitaweza au haitatekeleza sheria dhidi ya watendaji wake na kati ya vyombo vyake vya utendaji.

(b) Ingawa taarifa ya rushwa inapaswa kueleweka kwa mujibu wa sheria za nchi, lazima ieleweke pia kuhusisha matendo au kutotendwa kwa tendo wakati wa utekelezaji wa kazi au kuhusiana na utekelezaji wa kazi kutokana na zawadi, ahadi au motisha zilizoombwa au kupokelewa au upokeaji usio wa halali wa vitu hivyo baada ya tendo hilo kufanyika au kutofanyika.

(c) Maelezo ya "matendo ya rushwa" yaliyotajwa hapo juu yaeleweke kuwa yanajumuisha jaribio la kupata rushwa.

## Ibara ya 8

Watekelezaji wa sheria wanapaswa kuheshimu sheria na kanuni hizi. Na pia wanapaswa kuzuia na kupinga kwa nguvu zote ukiukwaji wa sheria kulingana na uwezo wao wote. Watekelezaji wa sheria ambao wana sababu ya kuamini ukiukwaji wa kanuni hizi umetokea au unategemea kutokea watoe taarifa ya jambo hilo kwa wakuu wao na inapobidi kwa vyombo vingine vinavyohusika au vyombo vyenye mamlaka ya kuchunguza au ya kurekebisha.

*Ufafanuzi*

(a) Kanuni hizi lazima zizingatiwe pale ambapo zimeingizwa katika sheria na utendaji nchini. Iwapo sheria na utendaji nchini ina vifungu vikali zaidi ya vilivyo kwenye kanuni hii, hivyo vifungu vikali zaidi ndivyo vitumike.

(b) Ibara hii inajaribu kuweka uwiano kati ya haja ya nidhamu ya ndani ya chombo cha sheria ambamo usalama wa watu kwa kiasi kikubwa unategemea kwa upande mmoja, na haja ya kushughulikia ukiukwaji wa haki za msingi, upande mwingine watekelezaji wa sheria wanapaswa kutoa taarifa katika mkondo wa uongozi na kuchukua hatua nyingine za kisheria nje ya mkondo wa uongozi pale ambapo hakuna njia nyingine inayofaa. Ieleweke kuwa watekelezaji wa sheria hawatapata adhabu za kiutawala au nyinginezo kwa sababu wametoa taarifa kuwa ukiukwaji wa kanuni umetokea au unategemea kutokea.

(c) Neno..... "vyombo vinavyohusika au vyombo vyenye mamlaka vya kuchunguza au kurekebisha" lina maana mamlaka yeyote au chombo kilichopo kwa mujibu wa

sheria, iwapo ni cha ndani ya mfumo wa utekelezaji wa sheria au cha kibinafsi chenye mamlaka ya kisheria, kidesturi au mamlaka nyingine yeyote kuchunguza malalamiko yanayotokana na ukiukwaji ya yale yaliyomo kwenye kanuni hizi.

(d) Katika nchi nyingine vyombo vya habari vinaonekana kama watekelezaji wa uchunguzi wa malalamiko kama yanavyoelezwa katika kifungu (c) hapo juu. Hivyo basi, watekelezaji wa sheria wanaweza kuwa na sababu kama njia ya mwisho na kulingana na sheria na desturi za nchi zao na kulingana na Ibara ya 4 ya kanuni hizi kuwasilisha ukiukwaji mbele ya umma kwa kupitia vyombo vya habari.

(e) Watekelezaji wa sheria ambao wanazingatia yaliyomo katika kanuni hizi wanastahili heshima, kuungwa mkono na ushirikiano toka kwa jamii na kwa chombo cha utekelezaji wa sheria wanachokihudumia na kutoka katika taaluma nzima ya utekelezaji wa sheria.

OHCHR LIBRARY
7915